SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

KUHUSU UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA HOSPITALI KUMI ZA WILAYA NA HOSPITALI MOJA YA MKOA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

RIPOTI YA MDHIBITI NA UKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA HOSPITALI KUMI ZA WILAYA NA HOSPITALI MOJA YA MKOA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR
2 Mtaa wa Tume, 71125 Kilimani Zanzibar, S.L.P 258
Simu/Nukushi: +255 24 223 400, Barua Pepe: info@ocagz.go.tz
Tovuti: www.ocagz.go.tz

MAREJEO NAM: CAC.132/385/01/4 **TAREHE: 26 MACHI, 2024**

MHE. DKT HUSSEIN ALI MWINYI,
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI,
AFISI YA RAIS IKULU,
S.L.P. 437,
ZANZIBAR, TANZANIA.

KUH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA KIUFUNDI WA UJENZI WA HOSPITALI KUMI ZA WILAYA NA MOJA YA MKOA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Ripoti ya Mwaka inayohusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Hospitali Kumi za Wilaya na Hospitali Moja ya Mkoa kwa kipindi wa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023.

Naomba kuwasilisha.

Ahsante.

....

DKT. OTHMAN ABBAS ALI
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU
WA HESABU ZA SERIKALI
ZANZIBAR.

AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka.

Dira

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi.

Dhamira

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa.

MISINGI YA MAADILI YA UKAGUZI

1. **Uaminifu** – Kuhakikisha Afisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia Sheria.
2. **Uadilifu** – Kuwa ni Afisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.
3. **Kuwa Huru** – Kuwa ni Afisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa Sheria.
4. **Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi** – Kuwa ni Afisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.
5. **Kutunza Siri** – Kuwa ni Afisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.
6. **Uwazi na Uwajibikaji** – Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma

YALIYOMO

YALIYOMO V

ORODHA YA MAJADWELI X

ORODHA YA PICHA XIII

VIFUPISHO XIV

SHUKURANI XV

DIBAJI VIFUPISHO XVII

SURA YA KWANZA 1

1.0 UTANGULIZI 1

1.1 HISTORIA YA MRADI 1

1.2 CHIMBUKO LA UKAGUZI 1

1.3 LENGO LA UKAGUZI 2

1.4 UPEO WA UKAGUZI 3

1.5 VIGEZO VYA TATHMINI 4

1.6 MBINU ZA UKUSANYAJI NA UCHAMBUZI WA TAARIFA 4

1.7 MCHAKATO WA UTHIBITISHAJI WA TAARIFA 8

1.8 VIWANGO VILIVYOTUMIKA KWA UKAGUZI 9

1.9 MUUNDO WA RIPOTI YA UKAGUZI 9

SURA YA PILI 11

2.0 MIFUMO YA USIMAMIZI WA UJENZI WA HOSPITALI UNGUJA NA PEMBA 11

2.1 UTANGULIZI 11

2.2 SHERIA HUSIKA 11

2.3 AINA ZA MIKATABA (NJIA ZA UNUNUZI) ZILIZOTUMIKA KATIKA UJENZI 12

2.4 MAJUKUMU NA WAJIBU WA WAHUSIKA WA MRADI 13

2.5 UTARATIBU WA KUSIMAMIA UJENZI WA HOSPITALI 15

2.6 MIRADI YA UJENZI ILIYOKAGULIWA 15

SURA YA TATU 17

3.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI KUMI ZA WILAYA NA HOSPITALI MOJA YA MKOA 17

3.1 UTANGULIZI 17

3.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA UPANGAJI WA MIPANGO YA UJENZI WA MIRADI YA HOSPITALI 18

3.3 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USIMAMIZI WA UNUNUZI KATIKA UJENZI WA MIRADI YA HOSPITALI 31

3.4 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USIMAMIZI WA MKATABA 38

SURA YA NNE 52

4.0 MATOKEO UKAGUZI KUHUSU MRADI WA UJENZI WA HOSPITALI YA MKOA LUMUMBA 57

4.1 UTANGULIZI 57

4.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA UPANGAJI WA MIPANGO YA UJENZI WA MIRADI YA HOSPITALI YA MKOA LUMUMBA 57

4.3 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA MCHAKATO WA UNUNUZI WA UPATIKANAJI WA MKANDARASI KWA AJILI YA UJENZI WA HOSPITALI YA MKOA WA LUMUMBA 58

4.4 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA 60

SURA YA TANO 64

5.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA KITOGANI 64

5.1 UTANGULIZI 64

5.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UPANGAJI WA MIPANGO YA UJENZI WA MIRADI YA HOSPITALI YA WILAYA KITOGANI 64

5.3 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USIMAMIZI WA UNUNUZI KATIKA UJENZI WA MIRADI YA HOSPITALI 65

5.4 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA 65

SURA YA SITA 67

6.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA MWERA PONGWE 67

6.1 UTANGULIZI 67

6.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA UPANGAJI WA MIPANGO YA UJENZI WA MIRADI YA HOSPITALI YA WILAYA MWERA PONGWE 67

6.3 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USIMAMIZI WA UNUNUZI KATIKA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA MWERA PONGWE 68

6.4 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA 69

SURA YA SABA 72

7.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA MBUZINI 72

7.1 UTANGULIZI 72

7.2 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA 72

SURA YA NANE 76

8.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA CHUMBUNI 76

8.1 UTANGULIZI 76

8.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA UPANGAJI WA MIPANGO YA UJENZI WA MRADI WA HOSPITALI YA WILAYA CHUMBUNI 76

8.3 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA MCHAKATO WA KUWAPATA WAKANDARASI WA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA CHUMBUNI... 77

8.4 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA... 77

SURA YA TISA ... 80

9.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA MAGOGONI ... 80

9.1 UTANGULIZI ... 80

9.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA UPANGAJI WA MIPANGO YA UJENZI WA MRADI WA HOSPITALI YA WILAYA MAGOGONI... 80

9.3 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA... 81

SURA YA KUMI ... 83

10.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA KIVUNGE ... 83

10.1 UTANGULIZI ... 83

10.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA MCHAKATO WA KUWAPATA WAKANDARASI WA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA KIVUNGE... 83

10.3 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA... 85

SURA YA KUMI NA MOJA ... 87

11.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA PANGATUPU... 87

11.1 UTANGULIZI ... 87

11.2 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA... 87

SURA YA KUMI NA MBILI 90

12.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA VITONGOJI 90

12.1 UTANGULIZI 90

12.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA MCHAKATO WA KUWAPATA WAKANDARASI KWA AJILI YA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA VITONGOJI 90

12.3 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA........ 92

SURA KUMI NA TATU 95

13.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA MICHEWENI 95

13.1 UTANGULIZI 95

13.2 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA........ 95

SURA YA KUMI NA NNE 99

14.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA KINYASINI 99

14.1 UTANGULIZI 99

14.2 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USIMAMIZI WA UNUNUZI KATIKA UJENZI WA MIRADI YA HOSPITALI 99

14.3 MATOKEO YA UKAGUZI YANAYOHUSIANA NA USIMAMIZI WA MKATABA........101

ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli Nambari 1: Nyaraka zilizokaguliwa na Sababu za Kukaguliwa...............5

Jadweli Nambari 2: Vipengele Muhimu vilivyozingatiwa wakati wa kutembelea miradi.. 6

Jadweli Nambari 3: Majaribio yaliopendekezwa kufanywa, Mbinu na Lengo la Majaribio 7

Jadweli Nambari 4: Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi..................... 10

Jadweli Nambari 5: Kanuni za Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo 11

Jadweli Nambari 6: Miongozo ya Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo 11

Jadweli Nambari 7: Hospitali kumi (10) za Wilaya na Moja (1) ya Mkoa 14

Jadweli Nambari 8: Hali ya Ujenzi wa Hospitali kumi za Wilaya na Hospitali moja ya Mkoa 15

Jadweli Nambari 9: Gharama za ziada zinazotoka na na kushindwa kufanya vyema Tathmini ya Mradi 19

Jadweli Nambari 10: Taarifa zilizolipiwa lakini hazikuweza kuandaliwa............20

Jadweli Nambari 11: Hali halisi ya utengenezaji wa michoro baada ya kukamilika kwa kazi za ujenzi (As-Built).........................22

Jadweli Nambari 12: Hali halisi ya Mipango ya upimaji na ukabidhi.................24

Jadweli Nambari 13:Vigezo ambavyo Wizara wametumia katika utengenezaji wa viluva.. 26

Jadweli Nambari 14: Tofauti baina ya muundo unaohitajika kwa mujibu wa miongozo na muundo kwa mujibu wa ujenzi uliofanyika 28

Jadweli Nambari 15: Tofauti katika ongezeko la fedha baina ya Makadirio na Tuzo 30

Jadweli Nambari 16: Bei ya mkataba kabla na baada ya kupunguza ukubwa wa ujenzi (sqm) 32

Jadweli Nambari 17: Mchanganuo wa Mzabuni aliezawadiwa bila ya kuwa vigezo.. 33

Jadweli Nambari 18: Tofauti ya gharama baina ya wazabuni waliopewa mikataba dhidi ya wazabuni waliopendekezwa na kamati ya tathmini.. 35

Jadweli Nambari 19: Uchambuzi wa Gharama za Mradi Zilizojumuishwa katika dhamana ya utekelezaji wa kazi (Perfomance security). 37

Jadweli Nambari 20: Kiasi kilicholipwa kwa ajili ya uandaaji wa michoro baada kukamilika kwa ujenzi kwa kila mradi 38

Jadweli Nambari 21: Kuchelewa kuwasilisha michoro mara baada ya Ujenzi kukamilika hadi tarehe ya Ukaguzi 31 Julai, 2023.......... 39

Jadweli Nambari 22: Malipo ya vifaa ambavyo havikupimwa wala kukabidhiwa.. 41

Jadweli Nambari 23: Gharama za tozo ya adhabu ya kushindwa kumaliza kazi kwa wakati.. 42

Jadweli Nambari 24: Idadi ya miezi na kiasi husika cha kuzuiliwa kwa ucheleweshwaji wa kuwasilisha mpango kazi kwa kila mwezi.. 43

Jadweli Nambari 25: Kiasi kilicholipwa kwa kazi ambazo mkandarasi hajazitekeleza 46

Jadweli Nambari 26: Faida na Mahudhurio ya Jumla kwa Wakandarasi Wakuu 48

Jadweli Nambari 27: Mkataba na kiasi cha kulipwa cha bima na dhamana (dhamana ya utekelezaji kazi) 50

Jadweli Nambari 28: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba 52

Jadweli Nambai 29: Bei ya Zabuni iliyowasilishwa kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba 53

Jadweli Nambari 30: Uchambuzi wa wakati halisi wa mshauri elekezi juu ya usimamizi wa mradi wa ujenzi 56

Jadweli Nambari 31: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kitogani 58

Jadweli Nambari 32: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe.. 60

Jadweli Nambari 33 : Mchanganuo wa Mzabuni aliezawadiwa bila ya kuwa sifa.. 62

Jadweli Nambari 34: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mbuzini.. 64

Jadweli Nambari 35: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Chumbuni 67

Jadweli Nambari 36: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Magogoni... 70

Jadweli Nambari 37: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kivunge 72

Jadweli Nambari 38: Mzabuni aliezawadiwa bila ya kuwa vigezo 73

Jadweli Nambari 39: Maelezo ya Mkataba za Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Pangatupu 75

Jadweli Nambari 40: Taarifa za Mkataba za Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Vitongoji 77

Jadweli Nambari 41: Mchanganuo wa Mzabuni aliezawadiwa bila ya kuwa vigezo.. 78

Jadweli Nambari 42: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Micheweni.. 80

Jadweli Nambari 43: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kinyasini 83

Jadweli Nambari 44: Marekebisho ya makosa wakati wa tathmini ya zabuni... 84

ORODHA YA PICHA

Picha Nambari 1: Wahusika wanaohusika katika Ujenzi wa Jengo la Hospitali..13

Picha Nambari 2:Mchakato wa Ujenzi wa Majengo ya Hospitali......................14

Picha Nambari 3: Nyufa za kimuundo zilizobainika katika Hospitali ya Wilaya Vitongoji..17

Picha Nambari 4: Nyufa za Muunganiko wa pamoja kati ya ghorofa ya kwanza Zege (Slab) na Bimu Beam...18

VIFUPISHO

OCAGZ	Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar
WHO	Shirika la Afya Duniani
TZS/Tsh	Shilingi ya Tanzania
IMF	Shirika la Fedha la Kimataifa
COVID-19	Ugonjwa wa Virusi vya Corona
VO’s	Maagizo ya Tofauti
BoQs	Makisio ya Gharama za Ujenzi
MoHZ	Wizara ya Afya Zanzibar
ZPPDA	Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar
APP	Mpango wa Ununuzi wa Mwaka
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
GN	Government Notice
AG	Mwanasheria Mkuu
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
ZRB	Bodi ya Mapato Zanzibar
GCC	Masharti ya Jumla ya Mkataba
SCC	Masharti Maalum ya Mkataba
PPR	Kanuni za Ununuzi wa Umma
IPCs	Cheti cha Malipo ya awali
ZBA	Wakala wa Majengo Zanzibar
ZBS	Taasisi ya Viwango Zanzibar

SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za mara kwa mara anazoendelea kuzichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo na kutoa maelekezo katika kufanya maboresho juu ya dosari mbali mbali zinazobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na hatua anazoendelea kuzichukua kutokana na hoja za ukaguzi zinazoibuliwa kuhusu matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, pamoja na watendaji mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano yao wanayokupatia katika utekelezaji wa majukumu yako ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu ya nchi yao.

Shukurani zangu za dhati ziende kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kujitolea kwa dhati kujadili na kutoa mapendekezo pamoja na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na Serikali kutokana na dosari zilizojitokeza na kuibuliwa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuniunga mkono na kunipa nguvu katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kikatiba pamoja na jitihada zake anazozichukuwa katika kusimamia misingi ya utawala bora na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji.

Vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kwa Bodi ya Utumishi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kusimamia maadili na nidhamu ya wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kazi za ukaguzi.

Kwa namna ya kipekee niwashukuru wafanyakazi wote wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Afisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Tanzania Audit Corporation (TAC Associates), Price Waterhouse Coopers (PWC), pamoja na Ernst & Young (EY) kwa kufanya kazi za ukaguzi kwa mashirikiano na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na juhudi zao mbali mbali walizozichukuwa hadi kukamilika kwa ripoti hii.

Mwisho, niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitatambua jukumu la vyombo mbali mbali vya habari kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuutambulisha Umma juu ya kazi zinazofanywa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo matokeo na mapendekezo ya kazi hizo huwasilishwa kwa jamii kupitia vyombo mbali mbali vya habari.

Natumia fursa hii, kuwasihi wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuwa na moyo wa dhati katika kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mashirikiano kwa ajili ya siku zijazo ili kuendelea kudumisha nidhamu ya Afisi ya Mdhibiti katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora.

DIBAJI

Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Hospitali kumi za Wilaya na Hospitali moja ya Mkoa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kwa kila mwaka.

Ripoti hii imejumuisha mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi ambapo matokeo, athari na mapendekezo ya ukaguzi yameelekezwa kwa Wizara ya Afya Zanzibar.

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma pamoja na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na hatimae taarifa hizo kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji.

Ripoti hii inajumuisha mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wangu ambapo nilifanya tathmini kwa kuangalia taarifa za fedha pamoja na nyaraka mbalimbali zinazohusiana na Ujenzi huo, taratibu za michakato ya manunuzi na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni mbali mbali.

Napenda kuchukuwa fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wangu kwa kujitolea kufanya kazi ya Ukaguzi pamoja na Uongozi wa Wizara ya Afya Zanzibar kwa kutoa ushirikiano wao mzuri ambao umewezesha kukamilisha Ripoti hii kwa wakati.

....

DKT. OTHMAN ABBAS ALI

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

ZANZIBAR

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 HISTORIA YA MRADI

Tarehe 11 Machi 2020, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza rasmi mripuko wa Ugonjwa wa Virusi vya Corona (COVID-19) kuwa ni janga la kimataifa. Kufuatia hatari zilizotarajiwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi bilioni 230 kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweza kukabiliana kikamilifu na athari za janga hilo. Fedha hizo zilipatikana kutoka Shirika Fedha la Duniani (IMF) chini ya Mpango wa Mikopo ya Haraka (RCF).

Mripuko wa UVIKO-19 nchini umeathiri afya ya jamii kwa kiasi kikubwa. Ugonjwa huo ulisababisha athari mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kiafya katika jamii hali iliyoongeza mahitaji ya ujenzi wa hospitali Zanzibar. Ili kudhibiti kuenea kwa virusi vya ugonjwa huo kwa kuimarisha uwezo wa kudhibiti na kuzuia maambukizi, awali Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitenga jumla ya shilingi bilioni 78.5 kwa Sekta ya Afya kwa ajili ya ujenzi wa hospitali na usambazaji wa vifaa tiba.

Hivyo, kutokana na maendeleo yaliyotajwa hapo juu, na nia ya Serikali, nilifanya Ukaguzi wa Kiufundi katika Ujenzi wa hospitali moja (1) ya Mkoa na hospitali kumi (10) za Wilaya kwa lengo la kubaini kama Ujenzi wa miundombinu/majengo ya Hospitali ulitekelezwa ipasavyo kwa mujibu wa viwango vilivyokubalika na kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha.

Miradi hiyo ilihusisha ujenzi wa Hospitali moja (1) ya Mkoa iliyopo Lumumba Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na Hospitali kumi (10) za Wilaya kama ifuatavyo kwa Wilaya ya Mjini (Chumbuni), Wilaya ya Magharibi A (Mbuzini), Wilaya ya Magharibi B (Magogoni), Wilaya ya Kaskazini A (Kivunge), Wilaya ya Kaskazini B (Pangatupu), Wilaya ya Kati (Mwera Pongwe), Wilaya ya Kusini (Kitogani), Wilaya ya Chake Chake (Vitongoji), Wilaya ya Micheweni (Micheweni) na Wilaya ya Wete (Kinyasini).

1.2 Chimbuko la Ukaguzi

Uamuzi wa kufanya Ukaguzi huu wa Ufundi ulihamasishwa kutokana na mambo makuu mawili ambayo ni kiwango kikubwa cha gharama kwa mujibu wa fedha zilizotumika pamoja na dosari za kiutendaji zilizoripotiwa zinazohusiana na gharama za juu kwa kulinganisha na ubora wa kazi za ukarabati zilizofanyika katika mradi. Maelezo ya taarifa hizo ni kama inavyoonekana hapo chini:-

1.2.1 Kiasi Kikubwa cha Fedha Kilichotengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali moja ya Mkoa na Hospitali kumi za Wilaya

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga jumla ya shilingi bilioni 72.8 kwa Wizara ya Afya kwa ajili ya ujenzi wa hospitali kumi (10) za Wilaya na hospitali moja (1) ya Mkoa ili kuhakikisha upatikanaji wa Afya ya umma katika Wilaya zote.

Hivyo, fedha hizo lazima zisimamiwe vyema ili kutambua thamani halisi ya fedha zilizotumika na kufikiwa lengo la kutoa afya kwa jamii.

1.2.2 Utendaji wa Miradi Iliyoripotiwa kuhusiana na ongezeko la Gharama na Udhaifu katika Ubora wa Kazi

Kutengwa fedha za ziada za jumla ya shilingi bilioni 19.2 kutoka kwenye kiasi cha mkataba wa awali wa jumla ya shilingi bilioni 72.8 ambazo zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za Wilaya na hospitali ya Mkoa. Vile vile, kulikuwa na matatizo ya utendaji yaliyoripotiwa kuhusiana na ubora wa majengo yaliyojengwa. Matatizo haya yalihusishwa zaidi na usimamizi duni wa miradi na mikataba, udhibiti wa ubora, kutofuata sheria na Kanuni za manunuzi pamoja na uandaaji na usanifu wa miradi usiojitosheleza.

1.3 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Afya imesimamia ipasavyo ujenzi wa Hospitali ya Mkoa na Wilaya ili kuhakikisha kuwa majengo yaliyojengwa yana viwango vinavyotakiwa ili kuongeza kasi ya utoaji wa huduma bora za afya katika ngazi za Mikoa na Wilaya.

1.3.1 Malengo maalum/mahsusi ya Ukaguzi

Malengo maalum/mahsusi ya ukaguzi yalikuwa ni kutathmini kama;

(a) Upangaji/Uandaaji na usanifu wa miradi ya ujenzi wa majengo na vifaa vya hospitali za Mkoa na Wilaya ulifanyika ipasavyo ili kuwezesha utoaji wa huduma bora za afya;

(b) Taratibu za Manunuzi na utoaji wa Mikataba/Tuzo kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake zilizingatiwa;

(c) Mifumo na taratibu za usimamizi wa muda, gharama na ubora wa mradi zilikuwa na ufanisi;

(d) Shughuli za Ujenzi wa Hospitali za Mikoa na Wilaya na ununuzi wa vifaa tiba zilizingatia masharti na viwango vyote vya kiufundi; na

(e) Ufuatiliaji wa kazi za ujenzi ulifanyika ipasavyo na kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

1.4 Upeo wa Ukaguzi

Wizara ya Afya ina jukumu la kutunga na kutekeleza sera kuhusu sekta ya afya nchini na usimamizi wa jumla wa kazi za ujenzi katika Hospitali za Rufaa, Hospitali za Mikoa, Hospitali za Wilaya na vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya Jamii. Hasa, Wizara ya Afya ina jukumu la kupanga/kuandaa, kusanifu, ununuzi, na usimamizi wa mikataba ya kazi za ujenzi wa Hospitali za Mikoa na Wilaya zinazofadhiliwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Ukaguzi huu ulihusisha Miaka miwili ya Fedha kuanzia 2021/2022 hadi 2022/2023 na ulishughulikia awamu zote kuanzia kuanzishwa kwa mradi hadi Kukabidhiwa na kuanza kutumika. Kipindi hicho cha Ukaguzi kilichaguliwa ili kuruhusu wakaguzi kupima kama malengo yaliyokusudiwa ya kujenga Hospitali yamefikiwa na kutoa hitimisho na Mapendekezo ya ukaguzi kulingana na matokeo.

Jumla ya vipengele vitatu vya usimamizi wa mradi vilizingatiwa ambavyo ni kupanga na kubuni, mchakato wa ununuzi na utoaji wa kandarasi, na usimamizi wa kandarasi katika suala la ubora, muda, upeo na usimamizi wa gharama.

Vipengele hivi vimefafanuliwa zaidi hapo chini;

(a) Kipengele cha Upangaji na Usanifu

Chini ya kipengele hiki, timu ya ukaguzi ilitathmini, ufanisi wa upembuzi yakinifu, usanifu na utayarishaji wa Hati za Zabuni ili kuthibitisha endapo muundo wa majengo umefanyika kama ulioidhinishwa.

(b) Kipengele cha Mchakato wa Ununuzi na Utoaji wa Mikataba

Hii ilihusisha kutathmini ni kwa kiasi gani watekelezaji wa mradi walisimamia mchakato wa manunuzi kwa namna ambayo inapunguza gharama na kutathmini endapo manunuzi yalikuwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Lengo lilikuwa ni kutathmini uzingatiaji wa taratibu za ununuzi na utoaji wa mikataba kama ilivyoainishwa katika Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji Mali za Umma ya 2016 na Kanuni zake za mwaka 2020.

(c) Usimamizi wa Muda, Ubora, Gharama na Upeo wa mradi

Chini ya kipengele hiki, Timu ya Ukaguzi ilitathmini utoshelevu wa mifumo na michakato ya kudhibiti muda, gharama na ubora wa mradi. Hii ni pamoja na kupanga utekelezaji wa mradi unaohusu tathmini ya mradi, upembuzi yakinifu, usanifu, makadirio ya muda na gharama na vipengele vya kuanzisha mradi. Masuala ya usimamizi wa mikataba, usimamizi na ufuatiliaji wa wakandarasi na washauri elekezi, ufungaji wa mradi na ukabidhi kazi kama ulitathminiwa.

Pia, ukaguzi ulitathmini ni kwa kiwango gani watekelezaji walihakikisha kuwa miradi inazingatia mahitaji ya mradi (specifications) na viwango. Zaidi ya hayo, ukaguzi ulitathmini ubora wa majengo pamoja na vifaa vilivyotumika.

Vilevile, Timu ya Ukaguzi ilitathmini ufanisi katika ulipaji na matumizi ya fedha za miradi iliyopangwa/iliyoidhinishwa, utoshelevu na ufanisi wa udhibiti wa ndani wa fedha na uzingatiaji wa Kanuni elekezi za fedha na masharti ya malipo.

1.5 Vigezo vya Tathmini

Vigezo vya tathmini vilivyotumika vilitokana na Mikataba, Manunuzi na sheria za fedha, viwango vinavyosimamia ujenzi kama vile Viwango vya Ujenzi vya British (British Standard) na maagizo kutoka Serikalini juu ya matumizi ya fedha za Mfuko wa dharura wa ahueni ya UVIKO - 19.

1.6 Mbinu za Ukusanyaji na uchambuzi wa Taarifa

1.6.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Taarifa

Ukaguzi ulitumia mbinu nne za ukusanyaji wa taarifa ambazo ni, mapitio ya nyaraka, mahojiano, kutembelea maeneo ya miradi pamoja na kupima ubora wa kazi zilizokamilika. Mbinu hizo ni kama zilivyoelezewa hapo chini:-

a) Mapitio ya Nyaraka

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa nyaraka mbalimbali ili kupata na kutathmini utoshelevu wa tathmini ya mahitaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa mradi. Taarifa zilizokusanywa kupitia nyaraka zilizopitiwa zilitumika kuthibitisha taarifa zilizopatikana kutokana na mahojiano na maafisa wanaohusika na utekelezaji wa mradi. Nyaraka zilizopitiwa ziliwezesha Timu ya Ukaguzi kukusanya taarifa za kina na za kuaminika na kuja na Mapendekezo ya Ukaguzi yenye kujenga.

Nyaraka zilizopitiwa ni zile zinazoangukia ndani ya muda uliowekwa na Ukaguzi wa Kiufundi yaani, 2021/2022 na 2022/2023, na zile zinazohusiana na upangaji wa miradi, manunuzi, fedha na nyaraka zinazohusiana na utendaji. Nyaraka maalum zilizokaguliwa na sababu za ukaguzi zimefafanuliwa katika jadweli hapo chini;

Jadweli Nambari 1: Nyaraka zilizokaguliwa na Sababu za Kukaguliwa

Aina ya Nyaraka	Sababu za Kukaguliwa
Ripoti za Usanifu na Mipango.	• Usahihi na Ukamilifu wa Mahesabu ya Usanifu. • Usahihi na Ukamilifu wa Vigezo vya Kiufundi. • Kufaa kwa muundo katika suala la uchumi na utendaji kazi (kufikia madhumuni). • Usahihi na Ukamilifu wa nyaraka za makadirio ya gharama (BoQ), uwiano, michoro na maelezo ya kiufundi.
Nakala za Mkataba (nyaraka ya makubaliano, Barua ya Kukubalika, Zabuni ya Mkandarasi, Masharti Maalum ya mkataba (SCC), Masharti ya jumla ya mkataba (GCC), Michoro, Nyaraka za makadirio ya gharama (BoQ), mazungumzo ya awali kabla ya mkataba).	Kutambua/kujua masharti yaliyotolewa katika mkataba yanayohusiana na malipo, ongezeko la gharama, masuala ya urejeshaji (recovery issues), masuala ya kuzuia fedha, Makosa yatayojitokeza, ucheleweshaji wa malipo na namna ya kushughulikia madai, n.k. Pia, kuangalia ikiwa bidhaa zote zimewekewa bei kwa usahihi.
Vyeti (cheti cha malipo ya muda, cheti cha kukamilika kwa mradi (cheti cha kukamilika kazi na cheti cha mwisho)	Kuweza kutathmini endapo fedha zilithibitishwa. Kuangalia jinsi ongezeko la gharama pamoja na madai yameshughulikiwa. Pia kuangalia jinsi bidhaa za ziada zilivyoshughulikiwa.
Taarifa za fedha za mwisho wa mradi (kufungwa kwa kandarasi, kurejesha dhamana, kurejesha pesa zilizozuiliwa wakati wa malipo ya kila awamu.	Kuangalia kama taarifa za fedha za mwisho wa mradi zimeandaliwa. Ikiwa malipo yote yaliolipwa yanaendana na gharama za mkataba, ongezeko la gharama na madai yote yaliodhinishwa.
Mpango Kazi uliofanyiwa mapitio/ maboresho.	Ili kutathmini ikiwa inaambatana na muda ulioongezwa.
Taarifa za muda za Maendeleo ya Mradi.	Kutathmini ni nini kimefanyika hadi tarehe ya mkutano wa eneo la mradi na changamoto zilizobainika wakati wa utekelezaji wa mradi.
Kumbukumbu za Malipo/ Vyeti.	Ili kubaini jumla ya kiasi halisi cha fedha kilicholipwa.
Maelekezo ya eneo la mradi.	Kutathmini maagizo yaliyotolewa na kupima athari za gharama na muda.
Kumbukumbu za Mkutano katika eneo la mradi na mikutano ya uongozi.	Kutathmini masuala yanayohusiana na gharama, wakati na ubora.

Aina ya Nyaraka	Sababu za Kukaguliwa
Ongezeko la gharama za mradi (Variation Orders)	Kutathmini ongezeko la gharama za mradi zilizotolewa na sababu zake juu ya gharama na wakati. Pia, kutathmini endapo ongezeko la mradi lilikubaliwa na pande zote mbili kwa mujibu wa mkataba.
Mawasiliano ya Mradi (Correspondence)	Kutathmini masuala yanayohusiana na gharama, muda na ubora wa mradi
Taarifa za upimaji	Kutathmini ubora wa miradi ya ujenzi iliyotekelezwa ikiwa ilikidhi vipimo vilivyotakiwa. Taarifa za upimaji zilizokaguliwa; Bomba na vifaa vya kazi, viluva, kokoto, uimara wa nguzo, saruji na pia, matokeo ya taarifa za upimaji wa vifaa vilivyowekwa kama pampu za maji na Jenereta.
Taarifa za Fedha	Kuangalia ufanisi wa utoaji na matumizi ya fedha za mradi zilizoidhinishwa, utoshelevu na ufanisi wa udhibiti wa ndani wa kifedha wa fedha za mradi na kuzingatia Kanuni za Fedha na masharti ya malipo yaliyoonyeshwa katika nyaraka za mradi husika. Ukaguzi wa taarifa za fedha za mwisho ikiwa ni pamoja na ongezeko la thamani na madai.

Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi, 2023

b) Mahojiano

Wakaguzi walifanya mahojiano na mwakilishi wa mshauri elekezi; Wakandarasi, Wahandisi kutoka Wizara ya Afya na Mjumbe wa Kamati ya Tathmini kutoka Wizara ya Afya.

Mahojiano yalifanywa ili kupata maelezo ya ziada kutokana na nyaraka zilizopitiwa pamoja na kutembelea miradi.

c) Kutembelea miradi

Taarifa zilizokusanywa kupitia mahojiano, ukaguzi wa nyaraka iliongezewa na kutembelea maeneo ya miradi ili kuthibitisha kile kilichotekelezwa. Timu ya Ukaguzi wa Kiufundi ilifanya ziara katika maeneo ambayo majengo ya hospitali yalijengwa kuanzia tarehe 17 hadi 26 Julai, 2023 ili kukagua na kuhakiki kazi halisi iliyofanyika na kufahamu ubora na ufanisi wa kazi zilizotekelezwa.

Wakati wa ziara ya maeneo ya miradi, Timu ya Ukaguzi wa Kiufundi ilihakiki ikiwa kazi zilizotekelezwa ziliendana na vipimo, michoro, Nyaraka za makadirio ya gharama (BoQ) na masharti yoyote yaliyotolewa katika mkataba.

Jadweli hapo chini linaonesha vipengele muhimu vilivyozingatiwa wakati wa kutembelea maeneo ya miradi.

Jadweli Nambari 2: Vipengele Muhimu vilivyozingatiwa wakati wa kutembelea miradi

Kipengele	Masuala yaliozingatiwa	Sababu ya kutathmini
Muda	Kasi ya utekelezaji ikiwa inaendana na mkataba	Kuwa na mtazamo wa hali ya utekelezaji
Ubora wa vifaa vya ujenzi	Vifaa (Majengo, vifaa vilivyowekwa n.k.)	Kuona ufanisi wa vifaa vilivyojengwa.
Ubora wa kazi zilizokamilika	Ufanyaji kazi wa vifaa	Ufanisi wa majengo na vifaa vilivyojengwa
Usimamizi wa Mradi	Upatikanaji wa wafanyakazi muhimu	Kupima kama mradi unasimamiwa
	Uwepo wa zana na vifaa vinavyohitajika	Ili kuhakikisha ubora wa kazi

Chanzo: Uchambuzi wa wakaguzi, 2023

d) Upimaji wa sehemu zilizojengwa za majengo

Wakaguzi walifanya majaribio ya uharibifu (destructive tests) na yasiyo ya uharibifu (non-destructive tests) ili kubaini kama kazi iliyojengwa inakidhi ubora uliobainishwa na kubainisha ubora wa miundombinu iliyojengwa kulingana na mahitaji yaliyowekwa. Jadweli hapa chini linatoa uchanganuzi wa majaribio yaliofanywa wakati wa kutembelea miradi.

Jadweli Nambari 3: Majaribio yaliopendekezwa kufanywa, Mbinu na Lengo la Majaribio

Namba	Kipengele	Aina za Majaribio	Lengo na Mbinu ya Majaribio	Njia za kufanya majaribio
1	Ubora wa Kazi.	Uimara wa nguzo/zege.	Upimaji wa uimara wa majengo	Majaribio yasiyo ya uharibifu.
2	Idadi, ukubwa, na nafasi zilitakiwa baina ya nondo na nondo.	Upimaji wa ubora kwa kutumia vifaa maalum (scanning).	Ili kuangalia ikiwa nondo (re-bars) zilizotumiwa zililingana na ukubwa ulioainishwa, idadi na nafasi ya baina ya nondo na nondo.	Upimaji wa ubora kwa kutumia kifaa maalum cha 'Re-bar Detector'.

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kulingana na majaribio yaliofanywa, 2023

1.6.2 Mbinu za Uchambuzi wa Taarifa

Taarifa zilizopatikana kupitia mahojiano, mapitio ya nyaraka pamoja na taarifa zilizobainishwa kutokana na majaribio ya ukaguzi zilichambuliwa kwa kutumia mbinu zifuatazo:-

i. Uchambuzi wa maelezo ambapo taarifa zilizopatikana zilichanganuliwa kwa kutumia 'pie chart', grafu na kuorodheshwa katika majadweli; na

ii. Uchambuzi wa mwenendo ambapo wakaguzi walichanganua mwelekeo wa taarifa zilizotolewa katika kipindi cha miaka tofauti na kuangalia kama suala lililo changanuliwa lilikuwa likipungua au kuongezeka.

Taarifa za ubora zilizopatikana kutokana na mahojiano, ukaguzi wa nyaraka za mradi na taarifa zilizobainishwa kutokana na kutembelea maeneo ya miradi na majaribio yaliofanywa, zilichanganuliwa kwa kuzilinganisha na kuzihusisha kwa lengo la kuweza kupata hitimisho lililojitosheleza.

Zaidi ya hayo, taarifa zilizofanikiwa kukusanywa na ukaguzi ziliweza kuchanganuliwa kuweza kupima ufanisi katika utekelezaji wa mradi.

1.7 Mchakato wa Uthibitishaji wa Taarifa

Taasisi iliyokaguliwa ilipewa fursa ya kupitia rasimu ya ripoti na kutoa maoni yake kuhusu ukweli wa taarifa zilizowasilishwa humo. Wizara ya Afya ilithibisha usahihi wa taarifa na takwimu zilizotumika na kuwasilishwa katika ripoti hii ya ukaguzi.

ile vile, rasimu ya ripoti iliwasilishwa kwa ajili ya mapitio ya ubora na uongozi ili kuboresha uwasilishaji na uchanganuzi wa ripoti na kuthibitisha usahihi wa mambo yaliyowasilishwa katika ripoti.

1.8 Viwango vilivyotumika kwa Ukaguzi

Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) vilivyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI). Viwango hivi vinahitaji kuwa ukaguzi ufanyike ili kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa ili kutoa msingi unaofaa wa matokeo na hitimisho kulingana na malengo ya ukaguzi. Kwa ujumla, kwa kuzingatia malengo ya ukaguzi, ushahidi uliopatikana ulitoa msingi wa kuridhisha wa matokeo na hitimisho lilifikiwa.

1.9 Muundo wa Ripoti ya Ukaguzi

Muundo wa Ripoti hii umegawika katika sura kumi na tano kama ifuatavyo:-

Sura ya Kwanza	Inawasilisha Utangulizi wa Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi.
Sura ya Pili	Inawasilisha Mifumo ya Usimamizi wa Ujenzi wa Hospitali Unguja na Pemba.
Sura ya Tatu	Inawasilisha Matokeo ya jumla ya Ukaguzi wa ujenzi wa Hospitali kumi za Wilaya na moja ya Mkoa.
Sura ya Nne	Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi wa Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba.
Sura ya Tano	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Kitogani.
Sura ya Sita	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe.
Sura ya Saba	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya Mbuzini
Sura ya Nane	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Chumbuni.
Sura ya Tisa	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Magogoni
Sura ya Kumi	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Kivunge.
Sura na Kumi na moja	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Pangatupu.
Sura ya Kumi na mbili	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Vitongoji.
Sura ya Kumi na tatu	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Micheweni.
Sura ya Kumi na nne	Inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Kinyasini.

SURA YA PILI

2.0 MIFUMO YA USIMAMIZI WA UJENZI WA HOSPITALI UNGUJA NA PEMBA

2.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mfumo wa Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo mapya ya Hospitali ya Mkoa na Wilaya. Sura hii inashughulikia sera na mfumo wa kisheria, wahusika wakuu ikiwa ni pamoja na majukumu yao makuu na uhusiano; taratibu za upangaji, ununuzi, ujenzi, fedha na ukamilishaji wa Majengo ya Serikali.

2.2 Sheria husika

Sheria na Kanuni mbalimbali zinazosimamia ujenzi wa Majengo ya Serikali zimefafanuliwa hapa chini:-

2.2.1 Sheria za Serikali zinazohusika na ujenzi wa majengo ya Serikali

Kuna sheria tofauti zinazosimamia shughuli za ujenzi Zanzibar kama zilivyowasilishwa katika jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 4: Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi

Sheria	Matumizi
Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, 2016	Sheria inatoa taratibu za kufuatwa wakati wa ununuzi hadi utekelezaji wa mradi. Sheria hii inamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa manunuzi yote yatafuata Sheria na Kanuni kama ilivyoelekeza
Sheria ya Kodi Mwaka 2008 (R.E)	Kusimamia masuala yote yanayohusiana na kodi
Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma, 2016	Kusimamia masuala yote yanayohusiana na malipo na idhini.

Chanzo: Mapitio ya sheria, 2023

2.2.2 Kanuni za Sheria zinazohusika na ujenzi wa majengo ya Serikali

Kuna Kanuni tofauti zinazoelekeza kuhusiana na udhibiti wa gharama katika ujenzi wa majengo ya Serikali, kama ilivyoelezwa katika jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 5: Kanuni za Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo

Kanuni	Matumizi ya Kanuni	Taasisi ya uwajibikaji
Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma, 2020.	Kanuni hii inasisitiza kwamba taasisi zote za ununuzi zinapaswa kudumisha taarifa zote, nyaraka na masuala yote yanayohusiana na kazi za ujenzi. Inaeleza zaidi kwamba taasisi za ununuzi zinapaswa kuhakikisha kuwa kazi zinakamilika kwa wakati kulingana na vipaumbele vya taasisi ya ununuzi kwa mafanikio ya kutosha ya uchumi na ufanisi.	Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma.
Kanuni za Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB) za mwaka 2018.	Inahitaji mradi wowote unaohusisha ujenzi, ufungaji au mabadiliko ya muundo wowote au kazi zingine zilizounganishwa nayo, kwa matumizi ya umma, ya kibiashara au vinginevyo kutekelezwa / kutolewa na mkandarasi aliyesajiliwa.	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi.
Kanuni za Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji majengo-2014.	Kanuni zinahitaji Wakadiriaji majengo kutoa huduma za awali na za msingi kuhusu udhibiti wa gharama.	Bodi ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji wa Majengo.

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka katika Kanuni za Usimamizi zilizopitiwa katika ujenzi wa Majengo Zanzibar, 2023.

Jadweli Nambari 6: Miongozo ya Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo

Sheria	Matumizi
Miongozo ya Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB - By-Laws)	Miongozo hii inahitaji kazi za ujenzi zitekelezwe kwa mujibu masharti yaliyowekwa katika Mkataba na kufuata taratibu za Ujenzi. Bodi pia ina jukumu la kuhakikisha kuwa mwenendo wa kitaaluma unadumishwa na kuzingatiwa na Wahandisi waliosajiliwa.

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye miongozo ya Usimamizi iliopitiwa katika ujenzi wa Majengo Zanzibar, 2023.

2.3 Aina za Mikataba (Njia za Ununuzi) zilizotumika katika Ujenzi

Kulikuwa na njia kuu mbili zilizotumika katika ujenzi wa hospitali kama zilizoelezwa hapa chini.

2.3.1 Njia ya Asili ya Ununuzi/Mpangilio wa Mikataba ya Viwango

Mpangilio wa mkataba wa viwango ni mkataba ambao wazabuni huwasilisha viwango vya makadirio ya kiasi kama ilivyoainishwa katika Nyaraka za makadirio ya ujenzi (BoQ) ambazo ni sehemu ya nyaraka za zabuni na ambazo bei ya jumla inatokana na mkusanyiko wa kiasi kilichotolewa kulingana na idadi na viwango hivyo. Malipo chini ya mkataba wa viwango huamuliwa na kipimo cha kiasi halisi kilichokamilishwa na kwa viwango kama zabuni inavyoelekeza. Katika aina hii ya mkataba ongezeko lolote la kazi litapelekea kuongezeka kwa gharama za ziada kwa mkandarasi na gharama zozote ambazo zitatokana na vitu visivyotarajiwa wakati wa kusanifu litapelekea kuongezeka kwa gharama kwa Wizara ya Afya.

2.4 Majukumu na Wajibu wa Wahusika wa Mradi

Wizara ya Afya ndiyo mhusika mkuu mwenye dhamana ya kusimamia ujenzi wa Hospitali za Rufaa, Hospitali za Mikoa, Hospitali za Wilaya na vituo vya afya nchini. Pia, jukumu la uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya ujenzi wa hospitali zote Zanzibar.

Watendaji wakuu wamegawanyika hasa katika makundi makuu matano, ambayo ni Wizara ya Afya, Mkandarasi, Mshauri Elekezi, Mamlaka ya Udhibiti (ZPPDA, AQRB, ERB) na mfadhili wa miradi ambayo ni Wizara ya Fedha. Wajibu wa kila Mhusika umefafanuliwa katika picha hapo chini.

Picha Nambari 1: Wahusika wanaohusika katika Ujenzi wa Jengo la Hospitali

Mfadhili wa Miradi

- **Wizara ya Fedha na Mipango**
- Wajibu wa kuhakikisha upatikanaji wa fedha.

Wizara ya Afya

- Wajibu wa kufanya upembuzi yakinifu, uandaaji wa hadidu Rejea, uelekezaji wa fedha za ujenzi wa miradi, kusimamia mchakato wa upatikanaji wa wahandisi na washauri elekezi na wasimamizi wa utekelezaji wa miradi. Pia, kuwalipa wahandisi na washauri elekezi kulingana na kazi iliyofanyika.

Mshauri elekezi

- Mshauri elekezi wa Ujenzi wa Majengo ya Serikali ana wajibu wa kuandaa kazi za awali inayojumuisha upembuzi yakinifu, uandaaji na kuisaidia Wizara ya Afya kipindi cha mchakato wa Zabuni, na kusimamia kazi za Ujenzi.

Wahandisi

- Wahandisi wanawajibu wa kutekeleza kazi za Ujenzi kulingana na nyaraka za Mkataba. Jukumu lao ni kuhakikisha ubora wa vifaa vinavyotumika katika Ujenzi kulingana na masharti ya Mkataba.

Mamlaka za Usimamizi

- **Architect and Quantity Surveyors Registration board**
- Reesponsible for monitoring and regulating Architects and Quantity Surveyors activities, conducts and consulting firms in Tanzania.

- **Engineers Registration Board**
- Responsible for monitoring and regulating engineering activities and conducts of engineers and engineering consulting firms in Tanzania

- **Contractors Registration Board**
- Contractors Registration Board (CRB), registers local and foreign contractors working in the construction industry in the country, regulates their activities and conducts, sets out criteria for registration of contractors, verify and ensure that all works are undertaken by registered contractors

- **Public Procurement and Disposal Authority (ZPPDA) is responsible for monitoring the procurement activities**
- Responsible for Monitoring the compliance of public procurement laws and Regulations

2.5 Utaratibu wa kusimamia ujenzi wa hospitali

Miradi ya Ujenzi huanza na uanzishaji wa mradi na upangaji, kubuni michoro, ununuzi, ujenzi, ukamilishaji wa mradi na kumalizika kwa kazi; na uendeshaji na matengenezo ya Majengo ya hospitali. Maelezo ya kila hatua yanaonyeshwa katika picha hapo chini.

Picha Nambari 2: Mchakato wa Ujenzi wa Majengo ya Hospitali



2.6 Miradi ya Ujenzi iliyokaguliwa

Ukaguzi huu ulihusisha hospitali moja (1) ya Mkoa na hospitali kumi (10) za Wilaya kama zifuatavyo:-

Jadweli Nambari 7: Hospitali kumi (10) za Wilaya na Moja (1) ya Mkoa

Namba	Jina la Hospitali	Hadhi ya Hospitali (Mkoa/Wilaya)
1.	Hospitali ya Lumumba	Mkoa wa Mjini Magharibi
2.	Hospitali ya Chumbuni	Wilaya ya Mjini
3.	Hospitali ya Mbuzini	Wilaya ya Magharibi A
4.	Hospitali ya Magogoni	Wilaya ya Magharibi B
5.	Hospitali ya Kivunge	Wilaya ya Kaskazini A
6.	Hospitali ya Pangatupu	Wilaya ya Kaskazini B
7.	Hospitali ya Mwera Pongwe	Wilaya ya Kati
8.	Hospiali ya Kitogani	Wilaya ya Kusini
9.	Hospitali ya Vitongoji	Wiliaya ya Chake Chake
10.	Hospitali ya Micheweni	Wilaya ya Micheweni
11.	Hospitali ya Kinyasini	Wilaya ya Wete

SURA YA TATU

3.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI KUMI ZA WILAYA NA HOSPITALI MOJA YA MKOA

3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Katika utekelezaji wa mradi huu jumla ya shilingi bilioni 72.8 zilitengwa katika Sekta ya Afya kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali kumi za Wilaya na Hospitali moja ya Mkoa, ambapo fedha hizo zilitolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mfuko wa Ahueni UVIKO-19 kama ni mkopo kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Jadweli hapo chini linaonyesha maendeleo ya kazi za ujenzi wa miradi kumi na moja (11) ya hospitali zilizokaguliwa.

Jadweli Nambari 8: Hali ya Ujenzi wa Hospitali kumi za Wilaya na Hospitali moja ya Mkoa

Namba	Jina la mradi	Bei ya Mkataba (Shs.)	Kiasi kilicholipwa hadi Tarehe ya Ukaguzi (Shs.)	Asilimia ya kukamilika kwa kazi
1.	Hospitali ya Wilaya ya Vitongoji	5,038,669,139	6,850,743,540	100
2.	Hospitali ya Mkoa ya Lumumba	24,717,192,531	21,556,123,939	100
3.	Hospitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe	5,071,148,905	6,879,306,982	100
4.	Hospitali ya Wilaya ya Magogoni	4,506,763,921	6,301,300,228	100
5.	Hospitali ya Wilaya ya Kitogani	4,782,843,802	6,659,284,193	100
6.	Hospitali ya Wilaya ya Kinyasini	4,976,732,968	5,921,397,576	100
7.	Hospitali ya Wilaya ya Micheweni	4,800,212,162	6,366,485,502	100
8.	Hospitali ya Wilaya ya Chumbuni	4,371,192,471	6,090,787,118	100
9.	Hospitali ya Wilaya ya Mbuzini	4,516,388,643	6,237,971,135	100
10.	Hospitali ya Wilaya ya Kivunge	4,854,044,142	5,400,495,064	100
11.	Hospitali ya Wilaya ya Pangatupu	4,478,584,783	6,115,992,73	100

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka katika Nyaraka za Mikataba na taarifa za Malipo, 2023

Jadweli hapo juu linaonyesha Ujenzi wa miradi yote hadi kufikia tarehe ya ukaguzi ilikua imekamilika na hatimae Wizara ya Afya ilisimamia kipindi cha uangalizi kulingana na mkataba.

3.2 Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Upangaji wa Mipango ya Ujenzi wa Miradi ya Hospitali

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusiana na upangaji wa kazi za ujenzi wa hospitali kumi na moja (11) mpya zilizojengwa Unguja na Pemba. Wizara ya Afya ilianza rasmi utekelezaji wa mikataba ya ujenzi wa hospitali hizo mnamo Disemba, 2021. Ukaguzi ulibaini dosari zifuatazo katika upangaji wa miradi.

3.2.1 Kutofanyika kwa uchunguzi wa kijiolojia (Geotechnical Investigation) kabla ya ujenzi wa hospitali kumi za Wilaya

Sehemu ya 1 ya British Standard (BS) 5930:2015 inaeleza kua, Lengo Kuu la uchunguzi wa jiolojia (Geotechnical investigation) katika mchakato wa ujenzi ni kuweza kupanga njia bora ya ujenzi, ili kuweza kutathmini na kutoa suluhisho la matatizo pamoja na ucheleweshaji ambao unaweza kutokea wakati wa ujenzi kutokana na changamoto za ardhini, maeneo ambayo maji yanatuama pamoja na changamoto nyenginezo, kwa njia ilio sahihi, kuchunguza vyanzo vya vifaa vya asili kwa matumizi ya ujenzi, na kuweza kuchagua maeneo ya utupaji wa taka au vifaa vya ziada.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu nambari 3 cha Sheria ya Maadili ya Wahandisi (ERB) ya 2020 imeelezwa kuwa Mhandisi atajitahidi kusimamia na kuendeleza uadilifu, na heshima ya taaluma ya uhandisi kwa kujitahidi kuongeza uwezo na heshima ya taaluma ya uhandisi.

Wakaguzi waliomba nyaraka ambazo ziliandaliwa wakati wa hatua ya upangaji wa miradi ili kutathmini ufanisi wake katika kutambua hatari zinazoweza kuukumba msingi wa jengo katika ujenzi na pia hatua zilizoendelezwa juu ya hatari zilizotambuliwa, ukaguzi ulibaini kuwa uchunguzi wa kijiolojia haukufanyika kabla ya kuanza kwa ujenzi wa hospitali kumi za wilaya.

Hali hii imechangiwa na upangaji usiriodhisha wa utekelezaji wa miradi na dosari kwa mhandisi kwa kushindwa kusimamia vyema kanuni za maadili za 'ERB' kwa kushindwa kuishauri Wizara ya Afya juu ya hitaji la kufanyika kwa uchunguzi wa kijiolojia.

Kushindwa kufanyika kwa uchunguzi wa kijiolojia, kunaweza kupelekea kuandaa muundo wa msingi wa jengo bila ya kujumuisha vihatarishi vya eneo la ujenzi, kama vile makazi ya udongo, maporomoko ya ardhi, 'liquifaction', au hatari zingine za kijiolojia, ambazo zinaweza kuhatarisha uimara wa jengo pamoja na usalama wa muda mrefu wa jengo.

Hali hii imejitokeza katika moja ya miradi kumi ya Ujenzi wa Hospitali za Wilaya ambayo ilikuwa na nyufa za miundo katika kuta na nguzo za jengo lake ambalo lilichangiwa na ujenzi kufanyika katika sehemu isiokuwa na udongo mzuri iliosababishwa na Wizara ya Afya kushindwa kumuelekeza Mkandarasi juu ya namna nzuri ya ujenzi wa majengo katika eneo hilo, kama inavyoonyeshwa katika Picha hapa chini.

Picha Nambari 3: Nyufa za kimuundo zilizobainika katika Hospitali ya Wilaya Vitongoji

Picha 3(a): Nyufa zilizobainika katika Nguzo za Hospitali ya Wilaya Vitongoji	Picha 3(b): Nyufa zilizobainika katika kuta za Wodi ya wagonjwa katika hospitali ya Wilaya Vitongoji	Picha 3(c): Nyufa zilizobainika katika Kuta za Vyoo katika hospitali ya Wilaya Vitongoji

Wakaguzi walibaini nyufa za muundo kuanzia katika msingi wa jengo, uliokusanywa kupitia kuta kuelekea katika ghorofa ya kwanza ya jengo, kama inavyoonyeshwa katika Picha nambari 3, hata hivyo, nyufa za muunganiko wa Jengo uliendeleza na kuathiri Zege (slab) ya ghorofa ya kwanza ya sakafu kama inavyoonyeshwa katika Picha hapa chini.

Picha Nambari 4: Nyufa za Muunganiko wa pamoja kati ya ghorofa ya kwanza Zege (Slab) na Bimu (Beam)

Picha nambari 4: inaonesha muunganiko wa nyufa zilizobainika katika Zege (slab) ya ghorofa ya kwanza

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kufanya yafuatayo:-

a) Kufanya tathmini ya uhimilivu wa udongo na uimara wake kwa kuwashirikisha wataalam wa kijiolojia kabla ya kuanza hatua za utekelezaji wa mradi.

b) Kuchukua hatua za haraka za kukabiliana na dosari zilizobainishwa katika Hospitali ya Wilaya Vitongoji ili kuzuia kuendelea kwa udhaifu uliobainishwa.

3.2.2 Kushindwa kuandaa vyema Tathmini ya Mahitaji na kupelekea ongezeko la shilingi 18,521,528,457

Ukaguzi ulipitia taarifa ya utekelezaji wa Mradi na kubaini kuwa upangaji na uandaaji wa miradi ya Ujenzi haikufanyika kwa ufasaha. Upeo wa miradi umekuwa ukibadilika kutokana na ongezeko la gharama za mradi ni zaidi ya gharama za awali za mkataba, kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 9: Gharama za ziada zinazotokana na kushindwa kufanya vyema Tathmini ya Mradi

Namba	Jina la mradi	Bei ya Mkataba (Tshs)	Ongezeko la Gharama (Tshs)	Asilimia ya ongezeko (%)
1.	Hospitali ya Wilaya Vitongoji	5,038,669,139	1,987,734,492	39
2.	Hospitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe	5,071,148,905	2,418,600,023	48
3.	Hospitali ya Wilaya ya Magogoni	4,506,763,921	1,955,933,631	43
4.	Hospitali ya Wilaya ya Kitogani	4,782,843,802	2,701,687,357	56
5.	Hospitali ya Wilaya ya Kinyasini	4,976,732,968	1,842,876,747	37
6.	Hospitali ya Wilaya ya Micheweni	4,800,212,162	1,898,990,741	40
7.	Hospitali ya Wilaya ya Chumbuni	4,371,192,471	1,878,234,594	43
8.	Hospitali ya Wilaya ya Mbuzini	4,516,388,643	1,879,244,390	42
9.	Hospitali ya Wilaya ya Kivunge	4,854,044,142	683,181,893	14
10.	Hospitali ya Wilaya ya Pangatupu	4,478,584,783	1,958,226,482	44
Jumla (Tshs)		**72,113,773,467**	**18,521,528,457**	**26**

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka katika nyaraka za Mkataba na kumbukumbu za Malipo, 2023

Sababu kuu zilizopelekea ongezeko la gharama ni kama zifuatazo:-

a) Kushindwa kuandaa vyema makadirio ya wahandisi ya mradi (Engineers Estimates)

Wakaguzi walifanya mapitio ya muundo wa majengo ya Hospitali za Wilaya na Mkoa na kubaini kuwa Wizara ya Afya haikuweza kuandaa vyema makadirio ya wahandisi (Engineers Estimate) ili kuweza kuainisha idadi ya vifaa ambavyo vingeendana na mahitaji ya mradi. Hali iliyopelekea ongezeko la uhitaji wa vifaa vya ziada wakati wa utekelezaji wa mradi.

b) Miradi ya ujenzi ya hospitali haikuweza kuanzishwa vyema na Wizara ya Afya

Wakaguzi walipitia nyaraka za mradi kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi na kubaini kuwa bodi ya Zabuni ilitakiwa kutoa dhamana juu ya kazi inayokusudiwa kufanywa kwa kulinganisha na mahitaji ya mradi lakini mpaka utekelezaji wa mradi unaanza Bodi ya Zabuni ilishindwa kutoa dhamana ya kazi inayokusudiwa.

c) Kukosekana kwa mapitio ya wataalam wa kiufundi kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi

Wakaguzi walipitia nyaraka za maandalizi ya mradi na kubaini kuwa mradi ulianzishwa na Wizara ya Afya bila kuhusisha idara ya watumiaji (User department) kwa ajili ya mapitio, na pia mapitio ya wataalam wa ujenzi ili kuonesha uhalisia wa ujenzi na pia uhalisia wa usanifu wa majengo yaliyopendekezwa.

Hivyo, Jadweli hapo juu linaonesha jinsi ambavyo Wizara ya Afya ilishindwa kufanya tathmini ya mradi na kupelekea ongezeko la jumla ya shilingi 18,521,528,456 kutokana na kazi za ziada na kazi za nje ambazo ni sawa na asilimia 26 ya bei ya mkataba wa awali.

Hali iliyopelekea kukosekana kwa uhakika wa fedha kutoka Serikalini, juu ya mgao wa fedha za ongezeko la kazi za nje na kazi za ziada kwa miradi hiyo. Hata hivyo, kwa miradi ya baadae Wizara ya Afya inaweza kukabiliwa na changamoto za kushindwa kukamilisha kazi endapo Serikali itashindwa kuingiza fedha za ziada ambazo hazikuwemo katika mpango wa awali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa katika miradi ya baadae, inafanya mapitio ya upeo wa mradi mapema ili kuwezesha kupatikana kwa fedha za kutosha kwa utekelezaji wa miradi.

3.2.3 Malipo yasiostahili ya jumla ya shilingi 40,000,000 kwa Wataalamu kwa ajili ya uandaaji wa Nyaraka za Mradi kwa Hospitali kumi za Wilaya

Kwa mujibu wa Kanuni ya 142(5) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma, 2020 inaeleza kuwa, Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma haitaalika zabuni za kazi isipokuwa michoro na vipimo vikiwa vimekamilika na makadirio thabiti ya gharama yameandaliwa.

Wakaguzi walibaini kuwa Wizara ya Afya ilifanya malipo ili kupata wataalam kadhaa kwa ajili ya kuandaa na kusanifu michoro ya majengo na Nyaraka za Zabuni. Wataalam hao ni pamoja na Wasanifu, Mkadiriaji Majengo, Mhandisi wa Muundo na Huduma na Mhandisi wa Umeme kwa jumla ya shilingi 40,000,000.

Aidha, Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ilipokea michoro na Nyaraka za makadirio ya gharama (BoQ) ambazo hazikukamilika na kuwepo kwa mapungufu kama yalivyotajwa katika Jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 10: Taarifa zilizolipiwa lakini hazikuweza kuandaliwa

Lengo	Hati ya Malipo	Kiasi kilicholipwa	Mapungufu yaliyojitokeza
Huduma za Umeme	H03PV2100001015	10,000,000	I. Kilichokosekana ni Michoro ya Umeme na vipimo (electrical drawings and Specifications)
Michoro ya Miundo ya Majengo na Maelezo yake (Structural drawings and Details)		10,000,000	I. Kukosekana kwa hesabu ya Muundo wa majengo kwa Wizara ya Afya kwa ajili ya kufanya tathmini na kuidhinisha. II. Kukosekana kwa maelezo ya muundo wa sakafu ya jengo kuu sehemu ya dharura na utawala, RMNHC,OPD and COT. III. Kukosekana kwa Maelezo ya Miundo kwa ghorofa ya kwanza katika hospitali zote. IV. Kukosekana kwa michoro ya Majengo mengine yaliyopo nje ya Jengo kuu la Hospitali
Michoro ya Usanifu na huduma (Architectural drawings and service drawings)		10,000,000	I. Michoro ya huduma za uzimaji wa moto haikuandaliwa
Nyaraka za Zabuni		10,000,000	I. Kutokukamilika kwa Nyaraka za Zabuni
Jumla ya fedha iliolipwa		**40,000,000**	

Chanzo: Hati za Malipo pamoja na nyaraka za Mawasiliano ya Mradi

Wakaguzi wamebaini kuwa kazi zote zilizoainishwa katika Jadweli hapo juu zinaonesha Miundo ya Majengo na Michoro ya Majengo ambayo imewasilishwa bila ya kukamilika wakati ilitakiwa wataalamu waweze kukamilisha kazi zote kwa mujibu wa makubaliano na Wizara ya Afya.

Wakaguzi walifanya mahojiano na msimamizi wa mradi chini ya idara ya Uhandisi iliyopewa dhamana ya usimamizi wa miradi ya Ujenzi wa Hospitali. Ukaguzi ulibaini kuwa kazi za uandaaji wa Nyaraka haikukamilika na kukabidhiwa kwa wahusika wa kusanifu Majengo.

Hii inaonesha kuwa kazi iliyotakiwa kufanyika haikukamilika na kufikiwa lengo lake na hii imechangiwa na ukosefu wa kuwepo kwa hadidu rejea ambazo zingewaongoza wataalamu juu ya upeo wa kazi za Miradi.

Katika kutafuta ufafanuzi zaidi ili kuelewa jinsi msimamizi wa mradi alivyosimamia utekelezaji wa mradi, Wakaguzi walifanya mahojiano na maafisa wa Wizara na kubaini kuwa, kutokana na mabadiliko ambayo yamefanyika wakati wa mapatano ya mikataba (Negotiation) kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 3.3.3 kuhusu kupunguza wigo wa kazi kutokana na changamoto za kifedha, msimamizi wa mradi alibainisha kuwa alitumia mpangilio wa awali lakini akapunguza vipimo ili kutoshea eneo lililojengwa.

Hata hivyo, kutokana na kukosekana kwa michoro iliokamilika, mahojiano na maafisa wa Wizara yalibainisha kuwa muundo wa jengo la hospitali ulitokana na maamuzi ya msimamizi wa ujenzi wakiwa katika eneo la ujenzi, ambapo Wizara ya Afya haikufikiria kurekebisha upeo wa kazi za Ujenzi katika muundo wa majengo ya hospitali ili kutoa muongozo kwa msimamizi wa mradi na maafisa wake wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

Athari za kutokufanyika kwa kazi hizo ni kwamba, Wizara ya Afya haina uhakika juu ya uhimilivu na usalama wa jengo kwa watumiaji kutokana na kutokuwa na uhakika wa muundo na pia kukosekana kwa muongozo wa usimamizi wa mradi wakati wa utekelezaji.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unashirikiana na:

(a) Wakala wa Majengo Zanzibar ili kutathmini usanifu na uhimilivu wa majengo yaliyojengwa kabla ya majengo hayo kutumika kikamilifu.

(b) Kuchukuwa hatua zinazofaa kuimarisha na kutoa mwongozo juu ya maandalizi ya muundo wa mradi.

3.2.4 Mipango isiojitosheleza ya uandaaji wa michoro baada ya kukamilika kwa kazi za ujenzi (As-built Drawings)

Kanuni ya 142(5) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma, 2020, inaeleza kuwa Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma haitaalika zabuni za kazi isipokuwa michoro na vipimo vikiwa vimekamilika na makadirio thabiti ya gharama yameandaliwa.

Wakaguzi walipitia nyaraka za makadirio ya gharama za Ujenzi (Bill of Quantity) wa Hospitali ambazo zitatumika kutengenezea michoro baada ya kukamilika kwa kazi za ujenzi (As-Built Drawings) na kubaini kuwa Wizara ya Afya haikuweza kujumuisha vipengele muhimu vya Ujenzi wakati wa utengenezaji wa michoro hio. Hali halisi ni kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 11: Hali halisi ya utengenezaji wa michoro baada ya kukamilika kwa kazi za ujenzi (As-Built)

Namba	Jina la Mradi	TEHAMA (ICT)	Uzimaji wa Moto (Fire fight)	Mitambo (Mechanical)	Bomba (Plumbing)	Umeme (Electrical)	Ufungaji wa Huduma za Gesi (Gas installation)	Kipoza Hewa (AC)
1.	Mbuzini Magharibi A Unguja	x	V	X	v	v	X	x
2.	Mradi wa Lumumba	x	V	X	v	v	X	x
3.	Chumbuni Mjini Unguja	x	V	X	v	v	X	x
4.	Magogoni Magharibi B Unguja	x	V	X	v	v	X	x
5.	Kinyasini Wete Pemba	x	V	X	v	v	X	x
6.	Kitogani Wilaya ya Kusini Unguja	X	V	X	v	v	X	x
7.	Micheweni Pemba	X	V	X	v	v	X	x
8.	Mwera Pongwe Wilaya ya Kati Unguja	X	V	X	v	v	X	x
9.	Vitongoji Wilaya ya Chake-chake	X	V	X	v	v	X	x
10.	Kivunge Kaskazini A Unguja	X	V	X	v	v	X	x
11.	Pangatupu Kaskazini B Unguja	X	V	X	v	v	X	x

Chanzo: Nyaraka za makadirio ya gharama za Ujenzi zilizotayarishwa

Ufafanuzi:

V- Inapatikana

X- Haipatikani

Wizara ya Afya ilipanga kutekeleza utoaji wa huduma, TEHAMA, huduma ya uzimaji wa moto, ufungaji wa Mitambo, Umeme, ufungaji wa mfumo wa Gesi, na ufungaji wa vipoza joto lakini Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Afya ilisimamia upatikanaji wa michoro baada kukamilika kwa kazi za ujenzi kwa ajili ya mfumo

wa uzimaji wa moto na Umeme na kushindwa kusimamia upatikanaji wa michoro baada ya kukamilika kwa kazi za ujenzi kwa ajili ya mfumo wa gesi, mfumo wa kupoza joto, Mitambo na mfumo wa TEHAMA.

Hali hii imesababishwa na maandalizi duni ya nyaraka za Makisio ya gharama za Ujenzi (Bill of Quantity) na mapitio duni ya nyaraka za zabuni kabla ya kuanza utekelezaji wa mkataba, na hii itasababisha ukosefu wa muongozo wa kutekeleza upatikanaji wa michoro baada ya kukamilika kwa kazi za ujenzi na kushindwa kutoa picha ya wazi ya njia za huduma zilizowekwa katika jengo ikiwa kuna matengenezo na ukarabati unaohitajika wakati wa kipindi cha uendeshaji.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unajipanga kwa ajili ya maandalizi ya kukamilisha kupata michoro baada ya kukamilika kwa kazi za ujenzi kabla ya wakandarasi kupewa vyeti vya kukamilisha miradi.

3.2.5 Mipango isiojitosheleza kwa ajili ya upimaji na kukabidhi mradi

Kanuni ya 142(5) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma, 2020 inaeleza kuwa Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma haitaalika zabuni za kazi isipokuwa michoro na vipimo vikiwa vimekamilika na makadirio thabiti ya gharama yameandaliwa.

Wakaguzi walipitia maandalizi ya nyaraka za makadirio ya gharama za ujenzi hasa kuhusiana na upimaji na ukabidhishaji wa kazi za Mradi na kubainisha kuwa Wizara ya Afya ilishindwa kusimamia vyema vipengele muhimu vya ujenzi wakati wa upimaji na ukabidhishaji wa kazi ni kama inavyoainishwa katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 12: Hali halisi ya Mipango ya upimaji na ukabidhi

Namba	Jina la Mradi	TEHAMA (ICT)	Uzimaji wa Moto (Fire fight)	Mitambo (Mechanical)	Bomba (Plumbing)	Umeme (Electrical)	Ufungaji wa Huduma za Gesi (Gas installation)	Kipoza Hewa (AC)
1.	Mbuzini Magahribi A Unguja	v	x	x	x	x	x	v
2.	Mradi wa Lumumba	v	x	x	x	x	x	x
3.	Chumbuni Mjini Unguja	v	x	x	v	v	x	x
4.	Magogoni Magharibi B Unguja	v	x	x	x	x	x	x
5.	Kinyasini Wete Pemba	v	x	x	v	v	v	x

Namba	Jina la Mradi	TEHAMA (ICT)	Uzimaji wa Moto (Fire fight)	Mitambo (Mechanical)	Bomba (Plumbing)	Umeme (Electrical)	Ufungaji wa Huduma za Gesi (Gas installation)	Kipoza Hewa (AC)
6.	Kitogani Wilaya ya Kusini Unguja	x	v	x	v	v	x	x
7.	Micheweni Unguja	v	x	x	x	x	v	v
8.	Mwera Pongwe Wilaya ya Kati Unguja	v	x	x	v	x	x	x
9.	Vitongoji Wilaya ya Chakechake	v	x	x	x	x	v	v
10.	Kivunge Kaskazini A Unguja	v	x	x	x	x	v	v
11.	Pangatupu Kaskazini B Unguja	x	v	x	v	v	x	x

Chanzo: Nyaraka za makadirio ya gharama za Ujenzi zilizotayarishwa

Ufafanuzi:

V- Inapatikana

X- Haipatikani

Wizara ya Afya ilipanga kutekeleza huduma ya upimaji na ukabidhishaji wa kazi, ambapo kwa huduma ya TEHAMA ilikuwa imeekewa mipango toshelevu lakini kulikua na dosari katika upangaji wa mfumo wa vifaa vya kuzimia moto, mabomba (Plumbing), umeme (Electrical), na kuunda mfumo sahihi ya gesi (Gas installation) na vipoza hewa (Air conditioning) kama inavyoonekana katika Jadweli hapo juu. Kwa huduma ya upatikanaji wa Mitambo (mechanical) na huduma ya kuzima moto (Firefighting) hazikuwemo katika maandalizi.

Hali hii imesababishwa na maandalizi duni ya nyaraka za Makisio ya gharama za Ujenzi (Bill of Quantity) na mapitio duni ya nyaraka za zabuni kabla ya kuanza utekelezaji wa mkataba na hii imesababishwa na kutokuwepo kwa muongozo wa ufanyaji vipimo na kuvikabidhi ambapo itasababisha kukosekana kwa picha halisi ya ufanyaji kazi wa vifaa hivyo ambavyo vimefungwa katika Majengo hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuandaa muongozo wa utekelezaji wa upimaji na ukabidhishaji wa mifumo iliyowekwa katika majengo ya hospitali kabla ya kuanza kutumika.

3.2.6 Hasara ya shilingi 527,791,500 kutokana na kushindwa kuandaa vyema vipimo vya Kiufundi kwa ajili ya uwekaji wa viluva katika maeneo ya Ujenzi wa hospitali (interlocking paving blocks)

Kanuni ya 142(5) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma, 2020, inaeleza kuwa Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma haitaalika zabuni za kazi isipokuwa michoro na vipimo vikiwa vimekamilika na makadirio thabiti ya gharama yameandaliwa. Aidha, BS 368: 1971 inaeleza kuwa (precast concrete flags) zitalazimika kua na uimara wa **112 lb (40Mpa)** wakati wa kufanywa kwa vipimo vya ubora.

Wakaguzi walikagua nyaraka kwa ajili ya uandaaji wa vipimo vya kiufundi kwa ajili ya viluva (Interlocking paving blocks) na kubaini kuwa vipimo havikuandaliwa kulingana na viwango vya uhandisi vinavyohitajika. Kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 13 : Vigezo ambavyo Wizara wametumia katika utengenezaji wa viluva

Namba	Jina la Mradi	Viluva kwa ajili ya shughuli nzito (Heavy Duty Paving Blocks)	Bei (Tsh)	Matokeo
1.	Mbuzini Magharibi A Unguja	"Precast Interlocking Concrete Paving Stones, Bs 368; Bedding, Jointing and Grouting with Cement Mortar (1:4); External"	80,500,000	Vinalingana na Vipimo vya BS
2.	Mradi wa Lumumba Mkoa wa Mjini Unguja	"Heavy Duty Paving Block Compressive Strength 4 To 10 Mpa; Hexahedral Interlocking With Irregular Shape Size 200 X 100 X 80mm Laid Over Sand Pillow; Blinded With Sand; Compacted By Hand Compactor"	200,000,000	Havilingani na Vipimo vya BS
3.	Chumbuni Mjini Unguja	"Precast Interlocking Concrete Paving Stones, Bs 368; Bedding, Jointing and Grouting with Cement Mortar (1:4); External"	48,400,000	Vinalingana na Vipimo vya BS
4.	Magogoni Magharibi B Unguja	"Precast Interlocking Concrete Paving Stones, Bs 368; Bedding, Jointing and Grouting with Cement Mortar (1:4); External"	90,500,000	Vinalingana na Vipimo vya BS
7.	Wilaya ya Micheweni	"Grade 30 Nominal Mix 1:1:2; 30N/Mm2 At"	69,240,000	Havilingani na Vipimo vya BS

Namba	Jina la Mradi	Viluva kwa ajili ya shughuli nzito (Heavy Duty Paving Blocks)	Bei (Tsh)	Matokeo
8.	Mwera Pongwe wilaya ya kati Unguja	"Precast Pavements"	250,039,500	Havilingani na Vipimo vya BS
9.	Vitongoni Wilaya ya Chakechake	"Precast Concrete (1:1^{1}/2:3) Interlocking"	8,512,000	Havilingani na Vipimo vya BS
10.	Kivunge Kaskazini A Unguja	"Interlocking Engineering Concrete Pavier Blocks Compressive Strength Not Less Than 40n/Mm2 As Supplied From Approved Manufacture Laid To Approved Pattern"	55,000,000	Vinalingana na Vipimo vya BS
Jumla			**527,791,500**	

Chanzo: Nyaraka za Mikataba, 2023

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa vifaa vilivyotumika katika ujenzi vyenye thamani ya jumla ya shilingi 527,791,500.00 vilitolewa kwa vipimo ambavyo havikuwa vikilingana na viwango vinavyokubalika vya BS 368: 1971.

Vifaa vya Ujenzi (Viluva) vilivyoorodheshwa katika Nyaraka za mkataba kwa viwango ambavyo havikubaliki kwa mujibu wa BS 368:1971, viliandaliwa kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya njia za kupitia Magari na Maegesho katika maeneo yaliyojengwa hospitali.

Hali hii imesababishwa na kutokupitiwa na kuidhinishwa kwa nyaraka za zabuni kabla ya kuzitoa kwa wazabuni na matokeo yake ikapelekea wakandarasi kufanya kazi kwa kutumia vipimo visivyo sahihi wakati wa uwekaji wa viluva (interlocking paving blocks) katika maeneo ya njia za kupita gari na maegesho.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa nyaraka za zabuni zinaandaliwa vizuri na kuidhinishwa na bodi ya zabuni kabla ya kuzitoa kwa wazabuni.

3.2.7 Kufanya Mabadiliko ya upeo wa kazi za Ujenzi wa Miradi bila kushauriana na Idara tumizi (User Department)

Sehemu ya 2.2.2.2 ya BS 8126 sehemu ya 1 juu ya maelezo ya Uimara inasema kuwa miundo ya Majengo inapaswa kupangwa na kutengenezwa ili isiathiriwe na athari za ajali. Hasa, hali zinapaswa kuepukwa ambapo uharibifu wa maeneo madogo ya muundo majengo au kushindwa kwa vitu vidogo vidogo ndani ya Muundo wa Jengo inaweza kusababisha kuanguka kwa sehemu kuu za muundo wa Jengo hilo.

Ukaguzi ulifanya Mapitio ya Nyaraka za mradi na kutathmini utoshelevu wa upangaji wa mradi na kubaini kuwa upeo wa mradi umetofautiana na ule wa awali kutokana na upatikanaji wa kazi za ziada.

Aidha, Ukaguzi ulifanya Mapitio ya taarifa za Mapatano na kubaini kuwa upeo wa kazi za mradi ulipunguzwa kutoka 3750m^2 hadi 2498m^2 kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha za kujenga kwa kufuata upeo wa awali. Hivyo, mabadiliko katika upeo yalitakiwa lazima kufanyiwa marekebisho katika muundo wa majengo lakini mahojiano na maafisa wa mradi yalibainisha kuwa muundo wa Majengo na vipimo vilibadilishwa kulingana na maamuzi ya msimamizi wa Mradi.

Hali hii imechangiwa na mipango duni ya utekelezaji wa mradi na hatua zake ili kuhakikisha kuwa ubora na uimara wa jengo unadumishwa jambo ambalo linaweza kupelekea usalama na uimara wa jengo kuwa hatarini.

(i) Muundo wa Majengo ya hospitali ulio chini ya viwango vinavyotakiwa

Kwa mujibu wa viwango vya Wizara ya Afya Vol 3, 2022 ya masuala ya ujenzi wa hospitali za Wilaya, Mkoa na vituo vya afya, imeainisha ukubwa wa vyumba vinavyohitajika katika idara husika ya matibabu.

Wakaguzi walipitia michoro baada ya kukamilika ujenzi (As-Built Drawings) ili kutathmini ukamilifu wa miundo ya ujenzi iliyojengwa na kubainisha kuwa vyumba vilivyojengwa ni tofauti na vile vinavyokubalika kwa mujibu wa viwango vya Wizara ya Afya, kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapa chini.

Jadweli Nambari 14: Tofauti baina ya muundo unaohitajika kwa mujibu wa miongozo na muundo kwa mujibu wa ujenzi uliofanyika

Eneo	Ukubwa wa Vyumba unaotakiwa	Eneo la Chumba (m^2)	Ukubwa wa Vyumba uliokuwepo	Eneo la Chumba (m^2)	Tofauti (m^2)	Asilimia (%)
Chumba cha Dawa	3.0x3.6	10.8	2.35 x 3.6	8.46	2.34	21.7
Eneo la kuhifadhi Baridi	3.6x4.2	15.12	2.35 x 3.6	8.46	6.66	44.0
Chumba kidogo cha Upasuaji	4.8x6.0	28.8	3.8 x 1.95	7.448	21.352	74.1
Chumba cha ICT	3.0x3.6	10.8	2.35 X 3.8	9.165	1.635	15.1
Chumba cha Uangalizi	9.6x4.2	40.32	3.0 x 3.1	9.6	30.72	76.2
Chumba kilichotengwa (Isolation wards)	12.6x7.2	90.72	6.0 x 6.35	38.1	52.62	58.0

Eneo	Ukubwa wa Vyumba unaotakiwa	Eneo la Chumba (m^2)	Ukubwa wa Vyumba uliokuwepo	Eneo la Chumba (m^2)	Tofauti (m^2)	Asilimia (%)
Wodi ya Upasuaji wa wanaume	15.6x7.2	112.32	6.0 x 6.15	36.9	75.42	67.1
Wodi za matibabu	15.6x7.2	112.32	6.0 x 6.0	36	76.32	67.9
Wodi ya Upasuaji wanawake	15.6x7.2	112.32	6.5 x 6.8	44.85	67.47	60.1
ICU ward	10x15	150	6.3 x 6.85	43.218	106.782	71.2
Chumba cha kubadilisha nguo	2.4x4.2	10.08	1.45 x 1.5	2.32	7.76	77.0
Jumla		**693.6**		**244.5**	**449.1**	**64.7**

Chanzo: Michoro ya Mradi na muongozo wa ujenzi wa Wizara ya Afya

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa vyumba 11 vilivyojengwa katika hospitali za Wilaya vilijengwa chini ya kiwango kwa 449.1m^2 sawa na asilimia 64 ya viwango vinavyohitajika. Hali hii imesababishwa na mabadiliko ya ukubwa bila uratibu wa idara zingine ambazo ni watumiaji ili kuhakikisha utoaji mzuri wa huduma za afya.

Vyumba vya hospitali vilivyojengwa ni vidogo ambavyo vinaweza kuwa na athari mbaya kwa wagonjwa, watoa huduma za afya, na utendaji wa ujumla wa jengo la hospitali katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora za afya.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa majengo ya hospitali yanajengwa kwa mujibu wa viwango kubalifu kulingana na miongozo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) au miongozo ya ndani ya Wizara ya Afya.

3.3 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usimamizi wa Ununuzi katika Ujenzi wa Miradi ya Hospitali

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu mchakato wa kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali kumi (10) za Wilaya na Hospitali moja (1) ya Mkoa kama ilivyoelezwa hapa chini:

Sehemu hii inatoa muhtasari na utangulizi wa mchakato wa ununuzi wa mradi. Ununuzi ni sehemu muhimu ya usimamizi wa mradi ambayo inahusisha kupata bidhaa, huduma, na rasilimali zinazohitajika ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi. Ripoti hii inaelezea dhana muhimu, hatua, na mambo yanayohusika katika mchakato wa ununuzi wa mradi.

3.3.1 Nyaraka za Zabuni za ujenzi wa Hospitali za Wilaya na Mkoa zilitolewa kabla ya Kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni

Kanuni ya 45(1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma GN. 6890 ya mwaka 2020 inaitaka Bodi ya Zabuni kuidhinisha rasimu ya Nyaraka za zabuni kabla ya kuzitoa Zabuni hizo.

Ukaguzi ulipitia kumbukumbu za manunuzi pamoja na nyaraka za kumbukumbu za Bodi ya Zabuni, hakukuwa na ushahidi wowote unaoonyesha kuwa hati ya zabuni ziliwasilishwa kwa Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa.

Hali hii imesababishwa na kutokuanzishwa kwa mchakato wa manunuzi na idara tumizi, kutokana na kushindwa kuwasilisha nyaraka za zabuni kwa Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa baada ya mahitaji kuzingatiwa. Aidha, hali hii inaleta hatari ya kutoa nyaraka za zabuni ambazo hazioneshi mahitaji yote yanayohitajika katika utekelezaji wa mkataba.

Matokeo yake, kulikuwa na tofauti ya ongezeko la gharama katika kila mradi, na baadhi ya vyumba, kama vile chumba cha dawa, ni vidogo sana kwa hospitali za Wilaya.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unaendeleza udhibiti wa ndani ambao utahakikisha hakuna zabuni iliyotolewa kabla ya idhini ya bodi ya zabuni.

3.3.2 Ongezeko la Gharama ambazo hazijaidhinishwa za jumla ya shilingi 36,016,453,214 kutoka kiasi kilichopangwa kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali 10 za Wilaya na Hospitali ya Mkoa ya Lumumba

Kanuni ya 125(1&2) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inasema kuwa kutakuwa na thamani inayokadiriwa ambayo ni msingi wa kazi za ununuzi; na zabuni yoyote iliyotathminiwa na iko juu au chini ya makadirio ya thamani ya manunuzi kama ilivyo, haitaidhinishwa isipokuwa itatimiza masharti kama ilivyoelezwa katika miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma Zanzibar.

Pia, kifungu nambari 43(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinataka manunuzi yaanzishwe au yaendelee tu kwa uthibitisho kwamba fedha kwa kiasi kamili kwa kipindi kinachohitajika zinapatikana au zitapatikana wakati ahadi ya mkataba itakapotolewa.

Mapitio ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka kwa ajili ya ujenzi wa hospitali 10 za Wilaya na hospitali ya Mkoa ya Lumumba yalionyesha kuwa jumla ya gharama zilizokadiriwa ni jumla ya shilingi 36,000,000,000 na mikataba iliotolewa ilikuwa ni jumla ya shilingi 72,016,453,214. Kama inavyooneka katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 15: Tofauti katika Ongezeko la fedha baina ya Makadirio na Tuzo

Maelezo	Eneo	Kiasi Tshs		
		Makadirio	Tuzo	Ongezeko
Ujenzi wa Hospitali 10 za Wilaya (7 Unguja & 3 Pemba)	Dunga / Mwerapongwe	2,200,000,000	5,071,148,905	2,871,148,905
	Mbuzuni	2,200,000,000	4,516,388,643	2,316,388,643
	Kivunge	2,200,000,000	4,854,044,141	2,654,044,141
	Pangatupu	2,200,000,000	4,385,864,537	2,185,864,537
	Kinyasini	2,200,000,000	4,976,732,967	2,776,732,967
	Chumbuni	2,200,000,000	4,366,592,470	2,166,592,470
	Kitogani/Makunduchi	2,200,000,000	4,782,843,801	2,582,843,801
	Micheweni	2,200,000,000	4,800,212,161	2,600,212,161
	Vitongoji	2,200,000,000	5,038,669,138	2,838,669,138
	Magogoni	2,200,000,000	4,506,763,920	2,306,763,920
Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba Unguja	Lumumba	14,000,000,000	24,717,192,531	10,717,192,531
Jumla		**36,000,000,000**	**72,016,453,214**	**36,016,453,214**

Chanzo: Mapitio ya Mpango wa mwaka wa ununuzi na Mkataba

Jadweli hapo juu, linaonyesha ongezeko la jumla ya shilingi 36,016,453,214 (sawa na asilimia 100) kutoka kiwango kilichokadiriwa.

Majadiliano yaliyofanyika baina ya timu ya Ukaguzi na maafisa kutoka Wizara ya Afya yalibainisha kuwa kuongezeka kwa gharama hizo kulihusishwa na ukadiriaji duni/usio mzuri wa gharama za mradi (Engineer's Estimate) kama inavyowezekana. Hali hii imesababishwa na uhaba wa Wakadiriaji wa Majengo kutoka Wizara ya Afya.

Timu ya Ukaguzi haikupewa uthibitisho wowote kwamba Mlipaji Mkuu (Paymaster General) aliidhinisha ongezeko hilo la gharama kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Kanuni 125 (1 na 2) za Kanuni za Ununuzi wa Umma ya 2020.

Kutokuidhinishwa kwa ongezeko hilo la gharama ni dalili ya kasoro katika usimamizi wa michakato na taratibu za ununuzi kama ilivyoainishwa katika Kanuni za manunuzi. Hali hii inaweza kusababisha kasoro katika udhibiti wa gharama kwa kila ununuzi uliofanywa kulingana na kiasi kilichokadiriwa. Aidha, inahatarisha kuingia katika huduma au mkataba bila kuwa na uhakika kwamba kutakuwa na fedha za kutosha kufidia gharama na inaweza kupelekea hatari kwa wakandarasi kutolipwa kulingana na masharti ya mkataba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba:

- Kuwa na wafanyakazi wenye uwezo wa kukadiria gharama za Ujenzi kwa usahihi kama inavyotakiwa; na
- Kuidhinishwa kwa tofauti ya gharama iliyojitokeza kutoka kwa kiasi kilichokadiriwa.

3.3.3 Kuongezeka kwa bei ya mikataba kwa jumla ya shilingi 10,860,568,900 kutokana na kutozingatia kupunguzwa kwa ukubwa wa ujenzi (Sqm) iliyokubaliwa wakati wa mapatano

Kanuni ya 134(1)(b) ya Ununuzi wa Umma GN. 6890 ya 2020, inaeleza kuwa mapatano yanaweza kufanywa na mzabuni alieshinda baada ya kufanyiwa tathmini kuhusiana na kupunguza kazi kwa sababu za bajeti.

Ukaguzi ulipitia taarifa za kumbukumbu za mapatano baina ya Wizara ya Afya na Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa hospitali kumi (10) za Wilaya za Unguja na Pemba na kuibaini kuwa pande zote mbili zilikubaliana kupunguza ukubwa (sqm) wa ujenzi kutoka 3750 hadi 2489 kutokana na sababu za kibajeti, hata hivyo, mkataba uliosainiwa haukuzingatia punguzo hilo, kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

Hata hivyo, Ukaguzi ulitembelea maeneo ya Ujenzi wa Miradi na kubaini uwepo wa upunguzwaji wa ukubwa wa ujenzi (sqm) hadi kufikia 2700 (sqm) kulingana na Ujenzi halisi wa Majengo ya Hospitali.

Jadweli Nambari 16: Bei ya mkataba kabla na baada ya kupunguza ukubwa wa ujenzi (sqm)

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya	Makadirio ya bei baada ya kupunguzwa kwa Ujenzi (Sqm) katika Tsh (Bila ya kodi la Ongezeko la thamani)	Makadirio ya bei baada ya kupunguzwa kwa Ujenzi (Sqm) katika Tshs (pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Bei ya awali kabla na baada ya kupunguza Tsh (pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Kiasi kilichoongezeka (pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)
Dunga/Mwera Pongwe	3,479,940,483	4,001,931,555	5,071,148,905	1,069,217,349
Mbuzuni	2,949,651,657	3,392,099,405	4,516,388,643	1,124,289,237
Kivunge	3,383,495,623	3,891,019,966	4,854,044,141	963,024,175
Pangatupu	2,836,463,316	3,261,932,813	4,385,864,537	1,123,931,724
Kinyasini	3,147,000,000	3,619,050,000	4,976,732,967	1,357,682,967
Chumbuni	2,855,778,910	3,284,145,746	4,366,592,470	1,082,446,723
Kitogani	3,302,748,878	3,798,161,210	4,782,843,801	984,682,591
Micheweni	3,147,000,000	3,619,050,000	4,800,212,161	1,181,162,161
Vitongoji	3,639,632,468	4,185,577,339	5,038,669,138	853,091,799
Magogoni	2,944,107,609	3,385,723,751	4,506,763,920	1,121,040,169
Jumla	**31,685,818,946**	**36,438,691,788**	**47,299,260,688**	**10,860,568,900**

Chanzo: Kumbukumbu za mazungumzo ya mapatano zilizofanyika mnamo 14 Desemba, 2021

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa jumla ya shilingi 10,860,568,900 hazikupunguzwa kuendena na marekebisho ya bei ya mkataba, ambapo Wakaguzi walibaini kuwa fedha hizo zilikua ni zaidi ya kiasi kilichokubaliwa wakati wa mapatano kutokana na kupunguzwa kwa kazi.

Ukauguzi unashauri Wizara ya Afya kuhakikisha malipo yanafanywa kulingana na kazi iliyofanywa ili kuepuka kulipa upeo wa kazi iliyopunguzwa.

3.3.4 Ongezeko la Bei ya Mikataba la jumla ya shilingi 955,519,488 kutokana na Utoaji wa Tuzo kwa Wazabuni wasio na sifa

Kanuni nambari 127 ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inamtaka mzabuni mwenye zabuni iliyotathminiwa vizuri kuwa mzabuni aliyefanikiwa.

Wakati wa ukaguzi wa taarifa za tathmini za ujenzi wa hospitali za wilaya katika hospitali za Wilaya za Vitongoji, Kivunge, Mwera Pongwe na Kinyasini, ukaguzi ulibaini kuwa mkataba wa zabuni ya ujenzi wa hospitali za Wilaya za Vitongoji, Kinyasini, Dunga, Makunduchi (Kitogani) haukutolewa kwa mzabuni aliyependekezwa na timu ya tathmini wala kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni, kama ambavyo inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 17: Mchanganuo wa Mzabuni aliezawadiwa bila ya kuwa na vigezo

Jina la Hospitali ya Wilaya	Mzabuni mwenye kiwango cha chini aliyependekezwa na Kamati ya Tathmini		Mzabuni aliyepewa Tuzo		Tofauti (Tsh)
	Jina la Mzabuni	Kiasi (Tsh)	Jina la Mzabuni	Kiasi kilichorekebishwa na kilichopunguzwa (Tsh)	
Vitongoji	Group Six Construction Limited	4,961,866,940	Salem Construction Limited	5,038,669,138	76,802,198
Kinyasini	Benchmark Engineering Company Limited	4,806,492,438	Group Six Construction Limited	4,976,732,967	170,240,529
Mwera pongwe	CRJE (East Africa) Limited	4,720,856,520	Rans Building Contractors Ltd	5,071,148,905	350,292,384
Kivunge	WCEL Limited	4,495,819,763	Mazrui Building Contractors	4,854,044,141	358,184,377
Jumla (Tsh).					**955,519,488**

Chanzo: Ripoti ya tathmini, kumbukumbu za Vikao vya bodi ya zabuni na mikataba iliyosainiwa

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa jumla ya shilingi 955,519,488 zimeongezeka kutokana utoaji wa tuzo kwa wazabuni wasio na vigezo.

Hali hii ilipekea kuwanyima fursa wazabuni waliopendekezwa na kamati ya tathmini na kupelekea ongezeko la gharama ya mradi kwa jumla ya shilingi 955,519,488.

3.3.5 Kushindwa kutoa barua ya nia ya utoaji tuzo kwa wazabuni wote

Kanuni ya 137(2) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020, inasema kwamba, baada ya kupokea mapendekezo ya Ukaguzi wa uamuzi wa tuzo kutoka kwa Bodi ya Zabuni, Afisa Masuuli atajiridhisha kuwa taratibu sahihi zimefuatwa na ndani ya siku tatu za kazi, atatoa taarifa ya nia ya kutoa mkataba kwa wazabuni wote walioshiriki katika zabuni husika na kuwapa siku kumi za kuwasilisha malalamiko.

Mapitio ya kumbukumbu za manunuzi kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali kumi (10) za Wilaya (7 Unguja na 3 Pemba); na Ujenzi wa Hospitali moja (1) ya Mkoa Unguja, Wizara ya Afya ilitoa barua ya kumjuulisha mzabuni aliyeshinda bila kutoa barua ya nia ya kutoa tuzo kwa wazabuni wote walioshiriki katika mchakato wa ununuzi ili kutoa nafasi ya malalamiko na mapitio ya kiutawala.

Hali hii ilikiuka moja ya kanuni ya msingi ya manunuzi ya umma kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 37 (b) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, ambayo inataka manunuzi yote yafanyike kwa namna inayozingatia uwazi, uwajibikaji na haki.

Pia, ilipelekea kupewa mikataba kwa wazabuni wasio na sifa na kupelekea ongezeko la gharama ya mkataba kwa jumla ya shilingi 955,519,488**,** kama ilivyoelezwa katika hoja iliyopo hapo juu. Kushindwa kutoa barua ya nia ya utoaji tuzo, kumepelekea kushindwa kutoa nafasi ya malalamiko kutoka kwa wazabuni na mapitio ya utawala.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba unaweka udhibiti ambao unazuia kutolewa kwa taarifa ya tuzo kwa mzabuni aliyeshinda kabla ya kuwajulisha wazabuni wote juu ya nia ya kutoa tuzo hiyo.

3.3.6 Kufanyika kwa majadiliano ya mapatano kabla ya kutolewa kwa idhini ya Bodi ya Zabuni kuhusiana na mapendekezo ya Kamati ya Tathmini kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali kumi (10) za Wilaya

Kanuni ya 134(3) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020, inasema kuwa mazungumzo na mzabuni hayataruhusiwa hadi baada ya Bodi ya Zabuni kupitisha mapendekezo ya mapitio ya ripoti ya Kamati ya Tathmini.

Wakaguzi walipitia taarifa za kumbukumbu za mazungumzo kwa ajili ya mapatano ya ujenzi wa hospitali kumi (10) za Wilaya na hospitali moja (1) ya Mkoa yaliyofanyika baina ya Wizara ya Afya na Wakandarasi na kubaini kuwa mapatano hayo yalifanyika mnamo tarehe 14 Disemba, 2021.

Aidha, Ukaguzi ulipofanya mapitio ya kumbukumbu ya Bodi ya Zabuni juu ya idhini iliotolewa kwa ajili ya ujenzi wa miradi hio na kubaini kuwa Bodi ya Zabuni iliidhinisha ripoti ya tathmini mnamo tarehe 16 Disemba, 2021 ikiwa ni siku mbili baada ya kufanyika kwa mapatano. Hivyo, Wizara ya Afya ilifanya mapatano na wazabuni kabla ripoti ya tathmini kutolewa idhini na Bodi ya Zabuni.

Matokeo yaliyojitokeza ni kuwa, wazabuni watano (5) waliohudhuria majadiliano hayo walipewa mikataba na kusaini wakati hawakupendekezwa na Kamati ya Tathmini wala kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni, kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 18: Tofauti ya gharama baina ya wazabuni waliopewa mikataba dhidi ya wazabuni waliopendekezwa na kamati ya tathmini

Mahali	Mzabuni aliyepewa tuzo	Bei ya Mzabuni aliyepewa tuzo (Tsh)	Mzabuni mwenye sifa kwa mujibu wa tathmini	Bei ya mzabuni mwenye sifa (Tsh)
Hopsitali ya Wilaya ya Vitongoji	SALEM CONSTRUCTION LTD	5,038,669,139	Group Six Construction Limited	4,961,866,940
Hopsitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe	RANS COMPANY LTD	5,071,148,905	CRJE (East Africa) Limited	4,720,856,520
Hopsitali ya Wilaya ya Kinyasini	GROUP SIX INTERNATIONAL	4,976,732,968	Benchmark Engineering Company Limited	4,806,492,438
Hopsitali ya Wilaya ya Kivunge	MAZRUI BUILDING CONTRACTOR	4,854,044,142	WCEL Limited	4,495,819,763
Hospitali ya Mkoa Lumumba	ESTIM CONSTRUCTION LTD	24,717,192,531	Group Six International Ltd	17,131,285,348

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa kumbukumbu za Bodi ya Zabuni

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa kulikuwa na ongezeko la jumla ya shilingi 8,541,466,676 kutokana na utoaji wa zabuni tano (5) zisizo na sifa. Hii ilikiuka moja ya kanuni za msingi za ununuzi wa umma kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 37 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, ambayo inataka manunuzi yote yafanyike kwa namna inayozingatia uwazi, uwajibikaji, haki, Uchumi na ufanisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba kuweka udhibiti ambao unahitaji kitengo cha ununuzi kufanya mapitio ya kina ya ripoti ya tathmini kabla ya kuwasilishwa kwa Bodi ya Zabuni kwa kuidhinishwa.

3.3.7 Kumbukumbu za majadiliano ya mapatano ya ujenzi wa Hospitali kumi (10) za Wilaya na Hospitali moja (1) ya Mikoa hazikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni

Kanuni ya 136 (2) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inahitaji timu ya mapatano kuwasilisha ripoti ya majadiliano kwa Bodi ya Zabuni.

Kupitia mapitio ya taarifa za bodi ya zabuni, ukaguzi ulishindwa kuthibitisha endapo ripoti ya taarifa za mapatano iliwasilishwa kwa Bodi ya Zabuni kwa ajili kupatiwa idhini.

Kujumuisha makubaliano yaliyokubaliwa wakati wa mapatano katika mkataba bila kuwasilishwa kwa Bodi ya Zabuni kwa ajili ya mapitio na kupatiwa idhini kunaleta hatari ya kujumuisha vifungu na masharti yasiyofaa katika mkataba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba makubaliano yote yanayotokana na mapatano yanaidhinishwa na bodi ya zabuni kabla ya kujumuishwa katika mikataba kwa utekelezaji.

3.4 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usimamizi wa Mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali kumi (10) za Wilaya na Hospitali moja (1) ya Mkoa Lumumba. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha mradi unatekelezeka kwa ufanisi kuweza kuwanufaisha wahusika. Inaelezea mambo muhimu ya usimamizi wa mkataba na kushajihisha umuhimu wa mawasiliano, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba, gharama, wakati na ubora.

3.4.1 Kushindwa kuongeza muda wa dhamana za Miradi kwa ajili ya kazi za mradi zilizoongezeka

Wakaguzi walipitia dhamana za mradi ikiwa ni pamoja na hati ya dhamana ya utekelezaji kazi (Performance security) pamoja na bima kwa miradi na kubaini kuwa wakandarasi waliwasilisha hati ya dhamana ya usalama wa kazi (security coverage) kwa gharama za mkataba wa awali lakini hawakujumuisha kazi za ziada kulingana na ongezeka kwa kazi. Mapungufu yafuatayo yameweza kubainika.

(a) Hati ya dhamana ya utekelezaji kazi haikuweza kugharamia na kujumuisha gharama zote za mradi kwa jumla ya shilingi 19,204,710,352

Sehemu ya 26 ya Masharti Maalumu ya mkataba, inasema kuwa hati ya dhamana ya utekelezaji wa kazi itakuwa sawa na asilimia 10 ya bei ya mkataba.

Wakaguzi walipitia dhamana za utekelezaji kazi zilizowasilishwa na wakandarasi na kubainisha kuwa dhamana ya utekelezaji wa kazi zilizowasilishwa kwa mradi huo zilijumuishwa na kugharamia bei za mikataba ya awali lakini hazikufanyiwa maboresho ili kuweza kuendana na bei halisi zilizorekebishwa za mikataba, kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 19: Uchambuzi wa Gharama za Mradi zilizojumuishwa katika dhamana ya utekelezaji wa kazi (Perfomance security)

Jina la mradi	Bei ya Mkataba (Tsh)	Dhamana ya kazi ya awali (Tsh)	Mikataba iliyorekebishwa	Bei	Kiasi ambacho hakikuwekwa kama Dhamana (Tsh)
			Bei (Tsh)	Dhamana ya Kazi (Tsh)	
Mwera Pongwe District Hopsital	5,071,148,905	507,114,891	7,489,748,928	748,974,893	2,418,600,023
Magogoni District Hopsital	4,506,763,921	450,676,392	6,462,697,552	646,269,755	1,955,933,631
Kitogani District Hospital	4,782,843,802	478,284,380	7,484,531,159	748,453,116	2,701,687,358
Kinyasini District Hopsital	4,976,732,968	497,673,297	6,819,609,715	681,960,972	1,842,876,747
Micheweni District Hospital	4,800,212,162	480,021,216	6,699,202,903	669,920,290	1,898,990,741
Chumbuni District Hopsital	4,371,192,471	437,119,247	6,249,427,065	624,942,707	1,878,234,594
Mbuzini District Hopsital	4,516,388,643	451,638,864	6,395,633,033	639,563,303	1,879,244,390
Kivunge District Hopsital	4,854,044,142	485,404,414	5,537,226,035	553.722,603	68,318,189
Vitongoji District Hospital	5,038,669,139	503,866,914	7,026,403,631	702,640,363	1,987,734,492
Pangatupu District Hopsital	4,478,584,783	447,858,478	6,436,811,265	643,681,127	1,958,226,483
Lumumba Regional Hospital	24,717,192,531	2,471,719,253	24,717,192,531	2,471,719,253	0 -
Jumla ya Kiasi cha Dhamana ya kazi ambayo hakikuwekwa					**19,204,710,352**

Chanzo: Nyaraka za Mkataba na kumbukumbu za Malipo

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa katika miradi kumi (10) iliyotekelezwa, kulikuwa na ongezeko la gharama za mradi na gharama ya ziada ambazo hazikujumuishwa wala kugharamiwa katika hati ya dhamana ya utekelezaji wa kazi.

Wakaguzi walibaini kuwa mradi huo unaofikia jumla ya shilingi 19,204,710,352 haukujumuishwa katika dhamana ya utekelezaji kazi, hali inayoweza kuisababishia Serikali hasara kubwa endapo Wakandarasi watashindwa kukamilisha Miradi. Hali hii imesababishwa na usimamizi usioridhisha wa ufuatiliaji wa vipengele vya mikataba ili kuhakikisha kuwa miradi yote inaekewa dhamana.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba unawaelekeza wakandarasi wote kuongeza mara moja dhamana za utekelezaji wa kazi (Performance Security) kulingana na gharama halisi za mikataba.

3.4.2 Kufanyika kwa malipo ya jumla ya shilingi 82,780,000 kwa ajili ya Michoro baada kukamilika kwa ujenzi (As-Built Drawings) ambayo haikuandaliwa

Kwa mujibu wa kifungu nambari 61.2 cha Masharti ya jumla ya mkataba na kifungu nambari 28 cha Masharti maalum ya mkataba, kinaeleza kuwa baada ya kukamilika kwa mradi, mkandarasi anatakiwa kuwasilisha michoro baada ya kukamilika kwa ujenzi kwa tarehe iliyoelezwa katika masharti maalum ya mkataba.

Ambapo kwa mujibu wa Masharti maalum ya mkataba mkandarasi anatakiwa kuwasilisha michoro baada ya kukamilika kwa ujenzi, ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kukamilika kwa mkataba. Pia, msimamizi wa mradi atatathmini utoshelevu wake wakati wa uwasilishaji.

Wakaguzi walipitia nyaraka za mawasiliano baina ya wasimamizi wa mradi na mkandarasi ili kutambua kama wakandarasi walifanikiwa kuwasilisha michoro baada ya kukamilika kwa ujenzi kulingana na mahitaji ya mkataba na kubainisha kuwa wakandarasi hawakuwalisha kama inavyoelezwa katika mkataba, mchanganuo wa malipo hayo unaoneshwa katika Jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 20: Kiasi kilicholipwa kwa ajili ya uandaaji wa michoro baada kukamilika kwa ujenzi kwa kila mradi

Namba	Jina la mradi	Kiasi (Tsh)
1.	Mbuzini Magharibi A Unguja	24,260,000
2.	Mradi wa Lumumba	-
3.	Chumbuni Mjini Unguja	12,360,000
4.	Magogoni Magharibi B Unguja	23,960,000
5.	Kinyasini Wilaya ya Wete Pemba	12,650,000
6.	Kitogani Wilaya ya Kusini Unguja	-

Namba	Jina la mradi	Kiasi (Tsh)
7.	Micheweni Wilaya ya Micheweni Pemba	3,126,000
8.	Mwera Pongwe Wilaya ya Kati Unguja	1,700,000
9.	Vitongoji Wilaya Chakechake Pemba	750,000
10.	Kivunge Wilaya ya Kaskazini A Unguja	3,990,000
11.	Pangatupu Wilaya ya Kaskazini B Unguja	-
Jumla		**82,780,000**

Chanzo: Nyaraka za mkataba kwa kila mradi

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa miradi nane (8) ililipwa kwa ajili ya kuandaa michoro baada kukamilika kwa ujenzi (As-Built drawings) kwa Wizara ya Afya, ambapo hadi baada ya siku 28 za kukamilika kwa mradi wakandarasi hawakuweza kuwasilisha mchoro baada kukamilika kwa ujenzi, na hadi kufikia tarehe ya ukaguzi hakukuwa na barua rasmi ya kuwasilisha michoro hiyo na nyaraka kamili za michoro. Hali hii imesababishwa na kushindwa kusimamiwa kwa masharti ya mkataba na msimamizi wa mradi.

Kushindwa kuwasilisha michoro baada ya kukamilika kwa ujenzi (As-Built drawings) kunaweza kuipelekea Serikali kupata hasara ya jumla ya shilingi 82,780,000.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba unawataka wakandarasi kuwasilisha michoro baada ya kukamilika kwa Ujenzi (As-built Drawing).

3.4.3 Kuchelewa kwa Uwasilishaji wa michoro mara baada ya Ujenzi kukamilika (As-Built drawings) kutoka kwa mkandarasi kusababisha kuwepo kwa madai ya shilingi 1,438,582,969.36 ambayo Wakandarasi wanatakiwa kulipa

Kwa mujibu wa kifungu nambari 61.2 cha masharti ya jumla ya mkataba na kifungu nambari 28 cha masharti maalum ya mkataba inaelezwa kuwa baada ya kukamilika kwa mradi, mkandarasi anatakiwa kuwasilisha michoro iliyojengwa kwa tarehe iliyoelezwa katika masharti maalum ya mkataba. Ambapo kwa mujibu wa Masharti maalum ya mkataba mkandarasi anatakiwa kuwasilisha michoro baada ya kukamilika kwa ujenzi (As-Built Drawings) ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kukamilika kwa mkataba na ikiwa ucheleweshaji wa kuwasilisha utatokea mkandarasi ataadhibiwa kwa kulipa asilimia 2 ya bei ya mkataba.

Wakaguzi walipitia nyaraka za mawasiliano kwa utekelezaji wa miradi ili kutathmini uwasilishaji wa michoro mara baada ya Ujenzi kukamilika na kubaini kuwa wakandarasi hawakuwasilisha michoro baada ya kukamilika kwa ujenzi kulingana na tarehe ilioekwa katika mkataba, hivyo, kunafanya kuwepo kwa ucheleweshwaji wa kuchelewa kwa tarehe yoyote ambayo watawasilisha. Maelezo zaidi yanaonyeshwa katika jadweli hapa chini:-

Jadweli Nambari 21: Kuchelewa kuwasilisha michoro mara baada ya Ujenzi kukamilika hadi tarehe ya Ukaguzi 31 Julai, 2023

Namba	Jina la mradi	Kiasi cha Kuzuiwa (Tsh)	Tarehe ya Kukamilisha kazi	Tarehe ya kuanza kuwasilisha michoro baada kukamilika kwa ujenzi	Tarehe halisi ya Uwasilishaji wa michoro baada kukamilika kwa ujenzi	Kuchelewa (Siku)
1.	Mbuzini Wilaya ya Magharib A Unguja	97,080,882.84	29/05/2023	27/06/2023	Haikuwasilishwa	34
2.	Mradi wa Lumumba	494,343,850.62	13/06/2023	12/07/2023	Haikuwasilishwa	19
3.	Chumbuni Wilaya ya Mjini Unguja	101,422,978.10	29/05/2023	27/06/2023	Haikuwasilishwa	34
4.	Magogoni Wilaya ya Magharib B Unguja	96,004,243.24	29/05/2023	27/06/2023	Haikuwasilishwa	34
5.	Kinyasini Wilaya ya Wete Pemba	95,656,876.03	29/05/2023	27/06/2023	Haikuwasilishwa	34
6.	Kitogani Wilaya ya Kusini Unguja	99,534,659.35	03/01/2023	01/02/2023	18/04/2023	76
7.	Micheweni Wilaya ya Micheweni Pemba	90,135,278.41	29/05/2023	27/06/2023	Haikuwasilishwa	34
8.	Mwera Pongwe Wilaya ya Kati Unguja	87,423,849.41	07/01/2023	05/02/2023	Haikuwasilishwa	176
9.	Vitongoji Wilaya ya Chakechake Pemba	90,327,772.87	29/05/2023	27/06/2023	Haikuwasilishwa	34
10.	Kivunge Wilaya ya Kaskazini A Unguja	97,080,882.84	29/05/2023	27/06/2023	Haikuwasilishwa	34
11.	Pangatupu Wilaya ya Kaskazini B Unguja	89,571,695.65	29/05/2023	27/06/2023	Haikuwasilishwa	34
Jumla (Tsh)		**1,438,582,969.36**				

Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi juu ya nyaraka za mawasiliano ya miradi

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa Wizara ya Afya haikuzuia kiasi cha fedha ambacho kinatokana na kuchelewa kuwasilisha michoro kulingana na mahitaji ya mradi. Ni mkandarasi mmoja tu aliyeweza kuwasilisha lakini uwasilishaji wake bado ulikuwa umechelewa.

Hali hii imesababishwa na usimamizi usioridhisha wa msimamizi wa mradi katika utekelezaji wa masharti maalum ya mikataba inayoifanya Wizara ya Afya kupoteza kiasi cha jumla ya shilingi 1,438,582,969.36.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba inakusanya kiasi kilichotajwa katika kila mkataba kutoka kwa wakandarasi kulingana na matakwa ya mkataba.

3.4.4 Kukosekana kwa kumbukumbu ya upimaji na kukabidhi vifaa vyenye thamani ya jumla ya shilingi 2,158,128,149.71

Kwa mujibu wa kifungu nambari 61.2 cha masharti ya jumla ya mkataba na kifungu nambari 28 cha masharti maalum ya mkataba inaelezwa kuwa baada ya kukamilika kwa mradi, mkandarasi anatakiwa kuwasilisha mwongozo wa uendeshaji wa vifaa vyote (Operation Manual) ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kukamilika kwa mkataba na ikiwa ucheleweshaji wa kuwasilisha utatokea mkandarasi ataadhibiwa kwa kulipa asilimia 2 ya bei ya mkataba.

Wakaguzi walipitia madai (penultimate) ambayo yalitolewa na wakandarasi ili kutathmini upatikanaji wa vitu ambavyo vilitakiwa kupimwa kabla ya kukabidhiwa na kubainisha kuwa vitu hivyo vilitolewa kama vilivyohitajika. Hata hivyo, Ukaguzi uliomba kupatiwa ripoti za upimaji wa ubora wa vifaa vilivyoainishwa na kubainisha kuwa hakukuwa na ripoti yoyote iliyowasilishwa katika miradi kumi (10) ambapo Mradi mmoja (1) tu wa ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba ndio ulifanikisha kuvipima vifaa hivyo. Mchanganuo unaonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 22: Malipo ya vifaa ambavyo havikupimwa wala kukabidhiwa

Namba	Jina la mradi	Thamani ya vifaa vilivyotumika katika ujenzi (Tsh)
1.	Mbuzini Wilaya Magharibi A Unguja	132,115,400.00
2.	Mradi wa Lumumba Mkoa wa Mjini Unguja	111,562,200.00
3.	Chumbuni Wilaya ya Mjini Unguja	242,048,000.00
4.	Magogoni Wilaya ya Magharibi B Unguja	127,615,400.00
5.	Kinyasini Wilaya ya Wete Pemba	198,605,200.00
6.	Kitogani Wilaya ya Kusini Unguja	
7.	Micheweni Wilaya ya Micheweni Pemba	660,888,990.00
8.	Mwera Pongwe Wilaya ya Kati Unguja	1,800,000.00
9.	Vitongoji Wilaya ya Chakechake Pemba	290,708,359.71
10.	Kivunge Wilaya ya kaskazini A Unguja	504,346,800.00
Jumla		**2,158,128,149.71**

Chanzo: 'Penultimate' zilizoandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi

Hata hivyo, Ukaguzi uliomba ripoti za vipimo lakini hakukuwa na ushahidi kwamba vifaa hivyo vilifanyiwa vipimo na kukabidhiwa.

Jadweli la hapo juu linaonyesha kuwa vitu vyenye thamani ya jumla ya shilingi 2,158,128,149.71 havikufanyiwa vipimo kabla ya kukabidhiwa kwa Wizara ya Afya na hii imesababishwa na usimamizi usio mzuri wa masharti ya mkataba na kupelekea kutokuwa na uhakika wa ubora wa vifaa vilivyotumika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba vifaa hivi vinapimwa na vyombo vinavyoaminiwa kutoka Serikalini kwa kushirikiana na ZBS kwa ajili ya kuhakiki vifaa hivyo kabla ya kutoa cheti cha kukamilika kwa Mradi.

3.4.5 Kiasi cha shilingi 3,565,705,391.59 ambazo hazikudaiwa ikiwa ni fidia kutokana na kuchelewa kukamilika kwa miradi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 62.2 (g) cha masharti ya jumla ya mkataba na kifungu nambari 29 cha masharti maalum ya mkataba vinaeleza kuwa mwajiri atadai fidia za kuchelewa kukamilika kwa mradi. Fidia ya kuchelewesha kukamilika kwa mradi itakuwa asilimia 0.1 ya bei ya mkataba ambapo haitazidi asilimia 10 ya ongezeko la ziada la siku za ucheleweshwaji.

Ukaguzi ulipitia Nyaraka za mawasiliano juu ya usimamizi wa muda wa mradi na kubaini kuwa miradi yote kumi na moja (11) ilichelewa kukamilika licha ya kwamba kulikuwa na upatikanaji wa muda ulioidhinishwa wa kukamilisha miradi.

Aidha, wakaguzi walipitia idhini ya ongezeko la muda wa kumalizika kwa miradi yote na barua zinazoonesha onyo la mwisho lililotolewa na Wizara ya Afya kwa wakandarasi, tathmini ya ukaguzi juu ya utekelezaji wa muda wa kukamilika kwa miradi ilibaini kuwa miradi yote ilichelewa kukamilika kwa zaidi ya tarehe iliyopangwa. Maelezo zaidi yamefafanuliwa katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 23:Gharama za tozo ya adhabu ya kushindwa kumaliza kazi kwa wakati

Jina ya Mradi	Thamani ya Mkataba (Tsh) A	Tozo ya adhabu ya ucheleweshwaji kwa siku (Tsh) (0.1% x A) = B	Makadirio ya kumalizika kazi	Tarehe halisi ya kukamilika kazi	Idadi ya siku za ucheleweshwaji Mradi C	Jumla ya Tozo ya adhabu ya ucheleweshwaji (Tsh) (BxC)
Mbuzini Magharibi A Unguja	4,854,044,142	4,854,044.14	31/08/2022	16/01/2023	138	485,404,414.20
Lumumba Mkoa wa Mjini Unguja	24,717,192,531	24,717,192.53	22/05/2023	30/06/2023	39	963,970,508.71
Mwera Pongwe Wilaya ya Kati Unguja	5,071,148,905	5,071,148.91	15/12/2022	10/02/2023	57	289,055,487.59
Magogoni Magharibi B Unguja	4,800,212,162	4,800,212.16	-	29/05/2023	0	0
Kinyasini Wilaya Wete Pemba	4,782,843,802	4,782,843.80	31/01/2023	29/05/2023	118	478,284,380.2
Kitogani Wilaya Kusini Kati Unguja	4,976,732,968	4,976,732.97	30/10/2022	16/01/2023	78	388,185,171.50
Michelweni Wilaya ya Micheweni Pemba	4,506,763,921	4,506,763.92	20/11/2022	03/01/2023	44	198,297,612.52
Chumbuni Magharibi A Unguja	4,371,192,471	4,371,192.47	30/11/2022	16/01/2023	47	205,446,046.14
Vitongoji Wilaya ya Chake chake Pemba	4,516,388,643	4,516,388.64	-	29/05/2023	0	0
Kivunge Kaskazini A Unguja	4,854,044,142	4,854,044.14	31/10/2022	10/02/2023	102	485,404,414.2
Pangatupu Wilaya ya Kaskazini B Unguja	4,478,584,783	4,478,584.78	31/12/2022	16/01/2023	16	71,657,356.53
Jumla	71,929,148,470	**71,929,148.46**				**3,565,705,391.59**

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka katika Nyaraka za mawasiliano za mradi, 2023

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa miradi yote ilichukua muda wa ziada kuliko muda ulioekwa wa kukamilika kwa mradi. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Wizara ya Afya za kutoa barua za onyo kwa wakandarasi kuwataka kukamilisha miradi kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba, Wizara ya Afya ilishindwa kuchukua hatua ya kudai fidia kwa mujibu wa makubaliano ya masharti ya mkataba.

Hivyo, masharti yasiyotekelezeka ya mkataba huo yanasababisha kuwepo kwa madai ya jumla ya shilingi 3,565,705,391.59 ikiwa ni fidia ya kuchelewesha kukamilika kwa mradi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba unadai fidia ya kuchelewesha kukamilika kwa mradi kulingana na mahitaji ya mkataba kutoka kwa wakandarasi wote.

3.4.6 Kushindwa kudai jumla ya shilingi 163,800,000 kutoka kwa wakandarasi walioshindwa kuwasilisha mapitio ya mpango kazi

Kwa mujibu wa kifungu cha 30.3 cha masharti maalum ya mkataba, kinamtaka mkandarasi kuwasilisha mpango kazi uliorekebishwa kwa kila mwezi na gharama za uchelewashaji wa kuwasilishwa kwa mapitio ya mpango kazi zitakuwa ni jumla ya shilingi 1,000,000.

Wakaguzi walipitia nyaraka za mawasiliano kwa miradi ili kutathmini uwasilishaji wa mpango kazi uliorekebishwa na kubaini kuwa kifungu hicho cha mkataba hakikutekelezwa na wakandarasi wote kulingana na masharti maalum ya mkataba, kama ilivyoelezwa katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 24: Idadi ya miezi na kiasi husika cha kuzuiliwa kwa ucheleweshwaji wa kuwasilisha mpango kazi kwa kila mwezi

Namba	Jina la mradi	Tarehe ya kusainiwa + mwezi 1	Tarehe ya kukamilika	Idadi ya Mwezi	Jumla ya kiasi (Tsh)
1.	Mbuzini Wilaya ya Magharibi A Unguja	15/12/2021	16/01/2023	13.2	13,233,333
2	Mradi wa Lumumba	07/02/2022	30/06/2023	16.9	16,933,333
3.	Chumbuni Wilaya ya Mjini Unguja	15/12/2021	16/01/2023	13.2	13,233,333
4.	Magogoni Wilaya ya Magharib B Unguja	15/12/2021	29/05/2023	17.7	17,666,667
5.	Kinyasini Wilaya ya Wete Pemba	15/12/2021	29/05/2023	17.7	17,666,667

Namba	Jina la mradi	Tarehe ya kusainiwa + mwezi 1	Tarehe ya kukamilika	Idadi ya Mwezi	Jumla ya kiasi (Tsh)
6.	Kitogani Wilaya ya Kusini Unguja	15/12/2021	16/01/2023	13.2	13,233,333
7.	Micheweni Wilaya ya Micheweni Pemba	15/12/2021	03/01/2023	12.8	12,800,000
8.	Mwera Pongwe Wilaya ya Kati Unguja	15/12/2021	10/02/2023	14.1	14,066,667
9.	Vitongoji Wilaya ya Chakechake Pemba	15/12/2021	29/05/2023	17.7	17,666,667
10.	Kivunge Wilaya ya Kaskazini A Unguja	15/12/2021	10/02/2023	14.1	14,066,667
11.	Pangatupu Wilaya ya Kaskazini B Unguja	15/12/2021	16/01/2023	13.2	13,233,333
Jumla					**163,800,000**

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa wakandarasi wote walifanikiwa kuwasilisha mpango wa kazi wa awali lakini walishindwa kuwasilisha mpango kazi ulioboreshwa kulingana na makubaliano ya mkataba. Bila kujali ukosefu wa utekelezaji, Wizara imeshindwa kuzuia kiasi kilichotajwa kwa mujibu wa mikataba yenye thamani ya jumla ya shilingi 163,800,000.

Hali hii imesababishwa na usimamizi usioridhisha kwa msimamizi wa mradi ili kuhakikisha kuwa mipango yote ya kazi inarekebishwa na kuboreshwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba unazuia kiasi kilichotajwa katika mkataba kutoka kwa wakandarasi wote kwa kiasi husika kabla ya taratibu za mwisho za hesabu (Final Account).

3.4.7 Kuwepo kwa wataalamu wanaofanya kazi bila ya kuwa na usajili wa Bodi ya Wakandarasi (ERB) kwa mujibu wa sheria za nchi

Kwa mujibu wa kifungu cha 14 (2) cha Sheria ya ERB, kinaeleza kuwa hakuna mtu atakayeajiri au kuendelea kuajiri mhandisi mtaalamu au mtu yeyote ambaye si mhandisi aliyesajiliwa.

Ukaguzi umebaini kupitia mapitio ya mikataba na ripoti za mkutano katika maeneo ya ujenzi kwa wakandarasi wote na kubainisha kuwa kampuni mbili (2) kati ya kumi na moja (11) zilihusika na wataalam wa kigeni katika utekelezaji wa kazi zao. Hata hivyo, Wakaguzi walibaini kuwepo kwa watumishi kumi (10) ambao hawakuwa na usajili na kibali cha ERB kulingana na mahitaji ya sheria ambapo watatu (3) ni kutoka katika Mradi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba, sita (6) kutoka Mradi wa Hospitali ya Wilaya Chumbuni, na mmoja kutoka Mradi wa Hospitali ya Wilaya Kinyasini.

Hali hii imesababishwa na Wizara kushindwa kusimamia vyema matakwa ya kisheria. Aidha, imepelekea kupoteza mapato kwa Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) ya jumla ya shilingi 16,157,500 na pia, inapelekea kukosekana kwa uhakika wa utaalamu wa wageni wanaohusika na miradi hio, majina ya wataalamu hao yanaonnekana katika **Kiambatisho nambari 1.**

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba wataalamu kutoka nje ya nchi wanafuata sheria za nchi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

3.4.8 Kuwepo kwa wataalamu wanaofanya kazi bila kuwa na vibali vya kazi kwa kufuata sheria za nchi

Kifungu cha 3(1) cha sheria ya uajiri kwa watu wasio na uraia (CAP.436) kinaeleza kuwa mwajiri yeyote anayeishi Tanzania Bara na anayetaka kushiriki kazi yoyote ataomba kwa Kamishna wa Kazi kupata kibali cha kazi.

Kupitia mapitio ya mikataba na ripoti za mkutano wa katika maeneo ya ujenzi kwa wakandarasi wote ukaguzi umebaini kuwa kampuni mbili (2) kati ya kumi na moja (11) zilihusika na wataalam wa kigeni katika utekelezaji wa kazi zao. Hata hivyo, Wakaguzi walibaini kuwepo kwa watumishi kumi (10) ambao hawakuwa na vibali vya kazi kulingana na mahitaji ya sheria, ambapo watatu (3) kutoka katika Mradi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba, sita (6) kutoka Mradi wa Hospitali ya Wilaya Chumbuni, na mmoja (1) kutoka Mradi wa Hospitali ya Wilaya Kinyasini.

Hali hii imesababishwa na Wizara kushindwa kusimamia vyema matakwa ya kisheria. Hali hii imepelekea kupoteza mapato kwa Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) ya jumla ya shilingi 12,500,000 na pia, inaweka hatarini usalama wa taifa kwani hatuna uhakika kuhusu wageni wanaotumika katika miradi inayotekelezwa nchini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba wataalamu kutoka nje ya nchi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi wanafuata sheria za nchi.

3.4.4 Malipo ya jumla ya shilingi 228,755,000 kwa wakandarasi kwa kazi ambazo bado hazijatekelezwa

Kifungu cha 40.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GC) baina ya Wizara ya Afya (MOHZ) na wakandarasi kinaeleza kuwa makisio ya gharama za ujenzi zinatumika kuhesabu bei ya mkataba. Mkandarasi atalipwa kwa kazi aliyofanya kwa kiwango kilichoainishwa katika makisio ya gharama za ujenzi.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya (vyeti vya penultimate) malipo halisi yaliofanywa kwa mkandarasi, Ukaguzi ulibainisha kuwa, mkandarasi aliwasilisha maombi na kufanyiwa malipo ya kazi zote ambazo zimeainishwa katika mkataba, aidha kupitia Ukaguzi uliofanywa, Wakaguzi walibaini uwepo wa malipo yaliofanyika kwa kazi ambazo hazikutekelezwa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba, Jadweli hapo chini linaonesha kazi ambazo hazikutekelezwa lakini zimefanyiwa malipo.

Jadweli Nambari 25: Kiasi kilicholipwa kwa kazi ambazo mkandarasi hajazitekeleza

Maelezo	Kiasi kilicholipwa kwa Wakandarasi kwa ajili ya upimaji, michoro baada ya Ujenzi kukamilika na (sterilizing) kwa Hospitali za Wilaya										Jumla ya Kiasi Kilicholipwa
	Micheweni	Mbuzini	Kivunge	Pongwe	Vitongoji	Chumbuni	Pangatupu	Kinyasini	Magogoni	Kitongani	
Kuruhusu (sterilizing) mitambo yote ya usambazaji wa maji	1,140,000	20,000,000	500,000	700,000	0	10,000,000	5,850,000	12,000,000	20,000,000	150,000	70,340,000
Upimaji wa mabomba na Misingi kwa Unyevu wa maji; Ukali wa hewa na utendaji	600,000	12,000,000	400,000	700,000	0	10,500,000	3,350,000	9,600,000	12,000,000	200,000	49,350,000
upimaji na kukabidhi ufungaji wa umeme kwa ujumla	1,000,000	3,500,000	1,350,000	700,000	0	4,560,000	0	12,000,000	3,500,000	1,350,000	27,960,000
Mchoro baada ya Ujenzi kukamilika	3,060,000	24,260,000	4,475,000	1,600,000	750,000	7,160,000	1,000,000	14,000,000	23,900,000	900,000	81,105,000
	5,800,000	**59,760,000**	**6,725,000**	**3,700,000**	**750,000**	**32,220,000**	**10,200,000**	**47,600,000**	**59,400,000**	**2,600,000**	**228,755,000**
Jumla ya kiasi kilicholipwa kwa ajili ya kupima, michoro baada ya Ujenzi Kukamilika na 'sterilizing'											**228,755,000**

Chanzo; Kutembelea maeneo ya Ujenzi pamoja na Ukaguzi wa vyeti vya malipo, 202

Jadweli hapo juu linaonyesha kiasi kilicholipwa kwa mkandarasi kwa kazi ambayo haikutekelezwa kulingana na nyaraka za makisio ya gharama za ujenzi katika mkataba. Serikali ililipa jumla ya kiasi cha shilingi 228,755,000 kwa wakandarasi kwa kazi ambazo bado hazikuwa zimetekelezwa na wakandarasi, na kupelekea kuwepo kwa upotevu wa fedha za Serikali.

Wakandarasi hao walidai malipo hayo kwa ajili ya kutengenezea mabomba ya maji, upimaji na kukabidhi pamoja na kuandaa 'michoro baada ya ujenzi kukamilika' ya majengo ya hospitali. Wakandarasi wote walipokea malipo ya shughuli zilizotajwa isipokuwa mkandarasi wa hospitali ya Vitongoji ambaye alilipwa kwa ufungaji wa Vipoza hewa.

Ukaguzi haukuona au kupokea ripoti yoyote ya upimaji kutoka kwa Wizara, iliyoidhinishwa michoro ya baada ya ujenzi kukamilika na ripoti ambazo zinaonyesha kuweka mitambo yote ya usambazaji wa maji lakini, ukaguzi ulibaini malipo tayari yamefanywa kwa shughuli hizo. Kuruhusu upimaji ni muhimu sana kwa sababu husaidia kuonesha maeneo ambayo yanaweza kusababisha hitilafu na kusaidia kuyatengeneza kabla ya hospitali kuanza kutumika.

Aidha, upimaji wa mabomba yote na mifereji ya maji ni muhimu sana katika majengo kwa sababu husaidia kuelezea maeneo ya kuvuja. Kushindwa kufanya hivyo husababisha kuvuja kwa maji na kuharibu jengo. Hii imeweza kuonekana na timu ya wakaguzi wakati wa kutembelea Hospitali ya Vitongoji ambapo mabomba ya maji yalianza kuvuja kabla ya matumizi rasmi ya jengo hilo.

Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa usimamizi wa karibu wa timu ya msimamizi wa mradi ambayo ilikuwa na jukumu la kuwaongoza wakandarasi ili kuzingatia matakwa ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba jumla ya shilingi 228,755,000 zinarejeshwa Serikalini kutoka kwa wakandarasi.

Aidha, Wizara iongeze usimamizi katika upimaji na uandaaji wa miradi ya baadae ili kuepusha upotevu wa fedha za mradi.

3.4.5 Malipo ya jumla ya shilingi 11,750,000 kwa wakandarasi kwa faida na mahudhurio (Profit and General Attendance) ya jumla ya kandarasi ndogo ndogo za Ujenzi (Sub-contracted works)

Kifungu B19 (a) cha viwango vya Upimaji wa Ujenzi wa Afrika Mashariki, 1976 kinaeleza kwamba, Kazi ambazo zinatakiwa kufanywa na mkandarasi mdogo aliyeteuliwa apewe kama gharama ya ziada au gharama za juu ambazo ni sawa na kifungu hicho hicho (b) kinachosema mahudhurio ya wakandarasi wadogo

waliochaguliwa yatatolewa kama kitu katika kila jambo na itachukuliwa kuwa ni pamoja na kuruhusu matumizi ya (scaffolding, Mess rooms, sanitary accomodation) vifaa vya ustawi; kuwezesha upatikanaji wa nafasi za huduma za Afisi na uhifadhi wa mimea na vifaa; kuwezesha upatikanaji wa mwanga na maji kwa ajili ya kazi zao; kuondoa takataka. Mahudhurio maalum yatatolewa kama kitu katika kila kazi ili kuweza kutoa maelezo (kwa mfano kupakua; kuhifadhi; kuinua; kuweka nafasi; kutoa nguvu; kutoa (scaffolding) maalum). Vivyo hivyo, kifungu A7 (ii) kinahitaji neno "jumla ya gharama ya msingi" ambayo inamaanisha jumla ya kazi au huduma zilizotolewa na mkandarasi aliyeteuliwa, mamlaka ya kisheria, au kazi ya umma au kwa vifaa au bidhaa kupatikana kutoka kwa muuzaji aliyeteuliwa.

Mapitio ya timu ya ukaguzi juu ya vyeti vya mwisho vya malipo yaliyofanywa kwa mkandarasi pamoja na kutembelea maeneo yaliyofanyika Ujenzi wa hospitali, yalibaini kuwa wakandarasi walidai na kulipwa kwa faida na mahudhurio ya jumla (Profit and General attendance) kwa kazi za ziada zilizofanywa na mkandarasi mkuu, kwa kawaida faida na mahudhurio ya jumla yanalipwa kwa mkandarasi mkuu kwa kazi iliyofanywa na wakandarasi wadogo wa ndani kama ilivyoelezwa kwenye jadweli hapa chini:-

Jadweli Nambari 26: Faida na Mahudhurio ya Jumla kwa Wakandarasi Wakuu

Jina la Mradi wa Ujenzi	Maelezo	Kiasi Katika Mkataba	Faida (Tsh)	Mahudhurio ya jumla	Kiasi kilicholipwa kwa Mkandarasi (Tsh)
Hospitali ya Wilaya ya Pangatupu	Special Doors	0	4,700,000.00	2,350,000.00	7,050,000.00
Hospitali ya Wilaya Kitogani	Special Doors	0	4,700,000.00	0	4,700,000
Jumla ya kiasi			**9,400,000.00**	**2,350,000.00**	**11,750,00.00**

Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi, 2023

Jadweli hapo juu linaonyesha kiasi cha faida na mahudhurio ya jumla yaliyolipwa kwa wakandarasi kwa kazi iliyotekelezwa na mkandarasi mkuu kama faida na mahudhurio ya jumla ambayo yalikuwa shilingi 9,400,000.00 na shilingi 2,350,000.00. Kwa ujumla, faida na mahudhurio ya jumla yalilipwa kwa mkandarasi mkuu kutoa msaada kwa wakandarasi wa ndani wakati wa utekelezaji wa kazi ikiwa ni pamoja na kuhifadhi vifaa, utoaji wa umeme na maji.

Hali hii imesababishwa na kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa mradi na kutokuwepo kwa ushauri wa upimaji wa kazi iliyofanyika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba jumla ya shilingi 11,750,000 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) zinarejeshwa Serikalini ili kuiepushia kuitia hasara Serikali itokanayo na kufanyika kwa malipo mara mbili kwa wakandarasi hao.

3.4.6 Kufanyika kwa Malipo ya ziada ya jumla ya shilingi 51,358,913 kwa ajili ya bima na dhamana ya usalama wa miradi ya Hospitali Kumi za Wilaya

Kifungu cha 14.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kati ya Wizara ya Afya na mkandarasi kinamtaka mkandarasi atoe, majina ya pamoja ya Mwajiri na mkandarasi, bima ya usalama wa mradi kuanzia tarehe ya kuanza hadi mwisho wa Kipindi cha Dhima ya muda wa uangalizi wa kazi iliyofanyika, kwa kiwango kilichotajwa katika Masharti Maalum ya Mkataba kwa mambo yafuatayo ambayo ni kutokana na hatari za mkandarasi; (a) Kupoteza au kuharibu Kazi, Mitambo na Vifaa (b) Kupoteza au uharibifu wa Mashine (c) Kupoteza au uharibifu wa mali (isipokuwa kazi, mitambo, mashine na vifaa) kuhusiana na mkataba na (d) kupata jeraha la kibinafsi au kifo.

Aidha, kifungu cha 55.1 cha masharti ya jumla ya mkataba baina ya Wizara ya Afya na Mkandarasi kinahitaji dhamana ya utendaji kazi iwasilishwe kwa mwajiri kabla ya tarehe iliyoainishwa katika barua ya kukubali tuzo na inapaswa kutolewa kwa kiasi na fomu ya benki au dhamana inayokubalika na mwajiri. Dhamana ya utendaji kazi inapaswa kuwa halali hadi siku 28 kabla ya utolewaji wa cheti cha kukamilka kwa kazi ikiwa ni kwa njia ya dhamana ya kibenki, na kwa upande wa dhamana ya utendaji italazimu kutumika hadi kwa kipindi cha mwaka mmoja baada ya kukabidhishwa kwa cheti cha kukamilika kwa kazi (Perfomance Bond).

Ukaguzi ulipitia nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi na vyeti vya (Penultimate) kubainisha kuwa wakandarasi walidai na kulipwa kwa ajili ya bima ya vihatarishi kwa hospitali za Wilaya ya Micheweni, Vitongoji, Pangatupu na Kinyasini kwa gharama za jumla ya shilingi 27,000,000, shilingi 27,000,000, shilingi 27,000,000 na shilingi 8,600,000 ambapo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba Wizara ya Afya haikupaswa kufanya malipo hayo, mchanganuo wa malipo hayo unaainishwa katika jadweli hapo chini.

Kwa upande mwingine, ukaguzi ulibaini miradi miwili haikuwasilisha dhamana ya ufanyikaji wa miradi (sureties), miradi hiyo ni Hospitali za Wilaya ya Kinyasini na Hospitali ya Wilaya Pangatupu ambazo hazikupaswa kulipwa kwa kuwa hazikuwa sehemu ya mkataba. Aidha, ukaguzi ulibaini hospitali sita za wilaya hazikutoa bei ya dhamana ya ufanyikaji wa mradi (sureties) katika hati yao ya mkataba, ambapo hospitali hizo za wilaya ni Micheweni, Mbuzini, Vitongoji, Chumbuni, Pangatupu na Magogoni kwa hiyo hazikupaswa kulipwa kwa kuwa hazikuwa kwenye mkataba.

Jadweli Nambari 27: Mkataba na kiasi cha kulipwa cha bima na dhamana (dhamana ya utekelezaji kazi)

Jina la Hospitali ya Wilaya	Hali ya dhamana iliyotolewa (Sureties)	Hali ya Bima iliyotolewa (Insurance Cover)	Gharama ya kutoa dhamana (10%) na bima ya vihatarishi kwa mkandarasi		Kiasi cha Kulipwa kwa Bima na Dhamana (Insurance and surreties) (Tsh)	Malipo yanayostahiki kukatwa kwa kushindwa kuwasilisha dhamana na Bima (Tsh)
			Kiasi cha mkataba kwa ajili ya kutoa dhamana (Sureties) (Tsh)	Kiasi cha mkataba kwa ajili ya kutoa bima (mkandarasi wa bima ya hatari zote) (Tsh)		
Micheweni	Imewasilishwa	Haijajumuishwa	0	27,000,000	20,000,000	20,000,000
Mbuzini	Imewasilishwa	Imejumuishwa	0	27,000,000	27,000,000	0
Kivunge	Imewasilishwa	Imejumuishwa	10,000,000	37,000,000	7,758,913	-39,241,087
Pongwe	Imewasilishwa	Imejumuishwa	30,000,000	11,000,000	41,000,000	0
Vitongoji	Imewasilishwa	Haijajumuishwa	0	27,000,000	30,000,000	30,000,000
Chumbuni	Imewasilishwa	Imejumuishwa	0	27,000,000	27,000,000	0
Pangatupu	Imewasilishwa	Haijajumuishwa	0	27,000,000	34,000,000	34,000,000
Kinyasini	Imewasilishwa	Haijajumuishwa	8,000,000	8,600,000	16,600,000	16,600,000
Magogoni	Imewasilishwa	Imejumuishwa	0	27,000,000	27,000,000	0
Kitongani	Imewasilishwa	Imejumuishwa	10,000,000	7,000,000	7,000,000	-10,000,000
Jumla			**58,000,000**	**225,600,000**	**237,358,913**	**51,358,913**

Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka kwa Nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi, Vyeti vya 'Penultimate' na vyeti vya malipo

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa jumla ya shilingi 51,358,913 zililipwa kwa wakandarasi ikiwa ni malipo ya bima na dhamana (sureties) wakati vitu hivyo havikutolewa dhamana na bima. Hivyo, malipo ya jumla ya shilingi 51,358,913 kwa ajili ya bima na dhamana ya miradi ilisababishwa na ufuatialiaji duni wa bima iliyotolewa na dhamana ya benki kulinganisha na hati ya mkataba. Hali hii imesababisha kuwepo kwa matumizi ya fedha za mradi kwa vitu ambavyo havikutekelezwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba jumla ya shilingi 51,358,913 zinarejeshwa kutoka katika malipo ya wakandarasi ambapo hawakupaswa kulipwa fedha hizo.

SURA YA NNE

4.0 MATOKEO UKAGUZI KUHUSU MRADI WA UJENZI WA HOSPITALI YA MKOA LUMUMBA

4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 28: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba

Vipengele	Maelezo ya Mkataba
Nambari ya Mkataba	NO.SMZ/IMF/H03/W/EP-RNCT/2021/2022/02
Jina la Mkandarasi	ESTIM CONSTRUCTION LTD
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	07 Januari, 2022
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	14 Januari, 2022
Muda wa Mkataba	Miezi 9
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	14 Oktoba, 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	30 Mei, 2023
Gharama za awali pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)	Tsh. 24,717,192,531.32 (pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT))
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)	
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	100%
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai, 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	Tsh. 21,556,123,939.20

4.2 Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Upangaji wa Mipango ya Ujenzi wa Miradi ya Hospitali ya Mkoa Lumumba

Sehemu hii inatoa matokeo ya ukaguzi ya uanzishwaji wa Mradi na mipango katika hatua ya awali na ndio hatua muhimu katika usimamizi wa mradi ili kuweza kufanikiwa. Aidha, sehemu hii inahusisha kufafanua upeo wa mradi, malengo, wahusika, na utoaji masuala muhimu ya mradi, pamoja na kuunda mpango kamili wa kuongoza mradi kutoka mwanzo hadi mwisho. Hapa kunatoa muhtasari wa awamu hizi mbili.

4.3 Matokeo ya Ukaguzi Kuhusiana na mchakato wa ununuzi wa upatikanaji wa Mkandarasi kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Lumumba

Sehemu hii inatoa muhtasari na utangulizi wa mchakato wa ununuzi wa mradi. Ununuzi ni sehemu muhimu ya usimamizi wa mradi ambayo inahusisha kupata bidhaa, huduma, na rasilimali zinazohitajika ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi. Ripoti hii inaelezea dhana muhimu, hatua, na mambo yanayohusika katika mchakato wa ununuzi wa mradi.

4.3.5 Ongezeko la Bei ya Mkataba la jumla ya shilingi 7,585,907,182.55 kutokana na Utoaji wa Mkataba kwa mzabuni asiekuwa na sifa

Kanuni nambari 127 ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya 2020 inamtaka mzabuni mwenye zabuni iliyotathminiwa vizuri kuwa mzabuni aliyefanikiwa.

Tarehe 3 Novemba, 2021 na tarehe 6 Disemba, 2021 Wizara ya Afya ilialika wazabuni watano kupitia zabuni isiyo ya wazi ya ujenzi wa Hospitali Mpya ya Mkoa Lumumba - Unguja, Zanzibar. Zabuni hiyo ilifunguliwa tarehe 17 Disemba 2021, ambapo wazabuni wote watano (5) waliwasilisha zabuni zao kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 29: Bei ya Zabuni iliyowasilishwa kwa ajili ya Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Lumumba

Namba	Mzabuni	Bei za Wakandarasi jumla ya shilingi (Tsh.)
1.	Mohamed Builders Ltd	27,111,455,481.00
2.	Group Six International Ltd	17,131,285,348.77
3.	Estim Construction Co.Ltd	23,971,061,990.86
4.	Hainan International Ltd	22,171,041,316.00
5.	CRJE (East Africa) Limited	23,971,061,990.86

Chanzo: Bei zilizowasilishwa na Ripoti ya tathmini

Ukaguzi ulipitia ripoti ya tathmini na kubaini kuwa, katika hatua ya awali, Group Six International Ltd iliondolewa kutokana na uwasilishaji wa zabuni isiyokamilika kama ni kielelezo namba moja, Masharti ya Jumla na kazi za awali (Preliminaries), hazikuainishwa. Kamati ya tathmini ilipendekeza Estim Construction Co. Ltd apewe mkataba kwa bei iliyosahihishwa ya jumla ya shilingi 24,717,192,531.32 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Tarehe 27 Disemba, 2021 bodi ya Zabuni ilikubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na kamati ya tathmini na kuidhinisha M/s. Estim Construction Co. Ltd kupewa mkataba wa jumla ya shilingi 24,717,192,531.32 ikiwa pamoja na kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Mnamo tarehe 6 Januari, 2021 Wizara ya Afya kupitia barua yenye kumbukumbu namba. AB/42/333/2021/22/141, ilitoa taarifa ya kumjuulisha Estim Construction Co. Ltd kuwa ameshinda tuzo kwa jumla ya shilingi 24,717,192,531.32 pamoja na Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT). Katika tarehe hiyo hiyo, kupitia barua yenye kumbukumbu namba. ECCL/22/1045/DP/dn, Estim Construction Co. Ltd iliiandikia barua Wizara ya Afya kukubali kufanya kazi ya Ujenzi wa Mradi wa Hospitali ya Mkoa ya Lumumba.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya nyaraka za zabuni zilizowasilishwa na kubaini kuwa Group Six International Ltd iliwasilisha nyaraka za Masharti ya Jumla ya Mkataba na kazi za awali (Preliminaries) hata hivyo, ukurasa wa muhtasari haukujumuishwa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 28.4 cha maelekezo ya zabuni, kinatoa fursa kwa Taasisi za Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma kufichua na kuondoa hali yoyote isiyo rasmi au isiyo ya kawaida katika Nyaraka za Zabuni ambayo haijumuishi kuongezeka au kupungua kwa vifaa vya Ujenzi.

Zaidi ya hayo, kifungu cha 28.2 kimefafanua kuwa kuongezeka au kupungua kwa Vifaa vya Ujenzi au kutoridhishwa ni moja ya njia kubwa ya kuathiri upeo, ubora, au utekelezaji wa kazi; Mipaka kwa njia yoyote kubwa ambayo haiendani na hati za Zabuni, Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ina haki na jukumu kwa Wazabuni kurekebisha dosari ambazo zitaathiri uwepo wa uwazi wa ushindani kwa Wazabuni ambao wamewasilisha Zabuni zao.

Ukaguzi umebaini kuwa ukurasa wa muhtasari uliokosekana katika nyaraka za masharti ya jumla ya Mkataba na kazi za awali (preliminaries) haukuwa wenye kuongeza au kupunguza vifaa, na kulingana na kifungu cha 29.2 cha Maelekezo kwa wazabuni (Instruction To Bidders), ikiwa mwajiri atakua na uharaka, basi anaweza kumuomba Mzabuni awasilishe taarifa au nyaraka muhimu ndani ya kipindi cha muda unaofaa ili kuweza kurekebisha dosari katika zabuni inayohusisha mahitaji ya nyaraka hizo ambazo mwanzo zilikataliwa.

Mahojiano ya ukaguzi na maafisa wa Wizara yalibainisha kuwa kupitia barua ya tarehe 15 Disemba, 2021 kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kwamba Kampuni ya M/s Group Six International Ltd iliorodheshwa kama Kampuni iliyozuiliwa kufanya kazi Zanzibar kutokana na utendaji usioridhisha katika mikataba ya awali.

Hata hivyo, kwa mujibu wa kifungu cha 20(13) Usajili wa Wakandarasi wa Zanzibar kwa Sheria [R.E of 2018] unahitaji aina yoyote ya uzembe kwenye maeneo ya Ujenzi inayosababisha kazi mbaya na kutokea kwa dosari za ujenzi kutachukuliwa kama kosa na adhabu ya mkandarasi itakua ni kushushwa daraja kama itakavyoamuliwa na Bodi au kusimamishwa au kufutiwa usajili.

Tarehe 3 Novemba, 2021, Bodi ya Usajili ya Wakandarasi - Zanzibar, kupitia barua na. ZCRB/AB.O1/27, iliwasilisha orodha ya wakandarasi waliosajiliwa Zanzibar wenye madaraja 1, 2, na 3 kama ilivyoombwa na Wizara ya Afya kupitia barua ya tarehe 1 Novemba, 2021 yenye kumbukumbu Na. AB/42/333/73, ambapo kampuni ya M/s. Group Six International Ltd ilijumuishwa kwenye orodha. Hivyo, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi Zanzibar ndio chombo chenye haki ya kuwaorodhesha wakandarasi waliozuiliwa kufanya kazi.

Ukaguzi umebaini kuwa, Uongozi wa Wizara ya Afya umeshindwa kufuata Sheria na kupelekea kuwepo kwa ongezeko la bei ya Mkataba kwa jumla ya shilingi 7,585,907,182.55 kutokana na kumpa Mkataba wenye thamani ya jumla ya shilingi 24,717,192,531.32 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kampuni ya M/s. Estim Construction Co. Ltd na kushindwa kuizawadia kampuni ya M/s. Group Six International Ltd ambayo ilikua na bei ya chini ya jumla ya shilingi 17,131,285,348.77.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unazingatia mapendekezo yanayotolewa na kamati ya tathmini ili kunusuru kujitokeza kwa ongezeko la gharama jambo ambalo linaweza kupelekea kuingiza hasara Serikali.

4.4 Matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa ya Lumumba. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha utekelezaji wa mradi na kuridhika kwa wahusika. Inaelezea vipengele muhimu vya usimamizi wa mkataba mzuri na inasisitiza umuhimu wa mawasiliano ya wazi, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba.

4.4.1 Hasara ya jumla ya shilingi 102,600,000 iliotokana na ufuatiliaji usioridhisha wa ratiba ya mahudhurio ya mshauri elekezi

Wakaguzi walipitia mkataba wa mshauri elekezi wa Hospitali ya Mkoa ya Lumumba na kubaini kuwa utaratibu wa malipo uliowekwa katika masharti maalum ya mkataba wa mshauri elekezi hauwezi kutoa nafasi kwa Wizara ya Afya kufuatilia malipo kwenye ratiba ya mahudhurio ili kutoa tafakari halisi juu ya kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa mshauri elekezi.

Hata hivyo, Wizara ya Afya ilianzisha utaratibu wa malipo kwa kuzingatia hatua zilizokamilika ambazo ziliweka ugumu kufuatilia kiasi halisi kinachotakiwa kulipwa kwa mshauri elekezi, kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapa chini:-

Jadweli Nambari 30: Uchambuzi wa wakati halisi wa mshauri elekezi juu ya usimamizi wa mradi wa ujenzi

Wafanyakazi	Nafasi	Malipo (Tsh)	Muda uliopende kezwa (Months) (Tsh)	Muda halisi (Months) (Tsh)	Tofauti	Kiasi cha ziada (Tsh)
Habib Nuru	Architect	12,000,000	1.8	1	0.8	9,600,000
Mahsen Mahdi	Ast. TL/ Project Manager	10,000,000	1.8	0.74	1.06	10,600,000
Abdulkarid Mohamed	Architect	8,000,000	1.8	0.1	1.7	13,600,000
Awadh Ramadhani	Quantity Surveyor	8,000,000	1.8	0.5	1.3	10,400,000
Mwelulila Mwengwa	Structural/ Civil Engineer	8,000,000	1.8	0.7	1.1	8,800,000
Shariff Sinkara	Mechanical Engineer	8,000,000	1.8	0.07	1.73	13,840,000
Eng. Fadhili Ilala	Electrical Engineer	8,000,000	1.8	0.53	1.27	10,160,000
Allen Ringo	ICT Engineer	8,000,000	1.8	0.4	1.4	11,200,000
Arch. Salim Mshirazy	Architect	6,000,000	0.5	0	0.5	3,000,000
QS. Asha Awadh Ramadhan	Quantity Surveyor	6,000,000	0.5	0	0.5	3,000,000
Eng. Mohamed Noor	Structural Engineer	6,000,000	1	0.1	0.9	5,400,000
Eng. Lameck	Electrical Engineer	6,000,000	0.5	0	0.5	3,000,000
Jumla						**102,600,000**

Chanzo: Mahudhurio ya Wakandarasi katika eneo la ujenzi

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa muda halisi wa timu ya mshauri elekezi hauko sawa na muda uliopendekezwa katika Mkataba.

Hata hivyo, Wakaguzi walibaini kuwa Wizara ya Afya haikuwasilisha Nyaraka za Mkataba huo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupitiwa, hali ambayo ilipelekea kupatikana kwa masharti yasiyofaa ya mikataba kwa Wizara ya Afya.

Ukaguzi umebaini upotevu wa jumla ya shilingi 102,600,000 tangu mkataba huo usainiwe, na kukubaliana juu ya ratiba ya malipo kulingana na bei ya mkataba ambayo iliathiri ufuatiliaji mkubwa wa Wizara ya Afya.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakiksha kuwa kwenye miradi ya baadaye ratiba ya malipo inapaswa kupimwa na ratiba iliyorekodiwa na Mhandisi/Meneja wa Mradi kutoka Wizara ya Afya.

4.4.2 Kukosekana kwa kumbukumbu ya upimaji na kukabidhi vifaa vyenye thamani ya jumla ya shilingi 111,562,200

Kwa mujibu wa kifungu nambari 61.2 cha masharti ya jumla ya mkataba na kifungu nambari 28 cha masharti maalum ya mkataba kinaeleza kuwa baada ya kukamilika kwa mradi, mkandarasi anatakiwa kuwasilisha mwongozo wa uendeshaji wa vifaa vyote (Operation Manual) ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kukamilika kwa mkataba na ikiwa ucheleweshaji wa kuwasilisha utatokea mkandarasi ataadhibiwa kwa kulipa asilimia mbili (2) ya bei ya mkataba.

Wakaguzi walipitia madai (penultimate) ambayo yalitolewa na wakandarasi ili kutathmini upatikanaji wa vitu ambavyo vilitakiwa kupimwa kabla ya kukabidhiwa na kubainisha kuwa vitu hivyo vilitolewa kama vilivyohitajika. Hata hivyo, Ukaguzi uliomba kupatiwa ripoti za upimaji wa ubora wa vifaa vilivyoainishwa na kubainisha kuwa hakukuwa na ripoti yoyote iliyowasilishwa kwa ajili ya upimaji na kukabidhi japo kuwa wakandarasi wa mradi huo walifanikiwa kuvipima.

Hata hivyo, ukaguzi uliomba ripoti za vipimo lakini hakukuwa na ushahidi kwamba vifaa hivyo vilifanyiwa vipimo na kukabidhiwa.

Hivyo, vifaa vyenye thamani ya jumla ya shilingi 111,562,200 havikufanyiwa vipimo kabla ya kukabidhiwa kwa Wizara ya Afya na hii imesababishwa na usimamizi usio mzuri wa masharti ya mkataba na kupelekea kutokuwa na uhakika wa ubora wa vifaa vilivyotumika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakiksha kuwa vifaa hivi vinapimwa na vyombo vinavyoaminiwa kutoka Serikalini kwa kushirikiana na ZBS kwa ajili ya kuhakiki vifaa hivyo kabla ya kutoa cheti cha kukamilika kwa Mradi.

SURA YA TANO

5.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA KITOGANI

5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 31: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kitogani

Vipengele	Maelezo ya Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/EPRNCT/2021/2022/01
Jina la Mkandarasi	Quality Building Contractors limited
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	15 Disemba 2021
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	28 Disemba, 2021
Muda wa Mkataba	Miezi 6
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	27 Juni, 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	30 Oktoba,2022
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tshs. 4,782,843,801.50 (VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tshs. 7,484,531,158.90
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	100%
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	6,659,284,193.30

5.2 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Upangaji wa Mipango ya (Dustify) Ujenzi wa Miradi ya Hospitali ya wilaya Kitogani

Sehemu hii inatoa matokeo ya ukaguzi ya uanzishwaji wa Mradi na mipango katika hatua ya awali na ndio hatua muhimu katika usimamizi wa mradi ili kuweza kufanikiwa. Aidha, sehemu hii inahusisha kufafanua upeo wa mradi, malengo, wahusika, na utoaji masuala muhimu ya mradi, pamoja na kuunda mpango kamili wa kuongoza mradi kutoka mwanzo hadi mwisho. Hapa kunatoa muhtasari wa awamu hizi mbili.

5.3 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usimamizi wa Ununuzi katika Ujenzi wa Miradi ya Hospitali

Sehemu hii inatoa muhtasari na utangulizi wa mchakato wa ununuzi wa mradi. Ununuzi ni sehemu muhimu ya usimamizi wa mradi ambayo inahusisha kupata bidhaa, huduma, na rasilimali zinazohitajika ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi. Ripoti hii inaelezea dhana muhimu hatua, na mambo yanayohusika katika mchakato wa ununuzi wa mradi.

5.4 Matokeo ya ukaguzi kuhusiana na usimamizi wa mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kitogani ambapo inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha mradi unatekelezeka kwa ufanisi kuweza kuwanufaisha wahusika. Vile vile inaelezea mambo muhimu ya usimamizi wa mkataba na kushajihisha umuhimu wa mawasiliano, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba, gharama, wakati na ubora.

SURA YA SITA



6.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA MWERA PONGWE

6.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 32: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe

Vipengele	Maelezo ya Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/EP-RNCT/2021/2022/01
Jina la Mkandarasi	Rans Company limited
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	15 Disemba, 2021
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	23 Disemba, 2021
Muda wa Mkataba	Miezi 6
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	22 Juni, 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tshs 5,071,148,905.00 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	7,489,748,928.00
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	6,879,306,982.53

6.2 Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Upangaji wa Mipango ya Ujenzi wa Miradi ya Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe

Sehemu hii inatoa matokeo ya ukaguzi ya uanzishwaji wa Mradi na mipango katika hatua ya awali na ndio hatua muhimu katika usimamizi wa mradi ili kuweza kufanikiwa. Aidha, sehemu hii inahusisha kufafanua upeo wa mradi, malengo, wahusika na utoaji masuala muhimu ya mradi pamoja na kuunda mpango kamili wa kuongoza mradi kutoka mwanzo hadi mwisho. Hapa kunatoa muhtasari wa awamu hizi mbili.

6.3 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usimamizi wa Ununuzi katika Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe

Sehemu hii inatoa muhtasari na utangulizi wa mchakato wa ununuzi wa mradi. Ununuzi ni sehemu muhimu ya usimamizi wa mradi ambayo inahusisha kupata bidhaa, huduma na rasilimali zinazohitajika ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi. Ripoti hii inaelezea dhana muhimu, hatua na mambo yanayohusika katika mchakato wa ununuzi wa mradi.

6.3.1 Dosari katika ufanyaji wa marekebisho ya makosa wakati wa tathmini ya zabuni

Kanuni ya 123 (2) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020, Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma itarekebisha makosa ya hesabu wakati wa tathmini ya zabuni.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya ripoti ya tathmini na kubaini kuwa kamati ya tathmini ilifanya makosa wakati wa masahihisho ya makosa ya zabuni (Correction of Error) ambapo kamati ya tathmini iliondoa na kurekebisha baadhi ya makosa ya kiasi kilichotajwa katika mjumuisho wa matumizi mengineo (Provisional Sum) na sio kurekebisha makosa ya hesabu kama inavyotakiwa na kwa mujibu wa sheria.

Aidha, kupitia mapitio ya kumbukumbu za majadiliano ya mapatano, Wakaguzi walibaini kuwa makosa ya hesabu yalifanywa na kuthibitishwa wakati wa majadiliano ya mapatano. Hali hii imesababishwa na usimamizi usioridhisha wa upitiaji wa ripoti ya tathmini kabla ya kutolewa tuzo kwa Mzabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unaweka udhibiti ambao unahitaji kitengo cha ununuzi kufanya mapitio ya kina ya ripoti ya tathmini kabla ya kuwasilishwa kwa Bodi ya Zabuni kwa kuidhinishwa.

6.3.2 Ongezeko la Bei ya Mikataba la jumla ya shilingi 350,292,384 kutokana na Utoaji wa Mkataba kwa mzabuni asie na sifa

Kanuni ya 127 ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inamtaka mzabuni mwenye zabuni iliyotathminiwa vizuri kuwa mzabuni aliyefanikiwa.

Kupitia mapitio ya ripoti ya tathmini ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe, Ukaguzi ulibaini kwamba baada ya tathmini kampuni ya M/s. CRJE East Africa Limited ndio ilikua na vigezo vya kuzawadiwa tuzo na kamati ya tathmini ilipendekeza tuzo itolewe kwa mzabuni M/s. CRJE East Africa Limited kwa thamani ya mkataba wenye jumla ya shilingi 4,720,856,520.

Katika kufanya mapitio ya hadidu rejerea za kumbukumbu za kikao cha mapatano, ilibainisha kuwa, tarehe 14 Disemba, 2021 Wizara ya Afya ilifanya kikao cha mapatano na kampuni ya Rans Building Contractors Ltd kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe kwa gharama ya shilingi 5,071,148,905 ikiwa ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa tarehe 14 Disemba 2021, Wizara ya Afya ilitoa taarifa ya tuzo kwa Mzabuni Rans Building Contractors Ltd kuwa ndio mshindi kwa thamani ya shilingi 5,071,148,905 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani.

Utoaji wa tuzo kwa mzabuni ambae hakupendekezwa na kamati ya tathmini kumepelekea ongezeko la shilingi 350,292,384 katika bei ya mkataba (shilingi 5,071,148,905 – shilingi 4,720,856,520) mchanganuo unaonekana katika jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 33 : Mchanganuo wa Mzabuni aliezawadiwa bila ya kuwa na sifa

Jina la Hospitali ya Wilaya	Mzabuni aliyependekezwa na kamati ya tathmini		Mzabuni aliezawadiwa Tuzo		Tofauti (Tsh)
	Jina la Mzabuni	Kiasi (Tsh)	Jina la Mzabuni	Kiasi (Tsh)	
Dunga (Mwera ponge)	CRJE (East Africa) Limited	4,720,856,520	Rans Building Contractors Ltd	5,071,148,905	350,292,384

Chanzo: Ripoti ya tathmini, hadidu rejea za bodi ya zabuni na mkataba

Jadweli hapo juu, linaainisha ongezeko la kiasi cha shilingi 350,292,384 katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe lililosababishwa na kumzawadia tuzo mkandarasi ambae hakufikia vigezo kwa mujibu wa ripoti ya tathmini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unazingatia mapendekezo yanayotolewa na kamati ya tathmini ili kunusuru kujitokeza kwa ongezeko la gharama jambo ambalo linaweza kupelekea kuingiza hasara Serikali.

6.4 Matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha utekelezaji wa mradi na kuridhika kwa wahusika. Inaelezea vipengele muhimu vya usimamizi wa mkataba mzuri na inasisitiza umuhimu wa mawasiliano ya wazi, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba.

6.4.1 Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe iliyopelekea ulipaji wa malipo za ziada kwa mkandarasi ya jumla ya shilingi 237,896,500.

Kifungu cha 45.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kati ya Wizara ya Afya na mkandarasi kinamtaka msimamizi wa mradi kupima thamani ya kazi inayotekelezwa. Vile vile, kifungu cha 45.4 cha mkataba huo kinahitaji thamani ya kazi inayotekelezwa kujumuisha thamani ya kiasi cha vitu katika Nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi iliokamilishwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya vyeti vya 'Penultimate' kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe na kulinganisha na vipimo vya kazi halisi iliofanyika eneo la ujenzi, Ukaguzi ulibaini uwepo wa malipo ya jumla ya shilingi 237,896,500.00 yaliolipwa kwa mkandarasi kwa ajili ya kazi ambazo zilikua hazijatekelezwa kama inavyoainishwa katika **Kiambatisho Nambari 2.**

Malipo hayo ya ziada yalisababishwa na kukosekana kwa vipimo vya pamoja baina ya Wizara ya Afya, mkandarasi na mshauri elekezi, ambapo ukaguzi ulibaini kuwa vipimo hivyo viliandaliwa na mkandarasi pekee bila ya uwepo wa Wizara ya Afya, ambapo Wizara ya Afya ilifanya zoezi la uthibitisho wa vipimo hivyo bila ya kufanya uhakiki wa upimaji.

Aidha, imebainika kuwepo kwa dosari katika maandalizi ya michoro ya miundo pamoja na (bar-bending schedule) ilikua ni miongoni mwa sababu zilizopelekea ongezeko katika malipo.

Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe ilikua ni miongoni mwa sababu iliyopelekea Wizara ya Afya kufanya malipo ya ziada kwa mkandarasi kwa kulinganisha na kazi halisi iliofanywa, hali hiyo imeipelekea Serikali kufanya matumizi yasiokuwa na tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya upembuzi yakinifu wa kazi zote zilizofanywa kabla ya malipo ya mwisho kwa mkandarasi ili kuhakikisha malipo yanaendana na kazi halisi iliofanyika kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba na kuhakikisha wanafanya uhakiki wa kazi zote zinazolipwa kwa mkandarasi.

HOSPITALI YA WILAYA
MBUZINI
DISTRICT HOSPITAL

SURA YA SABA


MUONGOZO WA MADAKTARI

7.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA MBUZINI

7.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 34: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mbuzini

Vipengele	Maelezo ya Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/EP-RNCT/2021/2022/01- Lot 3
Jina la Mkandarasi	M/s CRJE (EAST AFRICA) Limited
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	15 Disemba, 2021
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	23 Disemba, 2021
Muda wa Mkataba	Miezi 6
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	22 Juni, 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	31 Agosti, 2022
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Jumla ya shilingi 3,838,930,346.88 (Bila ya VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	6,518,368,655.70
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	100%
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	6,237,971,135.89

7.2 Matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbuzini. Vile vile inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha utekelezaji wa mradi na kuridhika kwa wahusika ambapo inaelezea vipengele muhimu vya usimamizi wa mkataba mzuri na inasisitiza umuhimu wa mawasiliano ya wazi, nyaraka na kuzingatia masharti ya mkataba.

Aidha, sehemu hii inahusisha kufafanua utoaji masuala muhimu ya mradi, pamoja na kuunda mpango kamili wa kuongoza mradi kutoka mwanzo hadi mwisho. Dosari zilizobainika katika sehemu hii ni kama zifuatazo:-

7.2.1 Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa Hospitali ya Wilaya Mbuzini iliyopelekea ulipaji wa malipo ya ziada kwa mkandarasi ya jumla ya shilingi 271,491,678.94

Kifungu cha 45.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kati ya Wizara ya Afya na wakandarasi kinamtaka msimamizi wa mradi kupima thamani ya kazi inayotekelezwa. Vile vile, kifungu cha 45.4 cha mkataba huo kinahitaji thamani ya kazi inayotekelezwa kujumuisha thamani ya kiasi cha vitu katika Nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi iliyokamilishwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya 'vyeti vya Penultimate' kwa ajili ya ujenzi wa Hospital ya Wilaya Mbuzini na kulinganisha na vipimo vya kazi halisi iliofanyika eneo la ujenzi, Ukaguzi ulibaini uwepo wa malipo ya jumla ya shilingi 271,491,678.94 yaliyolipwa kwa mkandarasi kwa ajili ya kazi ambazo zilikua hazijatekelezwa.

Malipo hayo ya ziada yalisababishwa na kukosekana kwa vipimo vya pamoja baina ya Wizara ya Afya, mkandarasi na mshauri elekezi, ambapo ukaguzi ulibaini kuwa vipimo hivyo viliandaliwa na mkandarasi pekee bila ya uwepo wa Wizara ya Afya, ambapo Wizara ya Afya ilifanya zoezi la uthibitisho wa vipimo hivyo bila ya kufanya uhakiki wa upimaji.

Aidha, dosari katika maandalizi ya michoro ya miundo pamoja na (bar-bending schedule) ilikua ni miongoni mwa sababu zilizopelekea ongezeko katika malipo.

Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya Mbuzini ilikua ni miongoni mwa sababu iliyopelekea Wizara ya Afya kufanya malipo ya ziada kwa mkandarasi kwa kulinganisha na kazi halisi iliyofanywa hali hiyo imeipelekea Serikali kufanya matumizi yasiokuwa na tija.

Wizara ya Afya inapaswa kufanya upembuzi yakinifu wa kazi zote zilizofanywa kabla ya malipo ya mwisho kwa mkandarasi ili kuhakikisha malipo yanaendana na kazi halisi iliyofanyika kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba na kuhakikisha wanafanya uhakiki wa yote yanayolipwa kwa mkandarasi.

SURA YA NANE

8.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA CHUMBUNI

8.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 35: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Chumbuni

Kipengele	Taarifa za Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/EP-RNCT/2021/2022/01
Jina la Mkandarasi	M/s CRJE (EAST AFRICA) Limited
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	15 Disemba 2021
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	29 Disemba, 2021
Muda wa Mkataba	Miezi 6
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	28 Juni 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	30 Novemba, 2022
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tshs. 4,371,192,470.62 (pamoja na VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tshs. 6,249,427,064.11
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	100%
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	Tshs. 6,090,787,118.50

8.2 Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Upangaji wa Mipango ya Ujenzi wa Mradi wa Hospitali ya Wilaya Chumbuni

Sehemu hii inaelezea kuwa uanzishaji na upangaji wa Mradi ni hatua muhimu katika usimamizi wa mradi ili kuweza kupelekea mradi wenye mafanikio, zinahusisha mchanganuo wa upeo wa mradi, malengo ya mradi, wahusika waliohusika katika mradi pamoja na kuandaa mikakati stahiki ya kuweza kusimamia mradi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Huu hapa ni muhtasari wa awamu hizi mbili.

8.3 Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Mchakato wa kuwapata Wakandarasi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Chumbuni

Sehemu hii inaelezea yaliobainika katika mchakato wa kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chumbuni kama ilivyoelezwa hapa chini:

8.4 Matokeo ya Ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa Mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha utekelezaji wa mradi na kuridhika kwa wahusika. Inaelezea vipengele muhimu vya usimamizi wa mkataba mzuri na inasisitiza umuhimu wa mawasiliano ya wazi, nyaraka na kuzingatia masharti ya mkataba.

8.4.1 Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa Hospitali ya Wilaya Chumbuni iliyopelekea ulipaji wa malipo ya ziada kwa mkandarasi ya jumla ya shilingi 354,548,428.92

Kifungu cha 45.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kati ya Wizara ya Afya na wakandarasi kinamtaka msimamizi wa mradi kupima thamani ya kazi inayotekelezwa. Vile vile, kifungu cha 45.4 cha mkataba huo kinahitaji thamani ya kazi inayotekelezwa kujumuisha thamani ya kiasi cha vitu katika Nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi iliokamilishwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya vyeti vya 'Penultimate' kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chumbuni na kulinganisha na vipimo vya kazi halisi iliyofanyika eneo la ujenzi, Ukaguzi ulibaini uwepo wa malipo ya jumla ya shilingi 354,548,428.92 yaliyolipwa kwa mkandarasi kwa ajili ya kazi ambazo zilikua hazijatekelezwa.

Malipo hayo ya ziada yalisababishwa na kukosekana kwa vipimo vya pamoja baina ya Wizara ya Afya, mkandarasi na mshauri elekezi, ambapo ukaguzi ulibaini kuwa vipimo hivyo viliandaliwa na mkandarasi pekee bila ya uwepo wa Wizara ya Afya, ambapo Wizara ya Afya ilifanya zoezi la uthibitisho wa vipimo hivyo bila ya kufanya uhakiki wa upimaji.

Aidha, dosari katika maandalizi ya michoro ya miundo pamoja na (bar-bending schedule) ilikua ni miongoni mwa sababu zilizopelekea ongezeko katika malipo.

Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya Chumbuni ilikua ni miongoni mwa sababu iliopelekea Wizara ya Afya kufanya malipo ya ziada kwa mkandarasi kwa kulinganisha na kazi halisi iliyofanywa hali hiyo imeipelekea Serikali kufanya matumizi yasiokuwa na tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kufanya upembuzi yakinifu wa kazi zote zilizofanywa kabla ya malipo ya mwisho kwa mkandarasi ili kuhakikisha malipo yanaendana na kazi halisi iliofanyika kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba na kuhakikisha wanafanya uhakiki wa kazi zote zinazolipwa kwa mkandarasi.

SURA YA TISA

HOSPITALI YA WILAYA
UJITIMAI
DISTRICT HOSPITAL
Wizara ya Afya
ZANZIBAR
MAADHIMISHO YA MIAKA (60) YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
KARIBU KATIKA UFUNGUZI WA
HOSPITALI YA WILAYA YA MAGHARIBI B UJITIMAI
MKOA WA MJINI MAGHARIBI UNGUJA.
Mgeni Rasmi
Mhe. DR. AMANI ABEID KARUME
Rais Wa Zanzibar Na Mwenyekiti Wa Baraza La Mapinduzi Mstaafu
TAREHE 29.12.2023
OCAGZ

9.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA MAGOGONI

9.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 36: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Magogoni

Kipengele	Taarifa za Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/EP-RNCT/2021/2022/01-LOT 2
Jina la Mkandarasi	M/s CRJE (EAST AFRICA) Limited
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	15 Disemba 2021
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	23 Disemba, 2021
Muda wa Mkataba	miezi 6
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	22 Juni 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	-
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 4,506,763,920.74 (Pamoja na VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 6,462,697,552.00
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	100%
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	Tzs 6,301,300,228.68

9.2 Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Upangaji wa Mipango ya Ujenzi wa Mradi wa Hospitali ya Wilaya Magogoni

Sehemu hii inaelezea kuwa uanzishaji na upangaji wa Mradi ni hatua muhimu katika usimamizi wa mradi ili kuweza kupelekea mradi wenye mafanikio ambapo inahusisha mchanganuo wa upeo wa mradi, malengo ya mradi, wahusika waliohusika katika mradi, pamoja na kuandaa mikakati stahiki ya kuweza kusimamia mradi kuanzia mwanzo hadi mwisho kama inavyoonekana katika muhtasari hapo chini:-

9.3 Matokeo ya Ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa Mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha utekelezaji wa mradi na kuridhika kwa wahusika. Inaelezea vipengele muhimu vya usimamizi wa mkataba mzuri na inasisitiza umuhimu wa mawasiliano ya wazi, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba.

9.3.1 Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa Hospitali ya Wilaya Magogoni iliyopelekea ulipaji wa malipo ya ziada kwa mkandarasi ya jumla ya shilingi 300,432,261.57

Kifungu cha 45.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kati ya Wizara ya Afya na wakandarasi kinamtaka msimamizi wa mradi kupima thamani ya kazi inayotekelezwa. Vile vile, kifungu cha 45.4 cha mkataba huo kinahitaji thamani ya kazi inayotekelezwa kujumuisha thamani ya kiasi cha vitu katika Nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi iliyokamilishwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya vyeti vya 'Penultimate' kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Magogoni na kulinganisha na vipimo vya kazi halisi iliofanyika eneo la ujenzi. Ukaguzi ulibaini uwepo wa malipo ya jumla ya shilingi 344,102,307.52 yaliolipwa kwa mkandarasi kwa ajili ya kazi ambazo zilikua hazijatekelezwa kama inavyoainishwa katika.

Malipo hayo ya ziada yalisababishwa na kukosekana kwa vipimo vya pamoja baina ya Wizara ya Afya, mkandarasi na mshauri elekezi, ambapo Ukaguzi ulibaini kuwa vipimo hivyo viliandaliwa na mkandarasi pekee bila ya uwepo wa Wizara ya Afya, ambapo Wizara ya Afya ilifanya zoezi la uthibitisho wa vipimo hivyo bila ya kufanya uhakiki wa upimaji.

Aidha, dosari katika maandalizi ya michoro ya miundo pamoja na 'bar-bending schedule' ilikua ni miongoni mwa sababu zilizopelekea ongezeko katika malipo.

Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya Magogoni ilikua ni miongoni mwa sababu iliopelekea Wizara ya Afya kufanya malipo ya ziada kwa mkandarasi kwa kulinganisha na kazi halisi iliofanywa hali hiyo imeipelekea Serikali kufanya matumizi yasiokuwa na tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya upembuzi yakinifu wa kazi zote zilizofanywa kabla ya malipo ya mwisho kwa mkandarasi ili kuhakikisha malipo yanaendana na kazi halisi iliofanyika kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba na kuhakikisha wanafanya uhakiki wa yote yanayolipwa kwa mkandarasi.

HOSPITALI YA WILAYA
KIVUNGE
DISTRICT HOSPITAL
MIAKA MITATU (3) YA MAFANIKIO YA MHE. DK. HUSSEIN ALI MWINYI
KARIBU KATIKA UZINDUZI WA
HOSPITALI YA WILAYA KIVUNGE
WILAYA YA KASKAZINI A, MKOA WA KASKAZINI UNGUJA
TAREHE: 23.10.2023
MHE. DK. HUSSEIN ALI MWINYI

SURA YA KUMI


SIEMENS
Healthineers
SOMATOM go.Top

10.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA KIVUNGE

10.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 37: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kivunge

Kipengele	Habari katika ya Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/E-RNCT/2021/2022/01-LOT 5
Jina la Mkandarasi	Mazrui Building Contractors Limited
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	15 Disemba 2021
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	23 Disemba, 2021
Muda wa Mkataba	Miezi 6
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	22 Juni 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	31 Oktoba, 2022
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 4,854,044,141.93 (Pamoja na VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 5,537,226,034.48
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	100%
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	Tzs 5,400,495,064.55

10.2 Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Mchakato wa kuwapata Wakandarasi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kivunge

Sehemu hii inaelezea yaliobainika katika mchakato wa kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kivunge kama ilivyoelezwa hapa chini:-

10.2.1 Ongezeko la Bei ya Mkataba la jumla ya shilingi 358,184,377 kutokana na Utoaji wa Mkataba kwa mzabuni asie na sifa

Kanuni ya 127 ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inamtaka mzabuni mwenye zabuni iliyotathminiwa vizuri kuwa mzabuni aliyefanikiwa. Kupitia mapitio ya ripoti ya tathmini ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kivunge, Ukaguzi ulibaini kwamba baada ya tathmini, kampuni ya M/s WCEL Limited ndio ilikua na vigezo vya kuzawadiwa tuzo na kamati ya tathmini ili pendekeza tuzo itolewe kwa mzabuni M/s WCEL Limited kwa mkataba wa jumla ya shilingi 4,495,819,763.50.

Katika kufanya mapitio ya hadidu rejea za kumbukumbu za kikao cha mapatano, ilibainisha kuwa, tarehe 14 Disemba 2021, Wizara ya Afya ilifanya kikao cha mapatano na kampuni ya M/S Mazrui Building Contractors kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kivunge kwa gharama za shilingi 4,854,044,141.94 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa tarehe 15 Disemba 2021, Wizara ya Afya kupitia dokezo lenye kumbukumbu nambari AB/42/333/2021/22/118 ilitoa taarifa ya tuzo kwa Mzabuni Mazrui Building Contractors kwa thamani ya shilingi 4,854,044,141.93 pamoja na VAT.

Utoaji wa tuzo kwa mzabuni ambae hakupendekezwa na kamati ya tathmini kumepelekea ongezeko la shilingi 358,184,377 katika bei ya mkataba (4,854,044,141 – 4,495,819,763). Mchanganuo bei unaonekana katika jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 38: Mzabuni aliezawadiwa bila ya kuwa vigezo

Jina la Hospitali ya Wilaya	Mzabuni aliyependekezwa na kamati ya tathmini		Mzabuni aliezawadiwa Tuzo		Tofauti (Tsh)
	Jina la mzabuni	Kiasi (Tsh)	Jina la mzabuni	Kiasi katika (Tsh)	
Kivunge	Ms/ WCEL	4,495,819,763.50	M/S Mazrui Building Contractors	4,854,044,141	358,184,377

Chanzo: Ripoti ya tathmini, hadidu rejea za bodi ya zabuni na mkataba

Jadweli hapo juu , linaonesha ongezeko la kiasi cha shilingi 358,000,000 katika ujenzi wa Hospitali ya Kivunge lililosababishwa na kumzawadia tuzo mkandarasi ambae hakufikia vigezo kwa mujibu wa ripoti ya tathmini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unazingatia ushauri unaotolewa na Kamati ya Tathmini ili kuepusha kuongezeka kwa gharama za ujenzi na kuingiza hasara Serikali.

10.3 Matokeo ya Ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa Mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha utekelezaji wa mradi na kuridhika kwa wahusika. Inaelezea vipengele muhimu vya usimamizi wa mkataba mzuri na inasisitiza umuhimu wa mawasiliano ya wazi, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba.

10.3.1 Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa Hospitali ya Wilaya Kivunge iliyopelekea ulipaji wa malipo ya ziada kwa mkandarasi ya jumla ya shilingi 115,067,133.41

Kifungu cha 45.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kati ya Wizara ya Afya na wakandarasi kinamtaka msimamizi wa mradi kupima thamani ya kazi inayotekelezwa. Vile vile, kifungu cha 45.4 cha mkataba huo kinahitaji thamani ya kazi inayotekelezwa kujumuisha thamani ya kiasi cha vitu katika Nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi iliokamilishwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya 'vyeti vya Penultimate' kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kivunge na kulinganisha na vipimo vya kazi halisi iliofanyika eneo la ujenzi. Ukaguzi ulibaini uwepo wa malipo ya jumla ya shilingi 115,067,133.41 yaliolipwa kwa mkandarasi kwa ajili ya kazi ambazo zilikua hazijatekelezwa.

Malipo hayo ya ziada yalisababishwa na kukosekana kwa vipimo vya pamoja baina ya Wizara ya Afya, mkandarasi na mshauri elekezi, ambapo ukaguzi ulibaini kuwa vipimo hivyo viliandaliwa na mkandarasi pekee bila ya uwepo wa Wizara ya Afya, ambapo Wizara ya Afya ilifanya zoezi la uthibitishaji wa vipimo hivyo bila ya kufanya uhakiki wa upimaji.

Aidha, dosari katika maandalizi ya michoro ya miundo pamoja na 'bar-bending schedule' ilikua ni miongoni mwa sababu zilizopelekea ongezeko katika malipo.

Dosari katika ufanyaji wa tathmini ya kazi iliyofanywa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kivunge ilikua ni miongoni mwa sababu iliyopelekea Wizara ya Afya kufanya malipo ya ziada kwa mkandarasi kwa kulinganisha na kazi halisi iliyofanywa imepelekea Serikali kufanya matumizi yasiokuwa na tija.

Wizara ya Afya inapaswa kufanya upembuzi yakinifu wa kazi zote zilizofanywa kabla ya malipo ya mwisho kwa mkandarasi ili kuhakikisha malipo yanaendana na kazi halisi iliofanyika kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba na kuhakikisha wanafanya uhakiki wa yote yanayolipwa kwa mkandarasi.

SURA YA KUMI NA MOJA

11.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA PANGATUPU

11.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 39: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Pangatupu

Vipengee	Taarifa za Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/EP-NCT/2021/2022/01-LOT 4
Jina ya ya Mkandarasi	M/s CRJE (EAST AFRICA) Limited
Tarehe ya Mkataba	15 Disemba 2021
Tarehe ya kuanza kazi	23 Disemba, 2021
Muda wa Mkataba	Miezi 6
Tarehe ya awali ya Kukamilika kazi	22 Juni 2022
Tarehe ya mapitio ya Kukamilika kazi	31 Disemba, 2022
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 4,478,584,782 (Pamoja na VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 6,115,992,730
Maendeleo ya Kazi (%) kwa mwezi wa Julai, 2023	100%
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	Tzs 6,115,992,730.09

11.2 Matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha mradi unatekelezeka kwa ufanisi kuweza kuwanufaisha wahusika. Inaelezea mambo muhimu ya usimamizi wa mkataba na kushajihisha umuhimu wa mawasiliano, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba, gharama, wakati na ubora.

11.2.1 Tathmini isiyoridhisha ya kazi iliyofanywa kwa Hospitali ya Wilaya ya Pangatupu kiasi cha shilingi 472,350,459.25

Kifungu cha 45.3 cha masharti ya jumla (General Conditions) baina ya Wizara ya Afya na mkandarasi kinamtaka msimamizi wa mradi kutathmini thamani ya kazi iliyotekelezwa. Aidha, kifungu cha 45.4 cha mkataba huo kinahitaji thamani ya kazi iliyotekelezwa kujumuisha thamani ya vifaa vilivyotumika katika BoQ.

Kupitia Ukaguzi wa vyeti vya 'Penultimate' za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Pangatupu pamoja na vipimo vilivyofanywa na Timu ya ukaguzi kwa kutumia michoro ya ujenzi, ukaguzi ulibaini tofauti baina ya fedha zilizolipwa kwa mujibu wa 'Penultimate Certificates' dhidi ya kazi halisi iliofanyika kwa mujibu wa vipimo vilivyofanywa na timu ya ukaguzi, ambapo ukaguzi ulibaini jumla shilingi 472,350,459.25 zililipwa kama ziada na kupelekea uwepo wa tofauti ya fedha baina ya vyeti vya 'Penultimate' na marejeo ya vipimo yaliofanywa na Timu ya ukaguzi kwa baadhi ya maeneo ya ujenzi ambayo yaliainisha tofauti ya jumla ya shilingi 472,350,459.25.

Malipo hayo ya ziada yalisababishwa na Wizara ya Afya kushindwa kufanya marudio ya vipimo vya pamoja na mkandarasi na mshauri elekezi, ambapo Ukaguzi ulibaini kuwa marudio ya vipimo hivyo yalifanywa na mkandarasi pamoja na Wizara ya Afya kuweza kuthibitisha bila ya uwepo wa mshauri elekezi wa Wizara, aidha malipo kwa ujenzi wa hosptitali ya Pangatupu yalifanyika kwa kuzingatia asilimia ya vifaa vinavyohitajika kwa mujibu wa mkataba bila ya kuzingatia kazi halisi iliofanyika, ambapo malipo yaliolipwa yameibainika kuwa ni makubwa kulinganisha na kazi halisi iliofanyika, aidha ukosefu wa michoro ya miundo (structural drawing) na 'bar bending schedule' nayo ni miongoni mwa sababu zilizopelekea utofauti uliobainika.

Tathmini isiyoridhisha ya kazi iliofanyika kwa ujenzi wa Hospitali ya Pangatupu imepelekea kufanyika kwa malipo ya ziada kwa mkandarasi ambayo hakustahiki kulipwa na kuisababishia Serikali kufanya matumizi yasio na lazima.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya mapitio ya kazi halisi iliofanyika kabla ya kufanya malipo ya mwisho kwa mkandarasi kuweza kuhakikisha kwamba malipo yote yanafanyika kwa mujibu wa kazi halisi iliofanywa kama ilivyoainishwa katika mkataba na kuondoa malipo ya ziada.

SURA YA KUMI NA MBILI

12.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA VITONGOJI

12.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 40: Taarifa za Mkataba za Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Vitongoji

Vipengele	Taarifa za Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/EP-RNCT/2021/2022/01-LOT 10
Jina la Mkandarasi	M/s Salem Construction Limited
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	15 Disemba 2021
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	2 Januari, 2021
Muda wa Mkataba	Miezi 6
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	2 Julai 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	-
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 5,038,669,138.75 (Pamoja na VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 7,026,403,630.85
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	100%
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	Tzs 6,850,743,540.08

12.2 Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na mchakato wa kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya Vitongoji

Sehemu inaelezea yaliobainika wakati wa Ukaguzi wa mchakato wa kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya Vitongoji.

12.2.1 Ongezeko la Bei ya Mkataba la jumla ya shilingi 76,802,198 linalotokana na Utoaji wa Mkataba kwa mzabuni asio na vigezo

Kanuni ya 127 ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, 2020 inamtaka mzabuni mwenye zabuni iliyotathminiwa vizuri kuwa mzabuni aliyefanikiwa.

Kupitia mapitio ya ripoti ya tathmini ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Vitongoji, Ukaguzi ulibaini kwamba baada ya tathmini kampuni ya M/s Group Six Construction Limited ndio ilikua na vigezo vya kuzawadiwa tuzo na kamati ya tathmini ilipendekeza tuzo itolewe kwa mzabuni M/s Group Six Construction Limited kwa shilingi 4,961,866,940.

Katika kufanya mapitio ya kumbukumbu za kikao cha mapatano, ilibainisha kua, tarehe 14 Disemba 2021, Wizara ya Afya ilifanya kikao cha mapatano na kampuni ya M/S Salem Construction Limited kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Vitongoji kwa gharama za shilingi 5,038,669,138 pamoja na kodi ya Ongezeko la thamani.

Aidha, Ukaguzi ulibaini kuwa tarehe 14 Disemba 2021, Wizara ya Afya kupitia dokezo lenye kumbukumbu nambari AB/42/333/2021/22/123 ilitoa taarifa ya tuzo kwa M/S Salem Construction Limited kwa thamani ya shilingi 5,038,669,138 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Utoaji wa tuzo kwa mzabuni ambae hakupendekezwa na kamati ya tathmini kumepelekea ongezeko la jumla ya shilingi 76,802,198 katika bei ya mkataba, mchanganuo unaonekana katika jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 41 : Mchanganuo wa Mzabuni aliezawadiwa bila ya kuwa na vigezo

Jina la Hospitali ya wilaya	Mzabuni aliyependekezwa na kamati ya tathmini		Mzabuni aliezawadiwa Tuzo		Tofauti (Tzs)
	Jina	Kiasi (TZS)	Jina	Kiasi (Tzs)	
Vitongoji	Group Six Costruction Limited	4,961,866,940	M/S Salem Constrution Limited	5,038,669,138	76,802,198

Chanzo: Ripoti ya tathmini na kumbukumbu za bodi ya zabuni na mkataba

Jadweli hapo juu linaainisha ongezeko la kiasi cha shilingi 76,802,198 katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Vitongoji lililosababishwa na kumzawadia tuzo mkandarasi ambae hakufikia vigezo kwa mujibu wa ripoti ya tathmini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unazingatia mapendekezo yanayotolewa na kamati ya tathmini ili kunusuru kujitokeza kwa ongezeko la gharama jambo ambalo linaweza kupelekea kuingiza hasara Serikali.

12.3 Matokeo ya Ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa Mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha mradi unatekelezeka kwa ufanisi kuweza kuwanufaisha wahusika. Inaelezea mambo muhimu ya usimamizi wa mkataba na kushajihisha umuhimu wa mawasiliano, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba, gharama, wakati na ubora.

12.3.1 Tathmini isioridhisha ya kazi iliyofanywa kwa Hospitali ya Wilaya Vitongoji na kupelekea ongezeko la shilingi 183,744,003.80

Kifungu cha 45.3 cha masharti ya jumla ya mkataba (General Conditions of contract) baina ya Wizara ya Afya na mkandarasi kinamtaka msimamizi wa mradi kutathmini thamani ya kazi iliyotekelezwa. Aidha, kifungu cha 45.4 cha mkataba huo kinahitaji thamani ya kazi iliyotekelezwa kujumuisha thamani ya vifaa vilivyotumika katika nyaraka ya makisio ya ujenzi (BoQ).

Kupitia Ukaguzi wa vyeti vya 'Penultimate' vya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Vitongoji pamoja na vipimo vilivyofanywa na Timu ya Ukaguzi kwa kutumia nyaraka ya makisio ya ujenzi. Ukaguzi ulibaini tofauti baina ya fedha zilizolipwa kwa mujibu wa 'Penultimate Certificates' dhidi ya kazi halisi iliofanyika kwa mujibu wa vipimo vilivyofanywa na timu ya Ukaguzi, ambapo jumla shilingi 183,744,003.80 zililipwa kama ziada, na kupelekea tofauti ya fedha baina ya vyeti vya 'Penultimate' na marejeo ya vipimo yaliofanywa na Timu ya Ukaguzi kwa baadhi ya maeneo ya ujenzi ambayo yaliainisha tofauti ya jumla ya shilingi 183,744,003.80.

Malipo hayo ya ziada yalisababishwa na Wizara ya Afya kushindwa kufanya marudio ya vipimo vya pamoja na mkandarasi na mshauri elekezi, ambapo Ukaguzi ulibaini kuwa marudio ya vipimo hivyo yalifanywa na mkandarasi pamoja na Wizara ya Afya kuweza kuthitisha bila ya uwepo wa mshauri elekezi wa Wizara.

Ukaguzi ulibaini malipo kwa ujenzi wa hosptitali ya Vitongoji yalifanyika kwa kuzingatia asilimia ya vifaa vinavyohitajika kwa mujibu wa mkataba bila ya kuzingatia kazi halisi iliofanyika, ambapo malipo yaliolipwa yamebainika kuwa ni makubwa kulinganisha na kazi halisi iliofanyika, aidha ukosefu wa michoro ya miundo (structural drawing) na (bar bending schedule) nayo ni miongoni mwa sababu zilizopelekea utofauti uliobainika.

Tathmini isioridhisha ya kazi iliofanyika kwa ujenzi wa Hospitali ya Vitongoji imepelekea kufanyika kwa malipo ya ziada kwa mkandarasi ambayo hayakustahiki kulipwa na hatimae kuisababishia Serikali kufanya matumizi yasiokua ya lazima.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kufanya mapitio ya kazi halisi iliofanyika kwa mujibu wa mkataba kabla ya kufanya malipo ya mwisho kwa mkandarasi ili kuepuka kujitokeza kwa malipo ya kazi za ziada.

SURA YA KUMI NA TATU

13.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA MICHEWENI

13.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 42: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Micheweni

Vipengele	Taarifa za Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/EP-RNCT/2021/2022/01-Mengi 9
Jina la Mkandarasi	M/s Benchmark Engineering Company Limited
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	15 Disemba 2021
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	3 Januari, 2021
Muda wa Mkataba	Miezi 6
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	2 Julai, 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	20 Novemba, 2022
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 4,800,212,161.80 (Thamani VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 6,366,485,503
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	100%
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	Tzs 6,366,485,502.82

13.2 Matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha mradi unatekelezeka kwa ufanisi kuweza kuwanufaisha wahusika. Inaelezea mambo muhimu ya usimamizi wa mkataba na kushajihisha umuhimu wa mawasiliano, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba, gharama, wakati na ubora.

13.2.1 Tathmini isioridhisha ya kazi iliyofanywa kwa Hospitali ya Wilaya Micheweni na kupelekea kuwepo kwa ongezeko la shilingi 240,943,966.90

Kifungu cha 45.3 cha masharti ya jumla ya Mkataba (GCC) baina ya Wizara ya Afya na mkandarasi kinamtaka msimamizi wa mradi kutathmini thamani ya kazi iliyotekelezwa. Aidha, kifungu cha 45.4 cha mkataba huo kinahitaji thamani ya kazi iliyotekelezwa kujumuisha thamani ya vifaa vilivyotumika katika BoQ.

Kupitia Ukaguzi wa vyeti vya 'Penultimate' za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Micheweni pamoja na vipimo vilivyofanywa na Timu ya Ukaguzi kwa kutumia michoro ya ujenzi, Ukaguzi ulibaini tofauti baina ya fedha zilizolipwa kwa mujibu wa Penultimate certificates dhidi ya kazi halisi iliofanyika kwa mujibu wa vipimo vilivyofanywa na timu ya ukaguzi, ambapo ukaguzi ulibaini jumla shilingi 240,943,966.90 zililipwa kama ziada na kupelekea uwepo wa tofauti ya fedha baina ya vyeti vya Penultimate na marejeo ya vipimo yaliyofanywa na timu ya ukaguzi kwa baadhi ya maeneo ya ujenzi ambayo yaliainisha tofauti ya jumla ya shilingi 240,943,966.90

Malipo hayo ya ziada yalisababishwa na Wizara ya Afya kushindwa kufanya marudio ya vipimo vya pamoja na mkandarasi na mshauri elekezi wa Wizara ambapo ukaguzi ulibaini kuwa marudio ya vipimo hivyo yalifanywa na mkandarasi pamoja na Wizara ya Afya na kuweza kuthibitishwa bila ya uwepo wa mshauri elekezi, aidha malipo kwa ujenzi wa Hospitali Micheweni yalifanyika kwa kuzingatia asilimia ya vifaa vinavyohitajika kwa mujibu wa mkataba bila ya kuzingatia kazi halisi iliyofanyika, ambapo malipo yaliyolipwa yamebainika kuwa ni makubwa ukilinganisha na kazi halisi iliyofanyika, aidha ukosefu wa michoro ya miundo (structural drawing) na (bar bending schedule) nayo ni miongoni mwa sababu zilizopelekea uwepo wa tofauti hiyo.

Tathmini isioridhisha ya kazi iliofanyika kwa ujenzi wa Hospitali ya Micheweni imepelekea kufanyika kwa malipo ya ziada kwa mkandarasi ambayo hakustahiki kulipwa na kuisababishia Serikali kufanya matumizi yasio na lazima.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kufanya mapitio ya kazi halisi iliyofanyika kabla ya kufanya malipo ya mwisho kwa mkandarasi kuweza kuhakikisha kwamba malipo yote yanafanyika kwa mujibu wa kazi halisi iliyofanywa kama ilivyoainishwa katika mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa malipo ya ziada.

13.2.2 Malipo ya ziada ya shilingi 20,000,000 kwa ajili ya Bima na Dhamana ya kazi

Kifungu 14.1 cha masharti ya jumla ya mkataba kati ya Wizara ya Afya na mkandarasi kinamtaka mkandarasi kutoa kwa majina ya pamoja ya Mwajiri na mkandarasi, bima ya kuanzia tarehe ya kuanza hadi mwisho wa Kipindi cha Dhamana kwa kiasi kilichotajwa katika Masharti maalum ya mkataba kwa matukio yafuatayo ambayo ni kutokana na hatari za mkandarasi; (a) Kupoteza au kuharibu kazi, mimea na vifaa (b) Kupoteza au uharibifu wa Vifaa (c) Kupoteza au uharibifu wa mali (isipokuwa kazi, mimea, zana na vifaa) kuhusiana na mkataba na (d) kuumia kwa mtu au kifo.

Aidha, kifungu cha 55.1 cha masharti ya jumla ya mkataba baina ya Wizara ya Afya na Mkandarasi kinahitaji dhamana ya utendaji kazi iwasilishwe kwa mwajiri kabla ya tarehe iliyoainishwa katika barua ya kukubali tuzo na inapaswa kutolewa kwa kiasi na fomu na benki au dhamana inayokubalika kwa mwajiri. Dhamana ya utendaji kazi inapaswa kuwa halali hadi siku 28 kabla ya utolewaji wa cheti cha kukamilka kwa kazi ikiwa ni kwa njia ya dhamana ya kibenki na kwa upande wa dhamana ya utendaji italazimu kutumika hadi kwa kipindi cha mwaka mmoja baada ya kukabidhishwa kwa cheti cha kukamilika kwa kazi.

Ukaguzi ulipitia vyeti vya ‘Penultimate’ pamoja na makisio ya gharama za ujenzi (BoQ) kama ilivyoainishwa katika mkataba na kubaini kuwa Wizara ya Afya ilifanya malipo kwa ajili ya Bima ya vihatarishi wakati wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Micheweni ambapo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba Wizara ya Afya haikupaswa kufanya malipo hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya malipo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma, aidha kuhakikisha fedha yote iliyolipwa kinyume na utaratibu (shilingi 20,000,000) inarudishwa Serikalini.

SURA YA KUMI NA NNE

14 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA KINYASINI

14.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya imeweza kusimamia mipango yake, masuala ya ununuzi, ujenzi na fedha za mradi wakati wa ujenzi wa hospitali za Unguja na Pemba. Fedha hizo zilielekezwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda Wizara ya Afya.

Jadweli Nambari 43: Maelezo ya Mkataba wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kinyasini

Vipengele	Maelezo za Mkataba
Nambari ya Mkataba	SMZ/IMF/H03/W/EP-RNCT/2021/2022/01-LOT 8
Jina la Mkandarasi	M/s Group six International Limited
Tarehe ya kusainiwa Mkataba	15 Disemba, 2021
Muda unaotakiwa kuanza Ujenzi	3 Januari, 2021
Muda wa Mkataba	Miezi 6
Muda halisi wa kumaliza Mkataba	2 Julai, 2022
Muda wa Mapitio wa kumaliza Mkataba	31 Januari, 2023
Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 4,976,732,967.75 (Pamoja na VAT)
Mapitio ya Gharama za awali pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT)	Tzs 6,395,633,033.24
Kazi inayoendelea (%) mpaka Julai, 2023	100
Malipo yaliyofanyika (%) mpaka Julai 2023 wakati Ukaguzi unafanyika	Tzs 5,921,397,576.51

14.2 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usimamizi wa Ununuzi katika Ujenzi wa Miradi ya Hospitali

Sehemu hii inatoa muhtasari na utangulizi wa mchakato wa ununuzi wa mradi. Ununuzi ni sehemu muhimu ya usimamizi wa mradi ambayo inahusisha kupata bidhaa, huduma, na rasilimali zinazohitajika ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi. Ripoti hii inaelezea dhana muhimu, hatua, na mambo yanayohusika katika mchakato wa ununuzi wa mradi.

14.2.1 Dosari katika ufanyaji wa marekebisho ya makosa wakati wa tathmini ya zabuni iliopelekea ongezeko la jumla ya shilingi 90,829,909 la bei ya mkataba

Kanuni ya 123 (2) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020, Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma itasahihisha makosa ya hesabu wakati wa tathmini ya zabuni.

Ukaguzi ulipitia mchakato wa zabuni ya ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya iliyopo Kinyasini, Wete - Pemba, na kubaini bei ya mzabuni M/S Group Six International Ltd ilikuwa ni jumla ya shilingi 4,976,732,967.75 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Aidha, ukaguzi ulifanya mapitio ya ripoti ya tathmini na kubainisha kuwa kamati ya tathmini ilisahihisha kiasi cha zabuni cha M/S Group Six International na bei mpya ya zabuni baada ya marekebisho ya hesabu ilikuwa ni jumla ya shilingi 4,968,862,344.75.

Ukaguzi ulipofanya mapitio ya hesabu ya zabuni ya mzabuni M/S Group Six International Ltd ilibaini kuwa gharama halisi za mkataba zilitakiwa kuwa ni jumla ya shilingi 4,878,032,435.28 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Mchanganuo unaonekana katika jadweli hapo chini.

Jadweli Nambari 44: Marekebisho ya makosa wakati wa tathmini ya zabuni

Vipengele	Mchanganuo wa Kamati ya Tathmini (Tshs.)	Mchanganuo wa Timu ya Ukaguzi (Tshs.)	Tofauti (Tshs.)
Preliminaries	100,000,000	100,000,000	-
Main Building	2,742,145,958	2,743,369,528	1,223,570
Other Building	747,603,907	747,597,807	(6,100)
Provisional and P.C Sums	554,000,000	482,000,000	(72,000,000)
Contingency	150,000,000	150,000,000	-
Insurance against injury to persons	15,000,000	2,200,000	(12,800,000)
Insurance against injury to property	10,000,000	2,200,000	(7,800,000)
Insurance against damages arising without negligence	2,000,000.00	4,200,000.00	2,200,000
Conditions of contract clause 51	-	2,200,000.00	2,200,000
conditions of contract clause 52	-	8, 000,000.00	8,000,000
Jumla ndogo	**4,320,749,865**	**4,241,767,335**	**(78,982,530)**
Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) (15%)	**648,112,479**	**636,265,100**	**(11,847,379)**
Jumla Kuu	**4,968,862,345**	**4,878,032,435**	**(90,829,909)**

Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi juu ya ripoti ya tathmini na uwasilishaji wa zabuni ya mkandarasi aliyepewa, 2023

Jadweli hapo juu linaonyesha dosari zilizofanywa na timu ya tathmini kwa kushindwa kufanya tathmini kwa mujibu wa kanuni za manunuzi za 2020.

Matokeo yake, ilipelekea kuongezeka kwa jumla ya shilingi 90,829,909 katika bei ya mkataba kutokana na marekebisho yaliyofanyika wakati wa tathmini. Hali hii ilisababishwa na kushindwa kuifanyia mapitio ripoti ya tathmini na kitengo cha ununuzi kabla ya kuwasilishwa kwa bodi ya zabuni kwa ajili ya idhini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba inaweka udhibiti ambao unahitaji kitengo cha ununuzi kufanya mapitio ya kina ya ripoti ya tathmini kabla ya kuwasilishwa kwa Bodi ya zabuni kwa kuidhinishwa.

14.2.2 Tofauti iliobainika baina ya bei ya zabuni na bei ya mkataba ya jumla ya shilingi 19,830,623

Ukaguzi ulibaini kwamba Wizara ya Afya kupitia dokezo la tarehe 14 Disemba, 2021 yenye kumbukumbu nambari AB/42/333/2021/22/21 ilitoa dokezo la kumtaarifu mkandarasi Ms.Group Six International Limited kuhusiana na lengo la kumzawadia zabuni ya ujenzi wa Hospitali ya wilaya Kinyasini - Wete Pemba.

Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Afya iliingia makubaliano ya mkataba na mkandarasi M/s Group Six International Limited kupitia mkataba nambari SMZ/H03/W/EP-RNCT/2021-2022/01 Lot 8 mkataba ambao ulikua na ongezeko la jumla ya shilingi 19,830,623 kwa kulinganisha na bei ya zabuni iliyoidhinishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa bei ya Tuzo inalingana na bei iliopendekezwa na kamati ya tathmini na kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.

14.3 Matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa mkataba

Sehemu hii inatoa matokeo yaliyojumuishwa kuhusu usimamizi wa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Inatoa muhtasari wa mchakato wa usimamizi wa mkataba wa mradi, ikionyesha umuhimu wake katika kuhakikisha mradi unatekelezeka kwa ufanisi kuweza kuwanufaisha wahusika. Inaelezea mambo muhimu ya usimamizi wa mkataba na kushajihisha umuhimu wa mawasiliano, nyaraka, na kuzingatia masharti ya mkataba, gharama, wakati na ubora.

14.3.1 Tathmini isioridhisha ya kazi iliyofanywa kwa Hospitali ya Wilaya Kinyasini-Wete Pemba kiasi cha jumla ya shilingi 149,548,548.57

Kifungu cha 45.3 cha masharti ya jumla ya Mkataba (GCC) baina ya Wizara ya Afya na mkandarasi kinamtaka msimamizi wa mradi kutathmini thamani ya kazi iliyotekelezwa. Aidha, kifungu cha 45.4 cha mkataba huo kinahitaji thamani ya kazi iliyotekelezwa kujumuisha thamani ya vifaa vilivyotumika katika BoQ.

Kupitia ukaguzi wa vyeti vya 'Penultimate' za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kinyasini pamoja na vipimo vilivyofanywa na timu ya ukaguzi kwa kutumia gharama za makisio ya ujenzi, ukaguzi ulibaini tofauti baina ya fedha zilizolipwa kwa mujibu wa 'Penultimate Certificates' dhidi ya kazi halisi iliofanyika kwa mujibu wa vipimo vilivyofanywa na timu ya ukaguzi, ambapo ukaguzi ulibaini jumla shilingi 149,548,548.57 zililipwa kama ziada.

Malipo hayo ya ziada yalisababishwa na Wizara ya Afya kushindwa kufanya marudio ya vipimo vya pamoja na mkandarasi na mshauri elekezi, ambapo Ukaguzi ulibaini kuwa marudio ya vipimo hivyo yalifanywa na mkandarasi pamoja na Wizara ya Afya kuweza kuthibitisha bila ya uwepo wa mshauri elekezi wa Wizara.

Ukaguzi umebaini malipo kwa ujenzi wa Hospitali ya Kinyasini yalifanyika kwa kuzingatia asilimia ya vifaa vinavyohitajika kwa mujibu wa mkataba bila ya kuzingatia kazi halisi iliofanyika, ambapo malipo yaliolipwa yameibainika kuwa ni makubwa kulinganisha na kazi halisi iliofanyika, aidha ukosefu wa michoro ya miundo (structural drawing) na 'bar bending schedule' nayo ni miongoni mwa sababu zilizopelekea utofauti uliobainika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya uhakiki wa kazi halisi iliyofanyika kabla ya kufanya malipo ya mwisho ili kuepusha kufanyika kwa malipo ya kazi ambazo hazijafanyika.

VIAMBATISHO

Kiambatisho Nambari 1: Usajili wa Wataalamu kutoka nje ya nchi katika ERB

Namba	Mkandarasi	Wataalamu kutoka Nje	Kiasi cha Bei ya Kibali (Tsh)
1.	M/S ESTIM Construction	Naran Varsan	3,231,500
2.		Padma Kumar	NA
3.		Yagdish Vekariya	3,231,500
4.	CRJE	Su Yu	3,231,500
5.		Liu Yumeng	3,231,500
6.		Zhao Yubin	NA
7.		Gratiania Rukibaril	NA
8.		Liu Wei	NA
9.		Zhang Mshindo	NA
10.		Shi Yan	3,231,500
Jumla			**16,157,500**

Kiambatisho Nambari 2: Malipo yaliofanyika kwa kazi ambazo hazijatekelezwa

Namba	Maelezo	Gharama (Tsh)
1.	Addition Work	59,800,000
2.	Frame	34,032,000
3.	Walling	79,874,500
4.	Roofing + Rain Water	523,000
5.	Finishes	47,820,000
6.	Painting & Decorations	8,322,000
7.	Emergency And Administration block	7,525,000
Jumla		**237,896,500**

OFFICE OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ZANZIBAR OCAGZ

Kiambatisho Nambari 3: Malipo yaliofanyika kwa kazi ambazo hazijatekelezwa

Namba	Maelezo	Gharama (Tzs)
1.	Foundation	96,228,196.52
2.	Female Ward	96,956,739.08
3.	Emergency and Administration	41,171,892.28
4.	Male Ward	22,215,173.13
5.	OPD And Laboratory	34,092,804.49
6.	Mortuary Building	53,437,502.02
Jumla		**344,102,307.52**